

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Saba – Tarehe 13 Septemba, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae!

Tunaendelea na Mkutano wetu wa Nane, Kikao cha Saba.

Katibu!

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Maelezo ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Kuhusu Muswada wa Sheria ya Reli wa mwaka 2017 *(The Railways Bill, 2017)*.

MHE. RASHID M. CHUACHUA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:

Maoni ya Kamati ya Miundombinu Kuhusu Muswada wa Sheria ya Reli wa mwaka 2017 *(The Railways Bill, 2017)*.

MHE. QAMBALO W. QULWI - NAIBU MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGE KWA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Maoni ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani Juu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Kuhusu Muswada wa Sheria ya Reli wa mwaka 2017 (*The Railways Bill, 2017*).

SPIKA: Katibu!

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI: Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Swali la kwanza litaelekezwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Nalo litaulizwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kule Mpwapwa wanamuita Mwaha.

Na. 82

Uanzishwaji wa Kata Mpya ya Mkanana

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Serikali ilikuwa na mpango wa kuanzisha Kata mpya ya Mkanana ambayo ina vijiji vya Mkanana na Chibwegele na vipo mlimani ambapo hakuna huduma yoyote kama vile barabara ambayo ni mbaya sana na hupitika kwa shida wakati wote.

(a) Je, mpango huo wa kuanzisha Kata mpya umefikia wapi?

(b) Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba kuanzishwa kwa kata hiyo kutawezesha kuwasogezea karibu huduma mbalimbali wananchi wa kata hiyo kuliko ilivyo sasa ambapo Makao Makuu yapo Kijiji cha Chitemo, umbali wa kilometa 45?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza nipende kumpongeza Mheshimiwa Geogre Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kwa jitihada anazozifanya kupeleka maendeleo katika Jimbo lake. Hata hivyo, kwa mujibu wa sheria maombi ya kugawa kata mpya yanaanzia katika Mikutano Mikuu ya Vijiji, Kamati ya Maendeleo ya Kata, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Mkoa. Vikao hivyo vikikubali maombi hayo na endapo yataonekana yamekidhi vigezo, Serikali haitasita kuanzisha Kata hiyo ya Mkanana kwa kuzingatia sheria zilizopo.

(b) Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzisha maeneo mapya ya utawala zikiwemo kata, ni kusogeza huduma karibu na wananchi. Hivyo, kama ilivyoelezwa katika sehemu (a) ya jibu langu hapo juu, endapo Kata ya Mkanana itakidhi vigezo vya kuanzishwa, ili kurahisiana upatikanaji wa huduma na kuchochea maendeleo katika kata hiyo, itafanyika.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza utaratibu wote umeshafuatwa, vijijji vimekaa, Kamati ya Maendeleo ya Kata imekaa, *Full Council* imekaa na mpaka kwenye Kamati ya Ushauri ya Mkoa na ni ombi la muda mrefu sana. Wananchi wa Mkanana wanapata shida, kwanza hakuna mawasiliano ya barabara kabisa na ninakuomba tukimaliza Bunge tuende kule upite ile njia uone kama inapitika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, kwa kuwa kwenye swali langu limetaja kuna umbali kutoka Mkanana,

Chibwegele mpaka Chitemo ni kilometa 45 ndipo wananchi wanafuata usafiri. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, utakuwa tayari kukubali ombi langu tufuatane na wewe sasa baada ya Bunge hili, ukawaone watu wa Mkanana, Chibwegele, wanavyopata shida?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi ni jirani na huko nikwambie kabisa, hakufikiki rafiki yangu, labda kwa mguu, lakini majibu. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri nipokee kama taratibu zote mpaka katika ngazi ya mkoa zimekamilika tutafanya ufuatiliaji kuangalia utaratibu umefanyika lini. Kama sio yale maombi ya zamani ambayo mwanzo yalikuwa hayakukizi vigezo, kama haya mapya, ofisi yangu nadhani inafanya uchambuzi wa maeneo mbalimbali katika maeneo haya mapya.

Mheshimiwa Spika, lakini katika jambo lingine la pili, Mheshimiwa Mbunge ameomba ikiwezekana twende pamoja, naomba nikueleze wazi na mimi niko pamoja kwa sababu, najua Mheshimiwa Mzee Lubeleje watu, wanahistoria hawafahamu kwamba Mpwapwa yote ilikuwa Jimbo moja wakati huo, baadaye ikagawanyika na Jimbo lingine la Kongwa. Kwa hiyo, alifanya juhudi hizi miaka mingi sana katika michakato mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwahakikishie Wana-Mpwapwa, Wana-Kongwa na sehemu uliyosema, tutafika pale tutabaini miongoni mwa mambo hayo, lakini hasahasa tatizo la barabara katika Wilaya ya Kongwa na Wilaya ya Mpwapwa, nini tufanye kwa pamoja kuwasaidia wananchi hawa ambao kwa kiwango kikubwa wameisaidia sana Serikali hii katika mambo mbalimbali.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Mwibara, swali fupi la nyongeza.

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alishuhudia mgawanyo wa majimbo mawili ya Bunda na Mwibara kutokutana ndani ya Halmashauri moja. Na kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri wa wakati huo, Mheshimiwa Simbachawene alikuja kushuhudia na kuamua kwamba, wabadilishe mipaka Jimbo la Bunda lirudi Bunda Mjini wawe Halmashauri moja na Mwibara ibaki yenyewe iwe halmashauri wakatuahidi watatoa *Government Notice* muda si mrefu na ilikuwa mwezi wa saba. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, hiyo *GN* imefikia hatua gani, Wana-Mwibara wanataka kusikia?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ni kweli analozungumza Mheshimiwa Mbunge hapa hazushi na bahati nzuri mimi nimepata fursa ya kutembelea majimbo haya yote matatu, Jimbo la Mwibara, Jimbo la Bunda Vijijini, hali kadhalika Jimbo la Bunda Mjini. Mgawanyiko wake kwa kweli, ulikuwa una changamoto kubwa sana na bahati nzuri harakati hizi zimeshaanza.

Naomba nichukue ombi lako hili Mheshimiwa Kangi, twende tukalifanyie kazi kwa undani kujua kwamba, hili jambo limefikia wapi na hasa taratibu zilizofuatwa pale, baadaye tutaweza kutoa maamuzi sahihi, lakini sitaki kutoa *commitment* ya moja kwa moja hapa, tunalifahamu hili jambo tutaenda kulifanyia kazi kwa maslahi mapana ya hizi halmashauri zetu ambazo ziko kule.

Na. 83

Rufiji, Kibiti na Kilwa Kuunganishwa Kwenye Umeme wa Gridi ya Taifa

MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA) aliuliza:-

Ni takribani miaka miwili sasa Serikali imeshindwa kuwahakikishia wananchi wa Jimbo la Rufiji kuwa na umeme wa uhakika kufuatia hitilafu ya mara kwa mara kwenye mitambo ya umeme unaozalishwa na gesi kutoka Kilwa.

Je, ni lini Serikali itawaunganisha wananchi wa Rufiji, Kibiti na Kilwa kwenye Gridi ya Taifa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omary Mohamed Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, lililoulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mbunge maarufu sana wa Kihesa Mgagao, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilwa, Rifiji pamoja na Kibiti zimeunganishwa katika Gridi ya Taifa kupitia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Somangafungu, Lindi hadi Kinyerezi, Dar es Salaam. Ujenzi wa mradi huu utanza mwezi Julai, 2018 na utakamilika mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kazi za ujenzi wa mradi huu zinahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilometa 198 kutoka Somangafungu, Lindi hadi Kinyerezi, Dar es Salaam. Lakini pia, kujenga Kituo cha Kupoza Umeme, lakini pamoja na mambo mengine mradi huu utaunganisha wateja mbalimbali na kusafirisha umeme utakaozalishwa kutoka Kituo cha Somangafungu chenye uwezo wa kuzalisha megawati 240. Mradi utafadhiliwa na Kampuni ya Sumitomo ya Japan kwa gharama ya dola za Marekani milioni 340.

SPIKA: Mheshimiwa Mwamoto, Mbunge wa Kilolo nilikuona, swali la nyongeza.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watu wa Rufiji na sehemu nyingine ambapo gesi hiyo itapita ni watu ambao wanasubiria kwa hamu jambo hilo. Bado hawajapata elimu ya kutosha kujua umuhimu wa jambo hilo kwenye maeneo yao. Sasa Serikali itakuwa tayari kupita kutoa elimu ya kutosha, hasa mashuleni, ili wananchi kazi hiyo itakapoanza ya kupitisha gesi waone kwamba ile ni rasilimali yao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa wananchi sasa walio wengi wanategemea gesi ikianza kutoka kwa wingi na tumepewa taarifa kwamba, kuna gesi ambayo inaweza ikatumika kwenye magari. Anatuambiaje Mheshimiwa tujue kwamba unafuu wa kutumia gesi ama petroli kutakuwa kuna tofauti kubwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mwamoto kwa kuuliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge wa Rufiji na Waheshimiwa Wabunge hawa wanafanya kazi nzuri sana kwenye majimbo yao. Ni matarajio yao kwamba wananchi wanawasikia vema.

Mheshimiwa Spika, elimu ambayo tumetoa mpaka sasa, nitoe tu taarifa kwa Mheshimiwa Mbunge wa Rufiji na Mheshimiwa Mwamoto, tumeshatoa elimu katika vijiji vya Mwaseni, vijiji vya Ngarambe, kijiji cha Korongo pamoja na Kotongo, lakini tunakwenda sasa kutoa mwezi wa 10 na wa 11 elimu katika maeneo ya Jaribu Magharibi na maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, tutaendelea kutoa elimu kwa ajili ya manufaa ya miradi hii ili wananchi wa Rufiji nzima waweze kuipata kwa hiyo, tunaendelea na utaratibu wa elimu kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, suala la pili kuhusiana na gesi kwenye magari, ni kweli kabisa ule mradi wa kutengeneza gesi kwa ajili ya matumizi ya kwenye magari na majumbani ulishaanza tangu mwaka 2016 na hivi sasa mwakani mradi

huo utaendelea. Tulishaanza katika Vituo viwili vya *DIT* pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mpaka sasa magari 16 yameshaunganishwa kwa kutumia gesi badala ya petroli. Na unafuu wake ni kwamba, unapunguza asilimia 40 ya matumizi ya kawaida ya petroli unapotumia gesi.

Mheshimiwa Spika, mradi huu kwa niaba ya Watanzania wote, utaanza mwaka 2018 hadi 2020 kwa kwenda katika Mkoa wa Dar es Salaam, Mtwara pamoja na Lindi.

SPIKA: Waheshimiwa naangalia ambaye kwake kuna shida kubwa zaidi ya umeme, Liwale! Kweli bwana Makujiganga kule, Mheshimiwa Mbunge wa Liwale tafadhali.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika,ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuharibikaharibika kwa mara kwa mara kwa kinu cha gesi pale Kilwa na kutokana na uchakavu wa mitambo ile, hitajio la Wilaya za Kilwa, Lindi pamoja na Liwale, *I mean Kilwa* pamoja na Rufiji pamoja na Liwale kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Waziri atueleze hapa ni nini kinachelewesha wilaya hizi kuongizwa kwenye Gridi ya Taifa kwa sababu ya uchakavu wa mitambo ya Kilwa kunafanya umeme usiwe wa uhakika katika Wilaya hizi tatu? Ahsante sana.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa maeneo ya Kilwa, Rufiji na maeneo ya Mkuranga hivi sasa hayapati umeme wa gridi na maeneo mengine ya karibu na pale, lakini hatua zinazofanyika sasa hivi tunajenga mradi wakusafirisha umeme kutoka

Somangafungu ambao nimeutaja, lakini kutakuwa na Mradi wa *Rufiji Stiegler's Gorge* ambao unaanza Disemba mwaka huu. Kwa hiyo, kinachocheleweshwa ni maandalizi ya ujenzi kabambe wa miradi mahususi ambayo itaunganisha wananchi wa maeneo yale na Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Stiegler's Gorge* na huu niliosema ambao ni wa kusafirisha umeme wa kutoka Somangafungu kupita Kinyerezi mpaka Dar es Salaam ndio pia, utawapatia nguvu ya kutosha ya umeme na kuunganisha kwenye Gridi ya Taifa, maeneo yote ya Rufiji, Kilwa pamoja na Mkoa wa Mtwara pamoja na Lindi. Kwahiyo, wananchi wa mikoa hii miwili niwahakikishie kwamba, ifikapo mwaka 2019/2020 tayari watakuwa wameshaunganishwa na Gridi ya Taifa.

Na. 84

Vifaa Vilivyo Kwenye *delivery Kits/Packs*

MHE. KHADIJA NASSIR ALI aliuliza:-

(a) Ni vifaa gani muhimu vimewekwa kwenye vifungashio vya akinamama wakati wa kujifungua (*delivery kit*) takribani 500,000 zinavyokusudiwa kusambazwa na Serikali?

(b) Je, ni kwa nini Serikali inasuasua kwenye usambazaji wa *delivery kits* kama mkakati ulivyo?

(c) Je, ni kwa kiasi gani agizo la Mwandoya la Serikali la kuanzisha huduma za upasuaji kwenye vituo vyote vya afya nchini limetekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda

kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuna tofauti ya matumizi ya maneno *delivery kits* ambayo humaanisha vifaa vyote vinavyopaswa kuwepo kituoni katika chumba cha kujifungulia na *delivery Packs* ambavyo, ni kifurushi muhimu anachotakiwa kupewa mama mjamzito akija kliniki kitakachomsaidia wakati wa kujifungua, kwa maana ya vifungashio (*delivery packs*). Vifungashio hivi vina vifaa vifuatavyo; pamba, pedi, kifungia kitovu cha mtoto, kitambaa cha kumfutia mtoto, sindano, mipira ya kuvaa mikononi (*surgical gloves*), mpira wa kulalia wakati wa kujifungua, uzi (*chronic cutgut 2"*), vidonge vya kuzuia umwagikaji wa damu na wembe. Na gharama ya vifungashio hivi ni shilingi 25,000 kwa kila kifurushi.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, hadi sasa imesambaza vifungashio (*delivery packs*) 60,000 kwa mikoa sita ya Kanda ya Ziwa ambayo vifo vingi vya wamama wajawazito na watoto vinatokea huko. Aidha, ni jukumu la kila halmashauri kuweka mahitaji ya vifungashio kwenye mpango kabambe wa afya wa Halmashauri, yaani *Comprehensive Council Health Plan (CCHP)*.

(c) Mheshimiwa Spika, agizo la Mwandoya lilitaka kila Halmashauri nchini kwa kutumia pesa zao za ndani kuhakikisha wamejenga au kukarabati vyumba vya upasuaji katika vituo vya afya kwa kipindi cha miezi sita, ili kupunguza vifo vya mama na mtoto na kupeleka huduma karibu zaidi kwa wananchi. Baada ya muda huo kumalizika Wizara imeongeza miezi mitatu kukamilisha agizo hilo. Wataalam wa Wizara kwa sasa wanatembelea vituo katika Halmashauri nchi nzima kufanya tathmini kubaini waliotekeleza na ambao hawajatekeleza, ili hatua za kinidhamu zifuate mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imepata ufadhili wa shilingi bilioni 66 kutoka Benki ya Dunia na

imeshirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kubainisha vituo 100 vitakavyoboreshwa, ili kutoa huduma za dharura za upasuaji wa kutoa mtoto tumboni. Taya ri fedha za utekelzaji zimeanza kupelekwa katika Halmashauri mbalimbali husika hapa nchini.

SPIKA: Muuliza swali nimekuona Mheshimiwa, tafadhali swali la nyongeza.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, ni lini Serikali itatoa ruzuku ya moja kwa moja kwa kinamama wanaojifungua ili kuondoa kadhia hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilielekeza kujenga vituo vya upasuaji kila kata. Je, ni lini Serikali itatekeleza agizo hili kibajeti? Nashukuru. *(Makoff)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Hamisi Kigwangalla tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Khadija Nassir Ali kwa kuuliza swali la kisera ambalo limetupa fursa ya kufafanua mambo mbalimbali ambayo ni kipaumbele kwa Wizara yetu kwa sababu yanahusu kupunguza vifo vya wakinamama wajawazito na watoto na yeye kama Mbunge mwanamama nadhani anaguswa na mtazamo wetu kwamba hiki ni katika vipaumbele vyetu pale Wizarani.

Mheshimiwa Spika, ruzuku kutoka Serikali kuu kwenda Serikali za Mitaa kwamba ni lini itatoka? Nadhani hakufanya mazingatio ya kutosha kwenye majibu yangu ya msingi kwa sababu tayari hapa hapa tu nimezungumza tuna zaidi ya bilioni 66 ambazo tunazipeleka kwenye Halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya kufanya maboresho kwenye

vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Na hiyo ni ruzuku kutoka Serikali kuu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwenye bajeti ya afya Fungu Namba 52 tumeweka bajeti ya dawa mbalimbali ambazo zinaenda kusaidia kupunguza vifo vinavyotokana na sababu mbalimbali za uzazi. Kwa mfano, tumeweka bajeti ya *Uterotonic drugs* kama *Oxycontisin* ambapo tunapeleka kwenye Halmashauri moja kwa moja, kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, pia tumeweka bajeti mahususi ya kutoa dawa za *magnesium sulphate* ambazo zinasaidia kutibu ugonjwa wa *eclampsia* (kifafa cha mimba) ambazo hizi ni katika sababu kubwa ambazo zinapeleka kupoteza maisha wakati wa uzazi.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali Kuu inasaidia sana kwenye kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa damu salama kwenye vituo vyote vya afya nchini na hii ni moja kwa moja tunatoa sisi tunapeleka msaada kule chini. Kwa hiyo, ruzuku tunatoa na tunatoa kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize hapa kwamba Wabunge wenzangu wote na Halmashauri zote nchini watambue jukumu la kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi ni la kwao wenyewe kwenye Halmashauri husika. Ni lazima tufanye uwekezaji kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, hakuna namna nyingine. Sisi Serikali kuu tunasaidia tu kujenga uwezo wa vituo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, Ilani ya CCM haizungumzii kujenga vituo vya upasuaji kwenye kila kata, Ilani ya CCM inazungumzia ujenzi wa vituo vya afya (*health centers*) kwenye kila kata na zahanati kwenye kila kijiji. Ilani ya uchaguzi inakwenda sambamba na Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi wa mwaka 2007/2017 ambapo Halmashauri zote nchini zinapaswa kujenga vituo vya afya kila Kata na zahanati kwenye kila kijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, jitihada bado zinaendelea kwenye Halmashauri mbalimbali nchini na sisi kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya awali, tunaendelea kujengea uwezo lakini pia ku-*support* halmashauri zetu kutimiza azima hii iliyowekwa kwenye Ilani ya uchaguzi ya CCM. (*Makofi*)

SPIKA: Swali hili limechukua muda mrefu, tunaendelea na swali la Wizara hiyo hiyo la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum. Meshimiwa Stella.

Na. 85

Kuondoa Kodi Kwenye Taulo za Kike Nchini

MHE. STELLA I. ALEX aliuliza:-

Kwa kuzingatia umuhimu wa taulo za kike nchini.

Je, Serikali inaonaje ikiondoa kodi kwenye taulo hizo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maombi ya kuondoa kodi kwenye taulo za kike yamewahi kuwasilishwa na watumiaji pamoja na wauzaji wa bidhaa hiyo.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo na maazimio yametolewa katika vikao mbalimbali vya wadau na Serikali. Maamuzi ya swala hili yamechelewa baada ya kubaini kuwa bidhaa hii haikuwa miongoni mwa orodha ya vifaa vya matibabu (vifaa tiba) ambavyo huondolewa kodi isipokuwa zimeondolewa ushuru wa uingizaji (*import duty*) na aina nyingine za kodi zinalipiwa kama bidhaa nyingine zote.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imewaandikia barua Wizara ya Fedha na Mipango kuona namna ya kuondoa kodi katika bidhaa hii. Majadiliano yanaendelea kuwezesha bidhaa hii iunganishwe katika orodha ya vifaa tiba ili viweze kupata msamaha wa kodi sambamba na vifaa vingine vya tiba. Hii itapunguza gharama za upatikanaji wake kwa kuziondolea baadhi ya kodi zenye kuongeza bei kwa kiwango kikubwa mfano kodi ya ongezeko la thamani (*Value Added Tax*).

SPIKA: Sasa naona na wanaume nao wanataka kuuliza swali la nyongeza hapa. Mheshimiwa Stella Ikupa. (*Kicheko*)

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kutokana na umuhimu wa taulo hizi za kike kwa wanawake na watoto wa kike Tanzania na kutokana na ughali wake ambao unapeleka wanawake wengi na watoto wa kike kushindwa kumudu kuzitumia na kwa kuwa Serikali imekiri kwamba maombi haya yameshawasilishwa na wadau wengi.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali inaweza ikatuambia nini wanawake wa Tanzania kwamba watoto wengi wanapata shida hasa watoto wa vijijini kwa sababu wanashindwa kuzipata hizi taulo kwa ughali wake. Sasa Serikali inaweza ikatuambia ni lini tutegemee kwamba lini huu mchakato utakamilika?

Mheshimiwa Spika, ingekuwa ni vizuri wakatuambia ni lini mchakato huu utakamilika kwa sababu kweli hili jambo ni suala nyeti sana kwa wanawake na watoto wa kike Tanzania? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri huwezi kuwa na majibu ya haya, haya majibu anatakiwa atoe Waziri mwenyewe kwa kweli. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri wa Afya kwa kuwa upo, majibu tafadhali, namuonea huruma Mnyamwezi huyu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, na mimi kwa kweli namshukuru sana Mheshimiwa Stella Ikupa kwa swali lake zuri la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mwanamke lakini pia nina watoto wa kike wawili, kwa hiyo, nakubaliana na yeye kabisa kwamba tuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa taulo za kike hasa kwa watoto walio vijijini na tunazo taarifa kuna watoto wanaweka mpaka majini ili kuweza kujisitiri pale wanapokwenda shule, lakini pia kuna watoto wanakosa hadi siku tano za masomo kwa sababu hawana zana za kujisitiri ili waweze kufanya masomo yao bila shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwahiyo, Wizara yangu nimeshamuandika Waziri wa Fedha kumuomba aharakishe mchakato huu, nilikuwa namtimizama hayupo lakini naamini wenzetu wa Wizara ya Fedha wanalifanyia kazi na tutakuja na majibu mazuri kadri itakavyokamilika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri amejibu majibu ya kutosheleza kabisa kwenye swali hili. Mimi ajenda hii naiona ni muhimu sana lakini sasa tuwatupie wenzetu wa Umoja wa Wabunge Wanawake wote humu Bungeni *(TWPG)* kwa kweli ni moja ya ajenda ambayo ni vizuri muiweke vizuri huko halafu muipe nafasi yake, ni moja ya maeneo ya kuyafanyia kazi kwa umakini mkubwa. Kwa hiyo, nawarudishia Mheshimiwa mama Margaret Sitta na timu yako muweze kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Wizara ya Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, Mbunge wa Ushetu.

Na. 86

Kuboresha Muundo wa Kamati za Ukaguzi

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA aliuliza:-

Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuboresha maeneo ya uendeshaji na usimamizi wa rasilimali ya Menejimenti, Bodi, Mabaraza ya Madiwani, Ukaguzi wa Nje, Ukaguzi wa Ndani na kuliacha eneo muhimu la Kamati za Ukaguzi (*Audit Committee*) kwenye Wizara, Idara, Wakala na Serikali za Mitaa.

Je, ni lini Serikali itaboresha Kanuni ili muundo wa Kamati za Ukaguzi ziundwe na Wajumbe wengi (*majority*) toka nje ya taasisi kuzingatia weledi na uzoefu ili kusimamia rasilimali kwa tija na ufanisi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, Mbunge wa Ushetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa Kamati za Ukaguzi umetajwa katika Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 kama ilivyorekebisha mwaka 2004 ambapo inaelezwa ya kwamba Kamati za Ukaguzi ziundwe na wajumbe watano; kati ya hao, mjumbe mmoja atoke nje ya taasisi. Aidha, kati ya wajumbe hao wa Kamati za Ukaguzi anatakiwa angalau mjumbe mmoja awe na uzoefu katika masuala ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mwaka 2013 Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa Mwongozo wa Utendaji Kazi wa Kamati za Ukaguzi katika taasisi za umma kuhusu idadi ya wajumbe kutoka nje ya taasisi kuwa wajumbe wawili au zaidi wateuliwe kutoka nje ya taasisi; mwongozo huo unawaelekeza Maafisa Masuuli kuwa wanaweza kuteua wajumbe kutoka nje ya taasisi kuanzia wajumbe wawili au zaidi. Hata hivyo, Wizara ya Fedha na Mipango inapitia upya Sheria ya Fedha za Umma na Kanuni zake ili tuweze kuwa na muundo mpya na huru wa Kamati za ukaguzi ili kuleta ufanisi.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Ushetu nimekuona, uliza swali la nyongeza.

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Naipongeza sana Serikali kwa hatua inayochukua ili kuweza kuboresha usimamiaji wa rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uwepo wa Kamati za Ukaguzi ni muhimu sana katika kuimarisha mfumo wa udhibiti katika taasisi hususan katika Halmashauri zetu. Kwa kuwa Kamati imara husaidia Maafisa Masuuli kutimiza wajibu wao na hii Kamati ni muhimu kwa ajili ya kusimamia pia mpango kazi wa Wakaguzi wa Ndani na Wakaguzi wa Nje. Kwa kuwa Serikali imetoa mwongozo wa mwaka 2013 na haujatekelezwa vizuri katika Halmashauri zetu.

Je, Serikali iko tayari kuzielekeza upya Halmashauri zetu kutekeleza mwongozo huu mzuri kikamilifu ili kuleta tija zaidi katika usimamiaji wa rasilimali zetu? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake katika kuhakikisha rasilimali za Taifa letu zinatumiwa ipasavyo na kama ailivyouliza, sisi kama Wizara tupo tayari na tumekuwa tukihakikisha Kamati hizi zinatekeleza maelekezo na miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, sasa kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba tunaendelea kushughulikia sheria hii pamoja na kanuni zake ili tuje na sheria itakayohakikisha rasilimali za Taifa letu zinasimamiwa ipasavyo.

SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 87

TRA Kukusanya Kodi ya Majengo

MHE. CECILIA D. PARESSO aliuliza:-

Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilitangaza kuzinyang'anya Halmashauri uwezo wa kukusanya mapato ya kodi ya majengo (*property tax*) na kuagiza kodi hiyo kukusanywa na Mamlaka ya Mapato (*TRA*).

(a) Je, baada ya Mamlaka ya Mapato kupewa jukumu hilo, ufanisi umefanikiwa kwa kiasi gani ikilinganishwa na mapato yaliyokuwa yakikusanywa na Halmashauri zenyewe?

(b) Kwa kuwa kodi ya majengo ilikuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa mapato ya Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji na majukumu ya kutoa huduma kwa wananchi hayajapunguzwa. Je, Serikali imejipanga vipi kufidia vyanzo hivyo vilivyopotea?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali kupitia Bunge lako Tukufu ilifanya mabadiliko ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (*The Local Government Finance Act, Cap. 290*) kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 na kuipa Mamlaka ya Mapato Tanzania jukumu la kukusanya kodi ya umiliki wa majengo yaani (*property tax*) kwa Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji 30. Ufanisi wa Mamlaka ya Mapato ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, makusanyo yatokanayo na kodi za majengo kutoka Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji 30 yaliyokuwa yakisimamiwa na *TRA* yameongezeka kutoka shilingi bilioni 28.28 kwa mwaka 2015/2016 zilizokusanywa na

Serikali za Mitaa hadi shilingi bilioni 34. 09 kwa mwaka 2016/2017 kipindi ambacho *TRA* ilianza kukusanya kodi hii. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 20.6 ya makusanyo ya Halmashauri husika kabla ya kodi hii kuhamishiwa *TRA*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kodi ya majengo imekuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa mapato ya Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji katika kutekeleza mipango ya utoaji wa huduma za jamii. Hata hivyo, hatua ya Serikali ya kuhamishia jukumu hilo la ukusanyaji wa kodi za majengo *TRA* haikulenga kuzinyang'anya Halmashauri vyanzo vya mapato bali kuimarisha ukusanyaji wake. Takwimu nilizotoa hapo juu zinadhihirisha kuwa *TRA* imefanya vema katika kukusanya mapato hayo ikilinganishwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu wa kibajeti ambao unaziwezesha Halmashauri kupata fedha za makusanyo ya kodi ya majengo iliyokusanywa na *TRA* ili kuziwezesha kutimiza majukumu yao. Utaratibu uliopo ni kwamba Halmashauri zinatakiwa kuomba fedha hizo kutoka Serikali kuu kwa kuzingatia makisio ya bajeti zao. Kwa mantiki hiyo, Halmashauri zinashauriwa kuzingatia utaraibu huo ili ziweze kupata fedha hizo.

SPIKA: Mheshimiwa Paresso nilikuona, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inakiri kwamba baada ya *TRA* kupokea jukumu hili mapato yameongezeka ukilinganisha na Halmashauri za Wilaya; na kwa kuwa Serikali mnapaswa kurudisha fedha hizo katika Halmashauri kwa wakati.

Je, ni lini Serikali *mtakoma hii tabia ya kuchelewesha fedha kupeleka kwenye Halmashauri zetu za Wilaya?* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 Serikali imefuta vyanzo vingi vya Halmashauri ambavyo vilikuwemo kwenye bajeti ikiwemo ushuru wa mabango, makanyagio, ushuru wa mazao chini ya tani moja, *farm gate price* kutoka asilimia tano mpaka asilimia tatu na kwa kiwango kikubwa uendeshaji wa Halmashauri zetu unategemea fedha za ndani (mapato ya ndani).

Je, Serikali sasa baada ya kufuta vyanzo hivi vingi ambavyo kwa kiwango kikubwa inaharibu utekelezaji wa bajeti zetu katika Halmashauri. Ni lini mtahakikisha fidia ya vyanzo hivi inatolewa na Serikali Kuu ili Halmashauri zetu ziendeleo kufanya kazi kwa ufanisi? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Paresso, nakupa nafasi urudie tena swali lako la kwanza kwa sababu umetumia Kiswahili kisichokubalika, hebu liweke vizuri. Ulikuwa unauliza nini?

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nafuta na nauliza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekuwa ikichelewesha fedha mmekuwa mnasema mnakusanya *TRA* na baadaye fedha zitarudishwa kwenye Halmashauri. Kwa kuwa mmekuwa mkichelewesha. Sasa ni lini mtaacha kuchelewesha ili fedha hizi ziende kwa wakati?

SPIKA: Hicho ndio Kiswahili kizuri. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwanza kwa kurekebisha Kiswahili kile lakini sio kosa lake ni kosa la watani zangu hawa wa Manyara, lakini nashukuru umerekebisha sasa imekaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nianze kusema kwamba kwanza Serikali haipendi kuchelewesha fedha hizi kupeleka katika Halmashauri zetu. Tunachofanya Wizara ya Fedha tunasimamia mpango wa *cash budget*, tunakusanya na

tunapokusanya tunahakikisha Halmashauri zetu zinapatiwa fedha kulingana na bajeti zao ambazo zimetenga.

Mheshimiwa Spika, hii inakwenda katika swali lake la pili alilosema tumefuta vyanzo vingi, lengo letu kama Wizara, kama Serikali, ni kuhakikisha tunapeleka unafuu wa maisha kwa wananchi wetu. Usumbufu wa kodi mbalimbali na ushuru ambao walikuwa wakisumbuliwa ndiyo ambao Mheshimiwa Rais wetu aliahidi kufuta na sisi kama Wizara tumesimamia na tumefuta.

Mheshimiwa Spika, kama Wizara niseme hatujawahi kuacha kupeleka bajeti kwa halmashauri zetu pale ambapo fedha yetu imekuwa inatosha. Tunapeleka na tunaahidi kuendelea kuzipeleka halmashauri zetu bajeti zao kama ambavyo zimepitishwa na Bunge lako tukufu, na nimhakikishie Mheshimiwa Cecilia kwamba halmashauri zote zitapata bajeti zao kama ambao zimepitishwa. Na hii ni dhamira yetu na tumeanza utekelezaji, na yeye ni shahidi kule kwenye halmashauri yake anaona jinsi ambavyo tunapeleka fedha hizi kwa sasa.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Kikwembe na Mheshimiwa Pauline Gekul mtauliza maswali ya nyongeza.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza. Wakati tunapitisha bajeti tuliongelea suala la kodi ya majengo kwamba nyumba za kawaida zitaanzia shilingi 10,000 na nyumba ambazo zinakuwa kwenye *level* ya maghorofa zitaanzia shilingi 50,000. Lakini cha kushangaza mpaka sasa hivi tunaona kodi hizi hazina uwiano, unakuta kati ya nyumba na nyumba mwingine anapelekewa kodi ya shilingi 10,000 mwingine shilingi 30,000, mwingine shilingi 40,000.

Je, nini kauli ya Serikali kuhusu hizi kodi na uwiano ambao si sawa kati ya Halmashauri ama Manispaa ndani ya Manispaa moja unakuta kata nyingine bei ni tofauti na kata nyingine bei ni tofauti, ama Halmashauri moja ni bei tofauti na Halmashauri nyingine ni bei tofauti.

Je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na kodi ambayo tuliipitisha sisi wenyewe Wabunge wakati wa bajeti? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya Serikali Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kuhusu swali hilo la Dkt. Kikwembe.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kodi aliyoiiongelea ya majengo inayokusanywa tofauti kutoka halmashauri moja kwenda halmashauri nyingine ni kodi iliyopitishwa na Bunge lako tukufu kwa ajili ya mwaka 2016/2017, ndiyo hiyo ambayo inakuswanywa na inaonekana kuna utofauti kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine, kodi ambayo Bunge lako tukufu imeipitisha mwaka huu wa 2017/2018 ni kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Kikwembe; kwa nyumba za kawaida ni shilingi 10,000 na nyumba za ghorofa kama ambavyo ilielezwa kwenye *Finance Act* ni shilingi 50,000. Kwa hiyo, utofauti unaoonekana ni ile tu wananchi wetu walichelewa kulipa kodi ya majengo ya mwaka 2016/2017 lakini kwa mwaka 2017/2018 kodi itakayotozwa ni kama ambavyo Bunge lako Tukufu limepitisha.

SPIKA: Mheshimiwa Gekul nilishakutaja.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, katika Bunge la Bajeti lililopita, tulipitisha au tulirekebisha Sheria ya Serikali za Mitaa kuhusu ushuru wa mazao; chini ya tani moja wakulima hawa wasitozwe, hasa mazao ya chakula, mfano mahindi na mazao mengine. Lakini Wakurugenzi na Mawakala katika halmashauri zetu wameendelea kuwatoza wananchi ambao wana magunia matano, matatu ya mahindi, mfano Geti la Galapo katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati – na hilo Geti la Galapo unalifahamu mtani wangu.

Nini kauli ya Serikali kuhusu ukaidi huu wa Wakurugenzi na Mawakala kuendelea kuwatoza wakulima wetu hata

magunia matatu ya mahindi wanalipa ushuru huo wa mazao, nini kauli ya Serikali?

SPIKA: Maelezo ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, sheria inabaki kuwa sheria na tunawataka wasimamizi wa sheria hii kule kwenye halmashauri zetu ambao ni Wakurugenzi wetu Watendaji wa Halmashauri zote kuhakikisha sheria hii inasimamiwa, mazao yetu yote ya biashara pamoja na ya chakula chini ya tani moja hayatakiwi kutozwa ushuru wowote, na hii ni sheria naomba itekelezwe. Na kama kuna jambo *specific* ambalo limetokea niwaombe sana wananchi wetu tuwasiliane. Namba zetu ziko hewani, ofisi zetu ziko wazi, tuwasiliane ili kuhakikisha sheria hii inatekelezwa kama ilivyopitishwa na Bunge letu Tukufu.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, swali linaulizwa na Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka.

Na. 88

Uchimbaji wa Bwawa katika Kijiji cha Mwasa

MHE. DANIEL E. MTUKA aliuliza:-

Kwa kuwa bwawa linalotarajiwa kuchimbwa katika Kijiji cha Mbwasa, Tarafa ya Kintinku ni bwawa la kimkakati kwa wakazi wa Tarafa nzima ya Kintinku.

Je, ni lini Serikali itaanza rasmi ujenzi wa bwawa hilo baada ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ilipanga kujenga Bwawa la Mbwaswa kwa kupitia Mto wa Msimu wa Luwila ikiwa ni hitaji la wananchi wa Kijiji cha Mbwaswa kwa ajili ya shughuli za kilimo, mifugo na matumizi ya nyumbani. Ujenzi wa Bwawa la Mbwaswa ulikusudiwa kunufaisha pia wananchi wa vijiji vya jirani vya Mwiboo, Mtiwe na Chikuyu, lengo kuu ikiwa ni kuimarisha kilimo cha umwagiliaji wa zao la mpunga. Hali hii inatokana na maeneo hayo kutokuwa na uhakika wa mvua za kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, upembuzi yakinifu na usanifu wa Bwawa la Mbwaswa ulifanyika kupitia Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Dodoma. Aidha, matokeo ya upembuzi huo yalibaini kuwa jumla ya shilingi 2,500,000,000 zingehitajika kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo. Hata hivyo, bajeti za maendeleo za fedha za ndani iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji ikiwemo Bwawa la Mbwaswa haikutolewa na hivyo kusababisha ujenzi wa bwawa hili kutotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilianza kufanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa Mwaka 2002. Kwa kutambua umuhimu wa ujenzi wa mabwawa kama hatua ya kimkakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Bwawa la Mbwaswa limepewa kipaumbele na litaingizwa katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuanza utekelezaji ili hatimaye lengo la Serikali na wananchi wa Kijiji cha Mbwaswa pamoja na vijiji vya jirani kuwa na kilimo cha uhakika.

SPIKA: Mheshimiwa Mtuka swali la nyongeza.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Nina maswali mawili ya ngongeza. Hali ya upatikanaji wa maji hasa katika eneo la Bonde la Ufa katika Jimbo la Manyoni Mashariki ni ngumu

sana, hivi ninavyozungumza mifugo inahangaika, watu wanahangaika, akinamama wanalala kwenye visima ambavyo havina uhakika wa kupatikana kwa maji, hali ni ngumu sana kwa kweli. Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba litawekwa katika kipaumbele cha bajeti inayokuja, ninaomba tu ni ombi, kwa *emergency*, kwa hali ambayo nimeielezea hii, hali ni ngumu, naomba liingizwe kwenye bajeti ya mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Kata ya Sorya Wilayani Manyoni, kwenye Jimbo langu katika harakati za kuhanangaika kuwatafutia ajira vijana na akina mama tumetenga eneo, zaidi ya eka 400 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na tumechimba visima vitatu kwa fedha yetu wenyewe. Tuna shida ya umeme kwa ajili ya kufunga pampu za kutoa maji ili tuweze kumwagilia.

Je, Serikali inaweza kutusaidia sasa kupeleka umeme kwenye visima vile ili kunusuru wananchi hawa wanaohangaika, hasa vijana, tuweze kumwagilia maeneo haya na tuweze kujinusuru kwa suala la njaa? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, tafadhali.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie kama tulivyoji-*commit* kwenye jibu la msingi, kwamba tutaweka kwenye bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa hiyo naomba nimhakikishie kwamba tutafanya hivyo kwa sababu tumeshatoa jibu la namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu ekari 400 ambazo mmepanga kuendeleza kilimo cha umwagiliaji; nilipokee ombi lake lakini tutaangalia uwezo wa bajeti iliyotengwa kwa mwaka huu wa fedha, kama itawezekana tutasaidia, lakini vinginevyo tutaangalia katika bajeti ya mwaka utakaofuata.

SPIKA: Tunaendelea bado tupo Wizara hiyo hiyo, swali na Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi.

Na. 89

Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria

MHE. MASHIMBA M. NDAKI aliuliza:-

Serikali imekamilisha mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Mji wa Ngudu na vijiji vilivyo karibu na mji huo Wilayani Kwimba. Mradi huo unatoa maji ya uhakika kuliko miradi ya visima vifupi ambavyo ni vya msimu. Lakini Mji Mdogo wa Malampaka na vijiji vingine vya karibu kama Jihu, Bukigi, Muhida, Lali, Nyabubinza na Mwang' honoli ambavyo vipo karibu na Mji wa Ngudu havijaunganishwa kwenye mradi huo.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunganisha Mji Mdogo wa Malampaka na vijiji vya Jihu, Bukigi, Muhida, Lali, Nyabubinza na Mwang' honoli katika mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria ili kuwapatia wananchi maji ya uhakika?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa maji safi toka Ziwa Victoria kwenda katika Mji wa Ngudu na vijiji vilivyopo kandokando ya bomba linalopeleka maji katika mji huo. Vijiji hivyo ni Runele, Ngatuli, Nyang' onge, Damhi na Chibuji. Mradi huu ulihusu ulazaji wa bomba kilometa 25 na sehemu nyingine ya bomba lilitumika bomba la zamani la mradi wa visima uliojengwa miaka ya 1970. Bomba hilo ni la kipenyo cha inchi nane na kulingana na usanifu halitoshi kuendeleza zaidi kwenda Malampaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nafikiri mnaona wenyewe sauti zenu, ni vizuri tu m-*regulate*. Ukisikiliza wewe mwenyewe utaona tu umuhimu wa kupunguza sauti kidogo.

Mheshimiwa Waziri, endelea na majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji imetekeleza Miradi ya Maji ya Malampaka, Sayusayu, Masayi, Njiapanda na Sangamwalugesha ambayo imekamilika na wananchi wanapata maji. Miradi ya Maji ya Lalago, Mandang'ombe na Jija inaendelea kujengwa na ujenzi umekamilika kwa asilimia 65. Serikali pia imekamilisha usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa Miradi ya Maji ya Mwambulimbu, Mwamanenge na Badi ambao utahudumia vijiji vitatu vya Muhiba, Jihu na Badi yenyewe. Ujenzi wa miradi hii utafanyika katika Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza miradi hii kwa awamu, hivyo, kwa vijiji ambavyo havipo katika awamu hii tunaomba Mheshimiwa Mbunge awasiliane na halmashauri husika ili viwe katika kipaumbele katika awamu zinazokuja.

SPIKA: Swali hili najua lina wadau wakubwa, Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Ndassa. Tuanze na Mheshimiwa Ndassa halafu Mheshimiwa Nyongo, maswali ya nyongeza.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilitenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya Mradi wa Maji Sumve, Madya na Malampaka, mwaka 2017/2018 ilitenga shilingi bilioni mbili kwa ajili ya mradi huo. Sasa Mheshimiwa Waziri katika majibu yake, kwa sababu ili maji yafike Mji wa Malampaka ni lazima yafike Sumve na Malya. Sasa nataka kujua, tulitegemea kwamba ungetaja, angalau kwamba Serikali imetenga

shilingi bilioni mbili kwa ajili ya mradi huo, lakini hukutaja hata kidogo. Sasa swali Mheshimiwa Waziri, pesa zilizotengwa sasa hivi hazipo tena au mradi huo umeshakufa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Mashimba nitarudi kwako baadaye. Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILAJI: Mheshimiwa Spika, majibu niliyoyatoa haya yanalingana na swali lilivyoulizwa na Mheshimiwa Mashimba. Lakini kwa maana ya kutaka afahamu mradi wa kupeleka maji Sumve mpaka Malampaka, tumetenga fedha hizo, mwaka huu, shilingi bilioni mbili, kwanza kwa ajili ya kukamilisha usanifu na makabrasha ya zabuni ili kusudi tuweze kutangaza *tender* ya kupeleka maji Sumve mpaka Malampaka. Nia ya Serikali ipo palepale, hakuna mabadiliko, hata kama tungesema tu hapa bila utekelezaji ingekuwa haitusaidii, lakini nia ya Serikali ipo na lazima tupeleke maji Sumve, Malya na Malampaka.

SPIKA: Mheshimiwa Mashimba, halafu Mheshimiwa Nyongo.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Spika, msingi wa swali hili ulikuwa ni maji kutoka Ziwa Victoria, sasa ninashukuru Mheshimiwa Ndassa, kaka yangu, ameuliza swali nililotaka kuuliza la nyongeza. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Nyongo.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Ninapenda kujua kwamba Maswa tumekuwa na tatizo kubwa sana la maji, kwa kweli hali ni mbaya na inahitajika hali ya dharura kutatua tatizo la maji katika Mji wa Maswa na maeneo yake. Sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, anatumakikishia vipi kwamba kuna njia

mbadala ya kupata maji katika Mji wa Maswa kwa sababu bwawa tunalolitumia limekauka kabisa? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo la wananchi wa Maswa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Wanasema hawaogi kabisa Wasukuma hawa.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nikiri, ni kweli bwawa ambalo Mji wa Maswa ulikuwa unategemea limekauka, na hii inatokana na matumizi yasiyokuwa endelevu ya wafugaji ambao walikuwa wanafuga jirani na lile bwawa kuweza kuzalisha matope na hivyo kufanya lile bwawa kujaa matope na maji kukauka. Kwa hiyo, Serikali tumetenga bilioni 1.1 katika Halmashauri ya Maswa, sasa katika fedha zile wanaweza wakatumia sehemu ya fedha hiyo katika kutafuta mpango wa dharura ili kuhakikisha kwamba wananchi wa pale wanapata maji.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ujumla, Mkoa wa Simiyu, tunao mpango mkubwa wa kupeleka maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Bariadi na wilaya hizo zote ambao unafadhiliwa na *KfW* pamoja na *Global Climate Fund*, huu ni Mfuko wa Mazingira Duniani, kwahiyu fedha hizo, Euro milioni 100 na Euro milioni 25 tayari tumezipata. Sasa hivi tunakamilisha tu usanifu wa kina na muda si mrefu tutatangaza tenda ili tuweze kuujenga mradi ule, huo ndio utakuwa jibu la Mkoa huu wa Simiyu kuliko hivi visima ambavyo kwa muda mfupi vinakuwa vinakauka.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua kwa Wizara hiyo hiyo ya Maji.

Na. 90

Mradi wa Maji – Mto Malagarasi

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA aliuliza:-

Wilaya ya Kaliua inakabiliwa na tatizo kubwa sana la maji hali inayosababisha wananchi wake wengi kuteseka kwa kukosa huduma hiyo muhimu na kutumia muda mwingi kutafuta maji umbali mrefu na hivyo kushindwa kufanya shughuli za maendeleo.

Je, mradi mkubwa wa kutoka Mto Malagarasi kwenda vijiji vya Kaliua mpaka Urambo utaanza lini na kukamilika lini?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo la maji katika vijiji vya Kaliua hadi Urambo, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kutoa maji Mto Malagarasi kwa kumuajiri mtaalam mshauri ambaye anaendelea na kazi ya usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya ujenzi. Kazi hiyo imepangwa kukamilika mwezi Oktoba, 2017.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya usanifu wa mradi huo. Aidha, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo, na mara fedha zitakapopatikana, itajulikana ujenzi wa mradi huo utaanza lini na kukamilika lini.

SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa Sakaya, Naibu Katibu Mkuu wa CUF. *(Makofi)*

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa huu ni mwaka wa nne tangu Serikali ilivyokuja na mpango wa kutoa maji Malagarasi lakini bado mradi uko kwenye upembuzi yakinifu na hata fedha

iliyotengwa, shilingi bilioni mbili mwaka huu ni kwa ajili ya upembuzi yakinifu, wakati huohuo wananchi wa Kaliua wanaendelea kuteseka kupata maji na akina mama wanateseka na watoto hawaendi shule kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huu ni mpango wa muda mrefu, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi wa kuwapatia wananchi wa Kaliua maji ya uhakika na masafi?
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Kampuni ya *GTI* imefanikiwa kuchimba kisima cha maji kwenye Kata moja ya Usindi na ikapata maji mengi pamoja na kuwa ardhi ya Kaliua haina maji kwenye *water table*, Serikali sasa ina mpango gani wa kupeleka wataalam wenye uwezo mkubwa Kaliua waweze kugundua maeneo yenye maji ya uhakika kwenye ardhi ili angalau tupate visima vyenye maji ya kutosha wananchi wapate maji ya kutosha waache kuteseka na adha kubwa ya maji Jimbo la Kaliua? Ahsante.
(Makofi)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waizi wa Maji na Umwagiliaji, *Engineer* Lwenge.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Sakaya alikuja ofisini na tukazungumza matatizo ya maji katika Wilaya yake na nikamueleza kwamba nitapeleka wataalam kupitia *TUWASA* ili wakasaidiane na Mhandisi wa Wilaya, inaonekana kidogo Mhandisi wa Wilaya hana uwezo wa kuweza kufanya usanifu wa miradi maana mpaka sasa ametengewa shilingi milioni 692 anataka azitumie zote kufanya usanifu, nimekataa kwamba haiwezekani ukatumia shilingi milioni 600 kwa usanifu, tunataka tupate matokeo.

Kwa hiyo, napeleka wataalam ili wakashirikiane angalau hata hicho kisima anachokizungumza tuweze kukiendeleza wananchi wa pale waweze kupata maji. (Makofi)

SPIKA: Tuendelee Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Maliasili na Utalii, swali linaulizwa na Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga, Mbunge wa Ulanga.

Na. 91

Ahadi ya Kuwapatia Ardhi Wananchi wa Kata za Ulanga

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA (K.n.y. MHE. GOODLUCK A. MLINGA) aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano aliahidi kuwapatia wananchi wa Kata za Lupiro, Iragua, Milola na Minepa eneo la ardhi oevu ya Bonde la Mto Kilombero kwa ajili ya makazi na kilimo pindi tu atakapoingia madarakani.

Je, utekelezaji wa ahadi hiyo imefikia wapi?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga, Mbunge wa Jimbo la Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliahidi kumaliza matatizo ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo maeneo ya kata nne zilizotajwa ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 22(e). Hata hivyo, utaratibu wa kushughulikia ahadi hiyo katika kata hizo haukutajwa kuwa ni kwa kumega sehemu ya ardhi oevu katika Bonde la Mto Kilombero. Napenda kutumia fursa hii kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kazi ya kushughulikia tatizo hili la ukosefu wa ardhi kwa wananchi wa kata hizo limeanza kupitia Mradi wa *KILORWEMP*, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (*TAWA*) na kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Serikali ya Mkoa wa Morogoro pamoja na Wilaya za Malinyi, Kilombero na Ulanga.

Mheshimiwa Spika, kazi hii inafanyika kwa umakini mkubwa ili kuepuka kukiuka misingi na dhana nzima ya uhifadhi, kwanza kwa kuzingatia vigezo na umuhimu wa ardhi oevu na pili kwa kuhakiki mipaka halali ya vijiji yaani *village approved survey plans*. Aidha, kupitia *Land Tenure Support Program* unaotekelezwa chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji inaandaliwa hadi hatua ya kutoa hati miliki za kimila kwa vijiji vyote vinavyozunguka Bonde la Mto Kilombero.

Mheshimiwa Spika, suala hili pia linafanyiwa kazi sambamba na maombi ya wananchi kupitia wawakilishi wao wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na Madiwani ambayo yamekuwa yakipelekwa katika ngazi mbalimbali likiwemo Bunge lako Tukufu. Kazi hii ni shirikishi, wananchi wa kata na vijiji katika Wilaya husika wanashirikishwa kikamilifu hadi kufikia maridhiano ya pamoja. Kwa mfano, katika Kijiji cha Igawa, Kata ya Igawa, Wilaya ya Malinyi, baada ya kufikia maridhiano na kwa kuzingatia vigezo vya pande zote, eneo la kijiji liliongezeka kutoka kilometa za mraba 39.8 hadi 86.97 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 118.5. Eneo la Kijiji cha Sofi Majiji liliongezeka kutoka kilometa za mraba 93.9 hadi 108.99 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 16.1. Kuongezeka au kupungua kwa eneo kunatokana na vigezo vilivyowekwa ingawa hadi sasa hakuna kijiji kilichopoteza eneo.

SPIKA: Mheshimiwa Mponda, swali la nyongeza.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa mchakato ambao unaendelea katika maeneo yale.

Swali la kwanza, kupitia huo Mradi wa *KILORWEMP*, wadau tulikaa mwezi Oktoba, 2016 katika Mji Mdogo wa Mikumi. Tulichokubaliana ni kwamba urejeshaji upya wa

mipaka ile utazingatia ushirikishi wa wananchi. Serikali wamefanya hilo lakini changamoto hapa, tunapojadiliana, tunapokubaliana katika urekebishaji wa ile mipaka lakini wakienda *site* watumishi/wataalam wale wa Serikali wanagoma, wanaelekeza kuweka mipaka kama wanavyotaka wao. Kwa mazingira hayo bado wataendelea mgogoro. Kwa nini sasa makubaliano yale na wananchi na wadau kwenye kijiji hayatekelezwi wanapokwenda kuweka upya ile mipaka? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali sasa mnafanya zoezi la kuondoa mifugo kwenye hifadhi kwa maeneo yale ya lile Bonde la Ardhi Oevu la Kilombero. Mifugo ile itakapotoka kule inakuja kwenye ardhi ya vijiji, ardhi ya vijiji ndiyo yenye vyanzo vya maji katika bonde lile la Kilombero. Je, Serikali mnavisaidiaje vijiji hivi kukabiliana na msukusuko huo wa ile mifugo itakapotoka kule kwenye lile bonde kuja kwenye ardhi ya vijiji? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili yaliyoulizwa na Mheshimiwa Dkt. Mponda, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza linasisitiza juu ya umuhimu wa ushirikishwaji wa wananchi jambo ambalo kwenye majibu yangu ya msingi nimelifafanua kirefu kwamba kwa mujibu wa mipango ya Serikali ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kufanya uhifadhi uweze kuwa endelevu na kuweza kutimiza masharti ya sheria, kanuni na taratibu bado utekelezaji wake unaendelea kusisitizwa na kwamba Serikali itaendelea kuona umuhimu wa ushirikishwaji wa wananchi. Katika mradi huu wa *KILORWEMP* tayari tunao mpango huishi unaoitwa *intergrated management plan* ambao kwa mujibu wa Kanuni za Mkataba za *RAMSAR Convention* tunapaswa kuuzingatia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nipokee maelezo yake ambayo nayasikia kwa mara ya kwanza hapa kwamba makubaliano yanayofikiwa katika vikao mbalimbali vilevile

vya ushirikishwaji wa wananchi wakati wa kwenda kuyatekeleza kule *site* yanakuwa yana kasoro au yana upungufu. Hili naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa niaba ya Serikali tunalipokea ili tuweze kufika kule kwenye maeneo yanayohusika tuweze kuona pengine katika utekelezaji, utendaji unakuwa una kasoro. Kwa hiyo, tukifika kule tutakwenda kushirikiana kuona namna gani tunaweza kuondoa hizo kasoro ndogo ndogo zinazoweza kukwamisha dhamira kuu ya Serikali ya kuweza kufanya uhifadhi uwe na mafanikio.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili linalohusiana na uondoaji wa mifugo kwenye maeneo yaliyohifadhiwa na changamoto zake, anataka kujua kwamba uondoaji wa mifugo katika maeneo yaliyohifadhiwa na mahsus katika suala hili ni suala la Bonde la Mto Kilombero kwamba mifugo ile hasa ng'ombe wanapokwenda katika maeneo ya vijiji wanakwenda kusababisha changamoto nyingine ambazo na zenyewe zinakuwa ni kubwa vilevile pengine ni kubwa zaidi kuliko wanapokuwa wako kwenye hifadhi kwa mujibu wa maelezo yake.

Napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba na hili nalo ni suala vilevile la ushirikishaji wa pande zote mbili kwamba Serikali na wananchi kwa pamoja tunapaswa kufanya kazi hizi kwa pamoja kwa kushirikishana ili kila mmoja atambue umuhimu wa uhifadhi lakini katika kusimamia uhifadhi, changamoto tunazokutana nazo wakati wa kusimamia tuweze kuzitatua kwa pamoja. Kwa hiyo, katika safari hiyohiyo ninayosema tutakuja tuweze kuona nini kiko *site*, tutaweza kuliangalia tatizo hili la mifugo inayoondoka katika maeneo ya hifadhi ya Mto Kilombero ili tuweze kuona namna ya kutatua changamoto hizo katika maeneo ya vijiji wanamoishi wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Waitara, swali fupi la nyongeza.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kuna mgogoro wa Hifadhi ya Kazimzumbwi kati ya Ukonga na Kisarawe na nimshukuru Mheshimiwa wa Maliasili na Waziri wa Ardhi na Mheshimiwa Waziri Mkuu tulishakutana tukafanya mazungumzo na kulikuwa na kesi Mahakamani ambayo imekwisha. Sasa wataalam wale wa Maliasili wameenda Kazimzumbwi, wamevunja nyumba za watu, wanapiga watu, wanaharibu mali za watu katika eneo hilo. Swali langu, hawa Waheshimiwa Mawaziri wawili, wapo tayari twende pale Kazimzumbwi au hapahapa Dodoma nipo tayari kuwaita wale wahusika tukae pamoja tukubaliane kumaliza mgogoro ule ili usilete maafa katika aneo lile? Ni hilo tu.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu Kazimzumbwi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, swali lake linafanana na maswali yaliyoulizwa na muuliza swali la msingi hapo awali, ni changamoto za utekelezaji wa usimamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa kwamba wananchi wamekuwa wakilalamika juu ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazohakikishia Serikali kwamba tunasimamia maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto moja inayojitokeza hapa ni kwamba, kwa sababu suala hili linahusisha pande mbili; upande mmoja ni Serikali ambayo inasimamia sheria, kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu yako masuala ambayo ni lazima yatekelezwe ili kuhakikisha kwamba uhifadhi unafanikiwa lakini upande wa pili ni wananchi ambao kwa maoni yao wanadhani katika kutekeleza shughuli mbalimbali za usimamizi wa hizo hifadhi upo utekelezaji ambao una kasoro kwa sababu unaleta athari kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa haiwezekani kupata uhalisia, ukweli na uhakika bila kwenda kwenye uhalisia wenyewe. Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ameuliza Mawaziri hao wanaweza kuongozana naye kwenda kuona hali ilivyo huko au wale wananchi labda

kupitia viongozi wao kama wanaweza kupata fursa ya kuja Dodoma na kuweza kuonana na Waziri mwenye dhamana na Msaidizi wake wanaosimamia Maliasili.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwa kifupi kwamba hii ya pili itakuwa ni nyepesi zaidi kwa sababu ahadi zetu za kufika kwenye maeneo mbalimbali ambayo yana changamoto zinazohusiana na maliasili na utalii zinakuwa ni nyingi na muda unakuwa hautoshi. Kwa hiyo, kama hili la pili Mheshimiwa Mbunge anaweza kulitekeleza kwa urahisi zaidi ni jepesi zaidi. Hebu tupate viongozi kutoka huko, waje hapa na kile ambacho wanaona kwamba ni sahihi kwa upande wao halafu tutakuja hapa kuzungumza masuala haya kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kwa sababu suala hili la Kazimzumbwi limeshawekwa vizuri kwa mujibu wa sheria lakini kama zipo changamoto basi ni utaratibu tu wa Serikali sikivu kuweza kusikiliza wananchi wanasema nini.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge hebu fanya utaratibu wa kuweza kupata viongozi wanaotoka kwenye maeneo haya wakija hapa basi mimi na Mheshimiwa Waziri tutaweza kuona namna bora zaidi ya kuweza kuwasikiliza halafu tutaweza kuona namna ya kuweza kushughulikia matatizo yao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

SPIKA: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mwenyekiti wa *PAC*.

Na. 92

Kutengeneza Miundombinu ya Maji - Hifadhi ya Mkomazi

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatengeneza miundombinu ya maji katika Hifadhi ya Mkomazi ili kuzuia wanyamapori kuzurura kwenye makazi ya wananchi wakitafuta maji na kuharibu mazao yao?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la wananchi wa Same Mashariki, Naibu Waziri, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mhandisi Ramo Makani, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi inapatikana katika nyanda kame na hivyo kukabiliwa na uhaba wa maji kwa ajili ya matumizi ya wanyamapori. Wizara imefanya juhudi za kuchimba mabwawa kwa ajili ya kuhifadhi maji ambapo hadi sasa kuna jumla ya mabwawa tisa ambayo ni Mabata, Kuranze, Zange, Ndindira, Nobanda, Ngurunga, Mbula, Kavateta na Maore. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya tabianchi ni mabwawa matatu tu yanahifadhi maji mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hiyo ya upungufu wa maji, Serikali inaendelea kuchimba mabwawa sita ili kukidhi mahitaji ambapo bwawa moja lilikamilika katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 na mengine matano yatachimbwa katika mwaka huu wa fedha 2017/2018.

Aidha, katika mwaka 2017/2018 kisima kirefu kimoja kitachimbwa kwa ajili ya kusukuma maji na kujaza mabwawa yanayokauka ili kukidhi mahitaji ya maji wakati wa kiangazi kikali na wakati huo huo doria za kudhibiti wanyamapori wasitoke nje ya hifadhi zinaendelea kuimarishwa.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Same Mashariki, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, mwaka jana mwezi Julai tulikwenda na Mkurugenzi Mkuu wa TANAPA kutembelea vyanzo vya maji kutoka Milima ya Shengena ambayo inatiririsha maji mengi ambapo yanapita siyo mbali sana na hifadhi hii ya Mkomazi kwa upande wa Same Mashariki. Naye akaridhia kwamba kweli yale maji yangeweza kuchukuliwa na kusaidia sana ambapo yatakuwa ni maji ya kudumu kuliko haya mabwawa ambayo yanakauka mara kwa mara. Sasa nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, kitu gani kimefanya ule mpango usitekelezwe na badala yake wanakwenda tena kuchimba mabwawa wakati tumeshaona mabwawa kwanza ni hasara kubwa na pili maji yake yanakauka kila mara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Waziri yuko tayari kutuma wataalam wake wakatembelee tena hii mito hasa Mto wa Hingilili ambao ndiyo unashusha maji mengi na kulinganisha na tathmini yake na kuchimba mabwawa ni ipi rahisi? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo muhimu ya wananchi wa Same Mashariki, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza, anatoa taarifa juu ya ziara yake na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka za Hifadhi za Taifa Nchini (*TANAPA*) kwenye Milima ya Shengena ambapo analiambia Bunge lako Tukufu kwamba waliweza kuona uwezekano kwamba eneo lile ni chanzo cha maji ambacho kingeaminika zaidi na kwa hiyo anataka kujua kwa nini Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii isingetumia chanzo kile badala ya vyanzo hivi ambavyo tumevieleza hapa vya kutumia maji kutoka ardhini.

Mheshimiwa Spika, masuala haya ambayo ni ya kisayansi msingi wake mkubwa ni utafiti na baada ya ziara anayoizungumzia, kilichofanyika ni kuangalia faida na hasara yaani *cost benefit analysis* na baadaye gharama za kuweza kutekeleza mradi ule wa kujenga miundombinu na kukusanya maji kutoka kwenye Milima ya Shengena na kuyafikisha

kwenye maeneo yanayohitajika, katika hatua za awali, ilionekana kwamba gharama zake kwa sasa hivi hayawezi kuwa yanaweza kumudu kibajeti kuliko kujenga kisima au visima hivi tulivyovieleza hapa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuwa hicho ni chanzo ambacho ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kingeweza kuwa ni cha kuaminika na cha kudumu zaidi lakini kikwazo ni suala la uwezo wa kibajeti hatujafunga hilo dirisha. Hilo dirisha bado liko wazi lakini tusingeweza kukaa sasa kusubiri kufanya jambo kubwa na la gharama kubwa badala ya kufanya lile linalowezekana kwa sasa hivi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge akubaliane na Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kwamba kwa sasa tutaendelea kutumia njia hii ya visima vifupi na visima virefu wakati tukiwa tunaangalia uwezo wa kibajeti utakapokuwa umepanda basi tutatekeleza lile la pili.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kwa kweli linamezwa na swali la kwanza kwa sababu alitaka kujua kama tunaweza kutuma wataalam kwenda kuangalia ile mito ambayo iko kule na kuweza kuona kama inaweza kutumika kama vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, jibu lake ni lilelile tu kwamba katika mito anayoitaja hata kama tukienda sasa hivi itakuwa ni suala la kulinganisha gharama na kwamba Wizara imeona hatua hizi zinazochukuliwa kwa sasa hivi ni za mpito ambazo zinaweza kushughulikiwa na uwezo wa kibajeti uliopo, lakini njia zile nyingine za kudumu zaidi za muda mrefu zitaangaliwa hapo baadaye baada ya uwezo wa kibajeti kuwa umepanda.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa.

Na. 93

Usikivu Wa TBC Kyerwa

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawapatia wananchi wa Kyerwa haki yao ya kusikiliza Redio ya Taifa (TBC Taifa) ili kujua yanayoendelea katika nchi yao kama ilivyokuwa hapo awali kabla ya kubadilisha teknolojia ya habari, badala yake sasa wanasikiliza redio za Rwanda na Uganda.

SPIKA: Majibu ya swali hilo la wananchi wa Kyerwa, Naibu Waziri, Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Anastazia Wambura, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kyerwa iko katika Mkoa wa Kagera ambapo matangazo ya redio yanapatikana kupitia mtambo wa TBC ulioko katika Manispaa ya Bukoba. Mtambo huu unasafirisha mawimbi ya redio katika maeneo mbalimbali ya Mkoa huu wa Kagera ikiwemo wananchi wa Jimbo la Kyerwa. Usikivu wa TBC katika eneo hili umeshuka na kusababisha baadhi ya maeneo kukosa matangazo ya redio ikiwemo Jimbo la Kyerwa. Ili kuimarisha usikivu katika maeneo ya mipakani ikiwemo Wilaya ya Kyerwa, mpango wa TBC ni kujenga mitambo ya *FM* katika maeneo haya ili wananchi wake waweze kupata matangazo kutoka redio yao ya Taifa TBC.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa na kama ilivyobainishwa katika hotuba ya Bajeti ya Wizara ya mwaka 2017/2018 TBC imeanza kutekeleza mpango huu katika Wilaya na maeneo

ya Kibondo, Nyasa, Longido, Tarime na Rombo na itaendelea katika wilaya nyingine ikiwemo Wilaya ya Kyerwa kadri bajeti inavyoendelea kuimarika.

SPIKA: Mheshimiwa Bilakwate, swali la nyongeza.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imekiri kuwa Redio ya Taifa haisikiki katika Wilaya ya Kyerwa na wananchi hao wanapofungua redio wanapata Redio ya Rwanda na Uganda kitu ambacho kimewafanya wananchi hawa kuonekana kama wametengwa kwa sababu hawawezi kupata taarifa ambazo ni muhimu zinazohusu Taifa lao.

Je Serikali haioni kuwa wananchi hawa wamekosa haki yao ya msingi ya kupata habari za Serikali hasa hasa kutoka kwa viongozi wao kama Mheshimiwa Rais anapokuwa anaongea na viongozi wengine? Hata mimi Mheshimiwa Mbunge ninapokuwa Bungeni nawawakilisha, hawa wananchi hawapati taarifa yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali haioni haja ya kuchukua hatua za dharura ili wananchi hawa waweze kupata taarifa ya Redio ya Taifa kwa sababu wanakosa hii haki ya msingi? Laini hata Televisheni ya Taifa haisikiki wala haionekani vizuri. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, wananchi hawa wametengwa hawapati habari, Kyerwa huko, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Innocent Bilakwate. Pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Innocent kwa maswali yake mawili mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba unipe ridhaa ya kuelezea suala hili kwa kirefu kidogo kwa sababu tuna Wilaya karibu 84 ambazo hazina usikivu wa redio katika nchi hii na suala hili limesababisha Wabunge wengi mara kwa mara kuuliza maswali yanayohusiana na usikivu wa redio yao ya Taifa. Kwa hiyo, naomba nitoe ufafanuzi kidogo ili kusudi tuweze kusaidiana kwa pamoja na kuhakikisha kwamba tatizo hili linapata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza ametaka kujua kwamba Serikali haioni kwamba wananchi wanakosa haki yao ya msingi ya kusikiliza redio yao ya Taifa. Nitoe tu maelezo kwa kifupi kwamba kuna matatizo ambayo yanasababisha au tuseme kuna *factors* ambazo zinasababisha kuathiri usikivu wa redio katika maeneo mbali mbali. Kwanza, ukirudi nyuma tulikuwa tunatumia mitambo ya *medium wave* ambayo ilikuwa inaenea katika nchi nzima lakini kutokana na uchakavu wa mitambo hii na gharama kubwa ya kuinunua au kuikarabati imebidi sasa tuweke mitambo ya *FM* katika kila mkoa. Kwa hiyo, kila mkoa una mtambo wa *FM*.

Mheshimiwa Spika, sasa masuala ambayo yanaathiri usikivu kwanza ni *capacity* ya ule mtambo wenyewe lakini pia uwepo wa milima katika maeneo husika kwa mfano kama eneo la Mheshimiwa Innocent kuna milima mirefu ambayo mitambo hii inashindwa kuufikia. Suala lingine ambalo linaathiri usikivu ni ule uharibifu wa baadhi ya vifaa kama *power amplifier* ambao unatokana na matatizo mbalimbali kama vile radi au kukatika kwa umeme. Katika eneo la Mheshimiwa Innocent, kule Bukoba upo mtambo ambao kuna kifaa kimeharibika – *MOSFET* imeharibika na imekufa kabisa, kwa hiyo, usikivu umeathirika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, hatua za haraka ambazo tumeamua kufanya, kwanza nimeshatoa maagizo ili kusudi wataalam waende katika maeneo yake, katika Wilaya ya Kyerwa ili kuweza kuona jinsi gani ya kutatua tatizo hili kwa sababu kwanza uwezekano upo wa kuweka *booster*, lakini pia waone kama wanaweza wakanunua kifaa kile ambacho kimeharibika.

Vilevile kuna utaratibu ambao sasa hivi TBC inafanya kuubadilisha mfumo wa *satellite uplink* ambayo iko Mikocheni, tunaamini kabisa kwamba hii *satellite uplink* ikirekebishwa ikawa ya kisasa zaidi tutaboresha usikivu kwa asilimia takribani 15 hivi.

Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge ambao maeneo yao hayana usikivu, kufikia mwisho wa mwaka huu tunaamini kabisa hii *satellite uplink* inaweza ikawa imerekebishwa, kwa hiyo, usikivu utakapokuwa umeboreka katika maeneo yao watupe taarifa. Vilevile, kutokana na uharibifu wa vifaa katika vile vituo vyenyewe, yale maeneo ambayo yana usikivu wakati wowote watakapoona usikivu umesita katika maeneo yale watupe taarifa mapema ili kusudi wataalam wetu waweze kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tunafanya kwa sasa hivi ni huu utaratibu wa kuweka mitambo ya *FM* yaani kuongeza *transmitter* katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, nimetoa maagizo tayari kwamba wataalam wapite katika maeneo ya mipakani waone ni wapi panapostahili kuwekwa *boosters* lakini ni wapi pia ambao panastahili kuwekwa *transmitters* mpya. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Susan nilikuona, swali la nyongeza.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri anasema takribani Wilaya 84 hazipati usikivu. Swali langu, ni kwa nini sasa ile kauli mbiu ya TBC ya Ukweli na Uhakika msiifute na muwe na kauli mpya?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, hatuwezi kufuta hiyo kauli mbiu kwa sababu tunatoa taarifa za ukweli na za uhakika, haihusiani kabisa na usikivu. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru Naibu Waziri wa Habari kwa majibu ya uhakika na ukweli. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa Mheshimiwa *Engineer* Mheshimiwa Atashasta Julius Nditije, Mbunge wa Muhambwe, aulize swali lake.

Na. 94

Mahitaji ya Maji Gereza Kibondo

MHE. MHANDISI ATASHASTA J. NDI TIYE aliuliza:-

Gereza la Wilaya ya Kibondo – Nyamisati limekuwa na ongezeko kubwa sana la wafungwa na mahabusu kwa sababu ya uwepo wa wakimbizi.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati unaofaa kupeleka mradi mkubwa wa maji kwenye gereza hilo ili kulinda afya za raia na askari walioko kwenye gereza hilo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhali *Engineer* Masauni.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Nditije, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kuna tatizo la upatikanaji wa maji katika Gereza la Kibondo. Mwaka 2010, Serikali kupitia Jeshi la Magereza lilitenga fedha kiasi cha shilingi milioni 20 kwa ajili ya kuchimba kisima kirefu na kazi hiyo ilifanywa na Wakala wa Uchimbaji Mabwawa na Visima iliyopo Ubungo Dar es Salaam. Uchimbaji wa kisima hicho ulikamilika tarehe 2 Oktoba 2010 na kilikuwa na uwezo wa kutoa lita 2,300 kwa saa ambayo ni sawa na lita 55,200 kwa siku. Kiasi hiki ni kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya

maji ya Gereza la Kibondo ambayo ni lita 94,870 kwa siku, hivyo kuwa na upungufu wa takriban lita 39,670 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014 upembuzi yakinifu ulifanywa na wataalam wa Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Mhandisi wa Mamlaka ya Maji Wilaya ya Kibondo na kushauri kuwa ili gereza hilo liondokane na tatizo la maji, Jeshi la Magereza linapaswa kuvuta maji kutoka mtandao wa maji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo hadi gerezani ambapo gharama zake ilikadiriwa kuwa ni shilingi 330,492,450. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti, mradi huo haujatekelezwa hadi sasa. Serikali inaendelea kufanya jitihada mbalimbali ili kuhakikisha tatizo la maji Gereza la Kibondo linapata ufumbuzi wa kudumu.

SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa *Engineer* Atashasta.

MHE. MHANDISI ATASHASTA J. NDIYIYE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba tu kwanza nimpe taarifa tu kwamba maji yalitoka ndani ya miezi sita tu kama na siku nane halafu mpaka sasa hivi toka 2010 lile gereza halina maji ya uhakika na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati huu mradi unategenezwa kipindi kile tulikuwa hatuna wakimbizi sasa hivi ninapongea 2015 tumepokea wakimbizi 120,000 na kati ya hao kuna wahalifu mbalimbali ambao nao wanatumia gereza hilo ambalo kipindi hicho kulikuwa na upungufu wa lita 39,000. Tunapozungumzia kwamba maji ni uhai na kwa kuwa na idadi ya wafungwa sasa imeongezeka, Serikali ina mpango gani wa dharura hata wa kuwashirikisha *UNHCR* ambao ndiyo wana dhamana ya wakimbizi katika kutatua tatizo hilo? Hilo ni swali la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa sheria inawapa kinga wafungwa wa kisiasa na wafungwa wengi ambao wanatoka kwa wakimbizi siyo wa kisiasa, ni wafungwa wa makosa ya kawaida na kwa kuwa sasa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wameanza kurudishwa makwao, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuwarudisha wale wafungwa ambao wako kwenye gereza ili kupunguza idadi ya wafungwa? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mhandisi Masauni.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushauri wake wa kulichukulia kwa uzito unaostahili tatizo hilo ambalo yeye kwa kuwa ni Mbunge amekuwa karibu na gereza na ameona shida hiyo inaathiri vilevile wananchi la kuhusisha *UNHCR* ni wazo zuri na tutalichukua. Tumekuwa tukishirikiana na *UNHCR* kwa miradi mbalimbali ya maendeleo hasa katika maeneo ambayo wilaya/majimbo/vijiji vilivyopo karibu na maeneo ya wakimbizi ikiwemo maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatuoni kwa nini tusichukue na hili jambo tukaliingiza katika mpango huu hasa ukitilia maanani ni juzi tu Mheshimiwa Makamu wa Rais amezindua mpango kabambe ambao utaweza kuwanufaisha zaidi wananchi wanaohusika katika maeneo ambayo wakimbizi wanaishi. Kwa hiyo, ni wazo zuri ambalo tumelichukua kwa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hoja yake ya wafungwa ambao wamefungwa kwenye magereza, tuna utaratibu wa kubadilishana wafungwa katika nchi mbalimbali ambao upo kabisa kisheria na kupitia utaratibu huo hilo jambo linafanyika. Kwa hiyo, siyo jambo geni limekuwa likifanyika miaka yote tu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swali la mwisho la leo na ninyi mnaona muda wetu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 95

Ujenzi wa Chuo Cha Ufundi Stadi (VETA) – Simiyu

MHE. GIMBI D. MASABA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) katika Mkoa wa Simiyu na kukijengea uwezo wa kutengeneza vifaa vya baiskeli, pikipiki na magari?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mradi unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa mkopo wa masharti nafuu imeendelea na maandalizi ya ujenzi wa chuo kipya cha mafunzo ya ufundi stadi cha Mkoa wa Simiyu ambapo kwa sasa Wizara imempata mtaalam wa kusanifu majengo na kusimamia ujenzi wa chuo hicho. Usanifu wa majengo hayo unatarajiwa kukamilika Novemba, 2017. Baada ya usanifu wa majengo hayo, zabuni ya ujenzi itatangazwa na ujenzi wa chuo hicho unatarajiwa kuanza Februari, 2018.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuanza kwa ujenzi wa chuo hicho, Serikali inaendelea kuandaa mahitaji halisi ya rasilimali watu, mitaala itakayotumika, mashine na mitambo, samani na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Maandalizi hayo ni kwa ajili ya kujengea chuo uwezo wa kutoa mafunzo ya ufundi stadi na kuwapata wahitimu wenye

stadi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutengeneza vifaa vya baiskeli, pikipiki na magari.

SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa Gimbi.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Waziri alivyosema kwamba usanifu wa majengo utakamilika mwezi Novemba 2017, swali langu linauliza, ni maeneo gani yaliyobainishwa kujengwa chuo hicho? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wakati Serikali inaendelea na mpango wa kujenga Chuo cha VETA Mkoa wa Simiyu, Serikali ina mpango gani kuwasaidia vijana wanaomaliza kidato cha nne wanaokosa sifa ya kuendelea na kidato cha tano? (*Makof*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa *Engineer* Manyanya.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, Chuo cha Mkoa cha Simiyu kinategemewa kujengwa eneo ambalo lipo umbali wa takribani kilometa tisa mpaka kumi ambapo kilikuwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (*FDC*), eneo linalojulikana kama Kinamhala, nashindwa kidogo kutamka jina hilo, lakini ni eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika swali lake la pili juu ya Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne na hawajafanikiwa kidato cha tano. Kwanza ni kwamba tunavyo vyuo mbalimbali vinavyoweza kuchukua wanafunzi wa aina hiyo lakini vilevile Serikali kupitia mpango mpya wa *ESPJ*, mpango ambao unajipanga katika kuzalisha ajira nyingi kwa vijana wetu wale waliomaliza darasa la saba, kidato cha nne na ngazi nyingine zote ili waweze kupata ujuzi kamili wa kuweza kujajiri. Kwa hiyo, kuna fedha tumeshapata nyingi kabisa, niwafahamishe

tu Waheshimiwa Wabunge, Waziri wangu ameshatoa maelekezo kuwa kutakuwa na semina kwenu ya kuwapitisha juu ya mpango huo ambao utakuwa na manufaa makubwa sana katika nchi yetu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtaona muda wetu wa maswali umeisha. Sasa tunaendelea na matangazo kama ifuatavyo:-

Kwanza, naomba kuwatambua wageni wetu walioko katika *Gallery* ya Spika ambao ni pamoja na Bibi Sarah Cooke, Balozi wa Uingereza nchini Tanzania. Karibu sana Mheshimiwa Balozi, karibu Dodoma, karibu Bungeni. Tumefurahi sana kukuona ukiwa pamoja na sisi. (*Makofi*)

Amefuatana na Bibi Beth Arthy, Mwakilishi Mkazi wa *DFID*, Bwana Marc Thayre, Mkuu wa Idara ya Siasa, Vyombo vya Habari na Masuala ya Umma na Bwana Ernest Sylvest, mtumishi wa Ubalozi, karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tuna wageni waliopo katika Jukwaa la Spika nao ni Katibu Mkuu Uchukuzi, Dkt. Leonard Chamuriho akiwa na wageni sita wa Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni viongozi kutoka Wizarani. Naomba msimame wageni wa Mheshimiwa Waziri, karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 130 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu ambao ni wanafunzi 125 wa kidato cha sita na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya Jamhuri Mkoa wa Dodoma. Jamhuri karibuni, hii ni awamu nyingine ya wanafunzi wa Jamhuri. Jana niliwaita Yangeyange na mnaona wanavyozidi kupendeza. Ahsanteni sana kidato cha sita tunawatarajia wote mtaenda Chuo Kikuu. (*Makofi*)

Wageni waliotutembelea kwa ajili ya mafunzo ni watumishi watatu wa Bunge la Uganda waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. *Staff of Ugandan Parliament*, karibuni popote pale mlipo. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mwanafunzi kutoka Chuo cha Tumaini ambaye amekuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, karibu pia. (Makofi)

Tangazo la mwisho ni kwa Waheshimiwa Wabunge wakristo wakatoliki, leo Jumatano, tarehe 13 Septemba, 2017 kutakuwa na ibada ya misa mara baada ya kuahirishwa Bunge katika Kanisa dogo lililopo ghorofa ya pili, ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wengine wote mnakaribishwa kushiriki ibada hii takatifu. Wabunge wakatoliki, saa saba mchana kwenye ukumbi wenu wa kawaida wa ibada na tangazo hili limeletwa na *Sister Cecilia Paresso*. (Makofi/Kicheko)

Ndiyo hii jana nilikuwa namwambia Mheshimiwa Ally Saleh mimi natangaza tu ndugu yangu sasa ukinilaumu kama nimeidhinisha haya, wajibu wangu tu kutangaza, kwa hiyo, usikasirike Mheshimiwa Ally Saleh.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka jana tulielekeza pamoja na mambo mengine kwamba Mheshimiwa Zitto Kabwe anatakiwa atokeze katika Kamati ya Maadili ili ajieleze kidogo katika mambo yanayohusisha kudhalilisha mhimili wa Bunge. Kwa kiburi kikubwa ameendelea tena kudhalilisha mhimili wa Bunge. Kwa maneno mengi ambayo mengine yote ni ya kupuuza Waheshimiwa Watanzania, ni mtu anayejaribu kufanya *divide and rule* kwa kujaribu sana kulinganisha uongozi wa sasa na uongozi wa Bunge la Kumi la wa Mheshimiwa Mama Makinda na uongozi wa Bunge la Tisa la Mheshimiwa Spika Sitta.

Kwanza nimwambie yeye na wengine wote wanaojaribu sana kufanya milinganisho ambayo haina maana, kila Bunge la miaka mitano huwa ni tofauti sana na Bunge lingine, tofauti kabisa. Kwa hiyo, sitaki kuingia kwenye kuchambua kwa sababu nikichambua hapa na nina uwezo huo wa kuchambua sana kwa sababu nilikuwepo kote huko lakini nimwambie kwamba Mheshimiwa Sitta na Mheshimiwa Makinda ni walimu wangu na hata siku moja sikio haliwezi kuzidi kichwa. Hawa ni watu ninaowaheshimu sana,

wamenilea na ni sehemu ya kunifikisha hapa nilipo. Kwa hiyo, mimi ni kichuguu tu, sasa utalinganishaje na milima mikubwa kama Mlima Kilimanjaro? Kwa hiyo, fitina yake hiyo wala haifanyi kazi, haina maana kabisa. *(Makofi)*

Vilevile nimkumbushe wakati wa Bunge la Tisa, Mheshimiwa Zitto aliwahi kuleta hoja fulani hapa Bungeni, wengi wenu hamkuwepo, sisi tulikuwepo. Ilikuwa ni hoja ya maana tu, nzuri inahusu Buzwagi, akaileta hapa, akaiwasilisha hapa, hoja yake ikakataliwa hapa hapa ilikuwa jioni. Akaanzishiwa hoja nyingine hapa hapa ya kukosa maadili fulani fulani akahukumiwa hapa hapa saa hiyo hiyo, yaani hoja ikaanza saa hiyo hiyo, ikajadiliwa saa hiyo hiyo akahukumiwa saa hiyo hiyo akapigwa nje zaidi ya miezi mitatu. Sasa mimi angalau namuanzia kule kwenye Kamati ya Maadili ajieleze angalau au anataka niende mkukumkuku kama huo huo wa Bunge la Tisa ili aone kwamba Ndugai anafanana na Mzee Sitta, hilo pia naliweza. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, yaani mnaalika matatizo mimi nawashangaa, wewe Zitto utapambana na Spika kweli? Naweza kukupiga marufuku kuongea humu mpaka miaka yako yote ikaisha na hakuna pa kwenda. Hakuna cha swali, hakuna cha nyongeza, hakuna cha kuongea chochote humu ndani ya Bunge utanifanya nini? Pambana na kitu kingine siyo Ndugai. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa haya ya Ndugai na nini wala sina matatizo nayo ila ya kudhalilisha mhimili ambayo anaendelea kuyafanya hayo siwezi kuyaacha, kwa sababu ni wajibu wangu kulinda mhimili huu kwa nguvu zangu zote. Nikiruhusu Wabunge ninyi kuwa mnadhalilisha mhimili tutazuiaje Watanzania wengine kudhalilisha mhimili huu, haiwezekani. Kwa hiyo, hili ni kosa la pili na lenyewe linaenda kwenye Kamati ya Maadili pia la kudhalilisha mhimili kwa yale maandishi yake ya jana. Tutakwenda pamoja, sambamba, mguu kwa mguu mpaka kitaeleweka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hapa tulipofika tumemaliza shughuli hii, leo hakuna mwongozo wala nini tutaendelea

na Miswada ya Serikali. Sasa naomba nimpishe Mheshimiwa Naibu Spika.

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Reli wa Mwaka 2017
(The Railways Bill, 2017)

(Kusomwa Mara ya Pili)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Reli wa mwaka 2017 *(The Railways Act, 2017)* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti Profesa Norman Sigalla King, Mbunge wa Makete kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu kwa kiasi kikubwa umezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuandaa muswada huu pamoja na marekebisho yake na wadau mbalimbali wa sekta ndogo ya usafiri wa reli ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa sheria itakayoanzisha Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) ambalo pamoja na mambo mengine litakuwa na jukumu la kusimamia kuendeleza miundombinu ya reli na kutoa huduma ya usafiri wa reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya muswada huu ni kuweka mfumo madhubuti wa utoaji huduma ya usafiri wa reli na usimamizi na uendeshaji wa miundombinu ya reli.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika muswada huu ni pamoja na:-

(i) Kuanzisha Shirika jipya la Reli la Tanzania na kuainisha majukumu, wajibu na mamlaka yake;

(ii) Kuainisha wajibu wa uteuzi, mamlaka na majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi;

(iii) Kuweka utaratibu wa uteuzi, majukumu na sifa za Mtendaji Mkuu;

(iv) Kuainisha vyanzo vya mapato ambavyo ni pamoja na Mfuko wa Reli, ruzuku kutoka Serikalini, nauli za abiria pamoja na tozo za usafirishaji wa mizigo;

(v) Kumtambua mdhibiti wa masuala ya uchumi na usalama katika sekta ya usafiri wa reli;

(vi) Kuainisha utaratibu wa kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo;

(vii) Kuainisha utaratibu wa kuratibu ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya reli ikiwa ni pamoja na uhifadhi wa eneo la reli;

(viii) Kuainisha utaratibu wa kusimamia masuala ya hifadhi ya mazingira kwenye mtandao wa reli ya Taifa;

(ix) Kuainisha utaratibu wa kuhamisha watumishi kutoka *TRL* na *RAHCO* kwenda katika shirika jipya;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(x) Kuainisha utaratibu wa kusimamia masuala ya fedha ili kuhakikisha kuwepo kwa matumizi sahihi ya fedha na mali nyingine za Serikali;

(xi) Kuainisha makosa na adhabu;

(xii) Mamlaka ya Waziri kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa sheria inayopendekezwa; na

(xiii) Kufuta Sheria ya Reli Na. 4 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi na Moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada huu inahusu utangulizi ambao unaainisha jina la Muswada, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria, matumizi yake na ufafanuzi wa maneno na misemo iliyotumika katika sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Pili inapendekeza kuanzishwa kwa Shirika la Reli Tanzania na madhumuni ya kuanzishwa kwake. Vilevile sehemu hii inaainisha majukumu ya shirika, mamlaka yake katika kuendeleza miundombinu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, utulie kidogo, Waheshimiwa Wabunge mnapiga kelele sana. Wako Waheshimiwa Wabunge humu ndani ambao wanataka kufuatilia mazungumzo anayotoa Mheshimiwa Waziri. Wote hapa ndani tunayo fursa ya kuzungumza na mwenzako lakini zungumza taratibu basi, humu ndani wako watu wamekuja kujifunza namna yetu ya uendeshaji Bunge. Kama ni lazima uzungumze kwa sauti toka nje kidogo halafu urudi, tafadhali tusifike mahali sasa tukaanza kutaja watu ili watulie. Mheshimiwa Waziri endelea. *(Makofi)*

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi na Moja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada huu inahusu utangulizi ambao unaainisha jina la Muswada, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria, matumizi yake na ufafanuzi wa maneno na misemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili inapendekeza kuanzishwa kwa Shirika la Reli Tanzania na madhumuni ya kuanzishwa kwake. Vilevile sehemu hii inaainisha majukumu ya shirika, mamlaka yake katika kuendeleza miundombinu na kutoa huduma za usafiri wa reli.

Sehemu ya Tatu inahusu kuanzishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi, mamlaka na majukumu ya Bodi, uteuzi wa Mwenyekiti, Wajumbe na Kamati za Bodi ya Wakurugenzi, masuala yatakayosababisha kuwepo kwa mgongano wa kimaslahi dhidi ya Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi pamoja na stahili zao. Baadhi ya majukumu ya Wajumbe wa Bodi ni kupitisha sera ya uendeshaji wa shirika, kusimamia matumizi bora ya rasilimali, kupitisha mpango kazi, bajeti na taarifa za fedha za mwaka. Aidha, sehemu hii inaainisha kuwa Mwenyekiti wa Bodi atateuliwa na Mheshimiwa Rais na Wajumbe wa Bodi watateuliwa na Waziri.

Sehemu ya Nne imeweka masharti kuhusu utawala wa shirika, uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, Wakuu wa Idara na watumishi wengine. Aidha, sehemu hii inaainisha kuwa Mkurugenzi Mkuu ndiye Mtendaji Mkuu wa shirika na atachaguliwa na Mheshimiwa Rais kwa njia ya ushindani kwa kuzingatia sheria na taratibu za utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tano inahusu kazi za ujenzi na matengenezo ya reli. Sehemu hii inatoa mamlaka kwa shirika kwa kutwaa ardhi kwa ajili ya matumizi ya miradi ya reli. Sehemu hii pia inaainisha masuala ya tathmini ya athari ya mazingira pamoja na mambo mengine yanayohusu ardhi ya shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Sita ina vifungu vinavyohusu kinga dhidi ya shirika kutokana na vifo vya abiria, majeraha, kuchelewa kwa mizigo, upotevu wa mizigo,

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wanyama ambao thamani yake inazidi kiwango kinachoainishwa na shirika, taarifa za uongo na bidhaa zilizohifadhiwa katika maghala ya shirika. Kinga inayopendekezwa ni dhidi ya bidhaa zisizoainishwa, vifo na majeraha yanayotokana na uzembe au sababu zilizo nje ya mamlaka ya shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Saba inaainisha taratibu za utoaji wa tiketi, bidhaa zisizoruhusiwa, vigezo vya ubebaji wa mizigo, taratibu za kufuatwa na shirika iwapo abiria atashindwa kulipa nauli na taratibu za kushughulikia mizigo iliyotelekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nane inahusu udhibiti wa shughuli za huduma za usafiri wa reli. Sehemu hii inaainisha majukumu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Reli. Baadhi ya masuala ambayo yatadhibitiwa ni pamoja na viwango vya nauli, tozo, usalama na ubora wa huduma inayotolewa.

Sehemu ya Tisa inahusu masuala ya fedha. Sehemu hii ina vifungu vinavyohusu vyanzo vya mapato, mwaka wa fedha, bajeti mahususi na ukaguzi wa mahesabu pamoja na taarifa ya utendaji ya mwaka. Aidha, sehemu hii inaainisha kwamba taarifa ya mwaka ya utendaji wa shirika itawasilishwa kwa Waziri ambaye ataiwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi inahusu makosa na adhabu. Baadhi ya makosa yaliyoainishwa ni matumzi ya ardhi ya dharura bila ridhaa ya reli, kuhatarisha usalama wa maisha ya watu wanaosafiri na treni au walio katika reli, kuweka au kutupa vitu hatarishi katika miundombinu ya reli kama vile mbao na mawe. Makosa mengine ni ulevi kazini, kugushi tiketi, kusafiri bila tiketi, kusafirisha bidhaa hatarishi kinyume na taratibu na wafanyakazi wanaohatarisha usalama wa huduma za reli. Aidha, kuna kifungu kinachotoa adhabu ya jumla kwa maeneo ambayo adhabu hajjaainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Moja inahusu masuala ya jumla kama vile mamlaka ya Waziri

kutunga kanuni, mamlaka ya shirika kubadilisha uelekeo wa maji kwa ajili ya ujenzi na ulinzi wa miundombinu ya reli, ujenzi wa makutano ya reli na barabara, matumizi ya reli wakati wa ujenzi, utengaji wa ardhi kwa ajili ya matumizi ya reli wakati wa kuandaa mpango kabambe, utunzaji wa nyaraka za reli na kufutwa kwa Sheria ya Reli ya mwaka 2002.

Vilevile Muswada huu unaainisha masuala ya wafanyakazi na stahili zao. Watumishi wa *RAHCO* na *TRL* wanaokidhi vigezo watahamishiwa katika shirika jipya na wengine katika Wizara au taasisi mbalimbali za umma. Aidha, watumishi ambao hawatahamishiwa katika shirika jipya Wizara au Taasisi nyingine za Umma, ajira zao zitaitishwa na watalipwa stahili zao zote kwa mujibu wa sheria na kwa kuzingatia masharti na vigezo vya ajira zao. Wafanyakazi ambao watahamishiwa katika shirika jipya na walikuwa wanachangia katika Mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii, wataendelea kuratibiwa na sheria za mifuko hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mali na madeni yote ya *RAHCO* na *TRL* yatahamishiwa katika shirika jipya. Vilevile Muswada huu unaainisha kwamba mikataba, makubaliano, kanuni na nyaraka nyingine zilizoandaliwa na kutungwa kabla ya sheria hii zitaendelea kutambuliwa mpaka zitakapositishwa au zitakapobatilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha Muswada huu ili Waheshimiwa Wabunge waujadili na hatimaye waukubali na kuupitisha ili nchi yetu iweze kuwa na mfumo madhubuti wa utoaji wa huduma ya usafiri wa reli, usimamizi na uendelezaji wa miundombinu ya reli kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(*Makofi*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

**MUSWADA WA SHERIA YA RELI WA MWAKA 2017
(THE RAILWAYS BILL, 2017) - KAMA UILIVYOWASILISHWA
MEZANI**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

SPECIAL BILL SUPPLEMENT

No. 6

3rd September, 2017

to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No. 6 Vol. 98 dated 3rd September, 2017

Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

THE RAILWAYS ACT, 2017

ARRANGEMENT OF SECTIONS

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

Section Title

1. Short title and commencement.
2. Application.
3. Interpretation.

PART II
TANZANIA RAILWAYS CORPORATION

4. Establishment of Corporation.
5. Objects of Corporation.
6. Functions of Corporation.
7. Protection of assets from execution or attachment.
8. Power to develop, maintain and provide rail infrastructure and services.
9. Power to delegate.
10. Preparation of Tariff Book.

PART III
BOARD OF THE CORPORATION

11. Establishment of Board.
12. Composition of Board.
13. Functions of Board.
14. Powers of Board.
15. Power of Board to appoint a committee.
16. Power of Board to delegate.
17. Observance of impartiality.
18. Conflict of interest.

19. Superannuation benefits.

PART IV
ADMINISTRATION AND MANAGEMENT OF THE CORPORATION

20. Appointment of Director General.
21. Duties and powers of Director General.
22. Corporation Secretary.
Employees whose employment will be terminated will be paid terminal benefits in accordance with the laws governing the terms and conditions of their service before termination. Employees who will be transferred to the Corporation and are members of any statutory, pension fund or any other superannuation scheme will continue to be governed by

the same laws under those funds or laws. All assets, interest, right, privileges, liabilities or obligations vested to RAHCO and TRL will be transferred and vested to the Corporation.

Further, the Bill proposes to retain all the undertaking made or deemed to have been prepared, subsidiary legislation, exemptions given or made before the commencement of this Bill shall remain in force until revoked, replaced or rescinded.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutunga Sheria mpya ya kuanzisha Shirika la Reli Tanzania, madhumuni na majukumu yake. Aidha, Shirika litakaloanzishwa pamoja na mambo mengine litakuwa na jukumu la kusimamia, kuendeleza miundombinu ya reli na kutoa huduma za usafiri wa reli.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu kuu Kumi na moja.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada huu inahusu utangulizi ambao unaainisha jina la Muswada, tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria, matumizi yake na ufafanuzi wa maneno na misemo iliyotumika katika Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Pili inapendekeza kuanzishwa kwa Shirika la Reli Tanzania na madhumuni ya kuanzishwa kwake. Vilevile Sehemu hii inaainisha majukumu ya Shirika, mamlaka yake katika kuendeleza miundombinu na kutoa huduma za usafiri wa reli.

Sehemu ya Tatu inahusu kuanzishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi, mamlaka na majukumu ya Bodi, uteuzi wa Mwenyekiti, wajumbe na kamati za Bodi ya Wakurugenzi, masuala yatakayosababisha kuwepo kwa mgongano wa kimaslahi dhidi ya Mwenyekiti na wajumbe wa Bodi pamoja na stahili zao. Baadhi ya majukumu ya wajumbe wa Bodi ni kupitisha sera ya uendeshaji wa Shirika, kusimamia matumizi bora ya rasilimali, kupitisha mpango kazi, bajeti na taarifa za fedha za mwaka. Aidha, sehemu hii imeainisha kuwa Mwenyekiti wa Bodi atateuliwa na Rais na wajumbe wa Bodi watateuliwa na Waziri.

Sehemu ya Nne inaweka masharti kuhusu utawala wa Shirika, uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, Katibu wa Shirika ambaye pia ndiye atakayekuwa Katibu wa Bodi, Wakuu wa Idara na watumishi wengine. Aidha, Sehemu hii imeainisha kuwa Mkurugenzi Mkuu ndiye Mtendaji Mkuu wa Shirika na atachaguliwa na Waziri kwa njia ya ushindani kwa kuzingatia Sheria za Utumishi wa Umma.

Sehemu ya Tano inahusu kazi za ujenzi na matengenezo ya reli. Sehemu hii inatoa mamlaka kwa Shirika ya kutwaa ardhi kwa ajili ya matumizi ya miradi ya reli. Sehemu hii pia inaainisha masuala ya Tathimini ya Athari za Mazingira pamoja na mambo mengine yanavyohusu ardhi ya Shirika.

Sehemu ya Sita ina vifungu vinavyohusu kinga dhidi ya Shirika kutokana na vifo vya abiria, majeraha, kuchelewa kwa mizigo, upotevu wa mizigo, wanyama ambao thamani yake inazidi kiwango kilichoainishwa na Shirika, taarifa za uongo na bidhaa zilizohifadhiwa katika

maghala na Shirika. Kinga inayopendekezwa ni dhidi ya bidhaa zisizoainishwa, vifo na majeraha yatokanayo na uzembe au sababu zilizo nje ya mamlaka ya Shirika.

Sehemu ya Saba inaainisha taratibu za utoaji wa tiketi, bidhaa zisizoruhusiwa, vigezo vya ubebaji wa mizigo, taratibu za kufuatwa na Shirika iwapo abiria atashindwa kulipa nauli na taratibu za kushughulikia mizigo iliyotelekezwa.

Sehemu ya Nane inahusu udhibiti wa shughuli za huduma za usafiri wa reli. Sehemu hii inaainisha majukumu ya Mamlaka. Baadhi ya masuala ambayo yatadhibitiwa ni pamoja na ushindani wa kibiashara, viwango, usalama na ubora wa huduma inayotolewa.

Sehemu ya Tisa inahusu masuala ya fedha. Sehemu hii ina vifungu vinavyohusu vyanzo vya mapato, mwaka wa fedha, bajeti, mahesabu na ukaguzi wa mahesabu pamoja na taarifa ya utendaji ya mwaka. Aidha, Sehemu hii imeainisha kwamba taarifa ya mwaka ya utendaji wa Shirika itawasilishwa kwa Waziri ambaye ataiwasilisha Bungeni.

Sehemu ya Kumi inahusu makosa na adhabu. Baadhi ya makosa yaliyoainishwa ni matumizi ya ardhi ya dharura bila ridhaa ya Shirika, kuhatarisha usalama wa maisha ya watu wanaosafiri na treni au walio katika reli, kuweka au kutupa vitu hatarishi katika miundombinu ya reli kama vile mbao na mawe. Makosa mengine ni ulevi kazini, kugushi tiketi, kusafiri bila tiketi, kusafirisha bidhaa hatarishi kinyume na taratibu na wafanyakazi wanaohatarisha usalama wa huduma za reli. Aidha, kuna kifungu kinachotoa adhabu ya jumla kwa maeneo ambayo adhabu haijaainishwa.

Sehemu ya Kumi na Moja inahusu masuala ya jumla kama vile, mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni, uwezo wa Waziri kuanzisha kampuni tanzu, Mamlaka ya Shirika kubadilisha uelekeo wa maji kwa ajili ya ujenzi na ulinzi wa miundombinu ya reli, ujenzi wa makutano ya reli na barabara, matumizi ya reli wakati wa ujenzi, utengaji wa ardhi kwa ajili ya matumizi ya reli wakati wa kuandaa Mpango Kamambe, utunzaji wa nyaraka za reli na kufutwa kwa Sheria ya Reli, 2002.

Vile vile Muswada umeainisha masuala ya wafanyakazi na stahili zao. Watumishi wa RAHCO na TRL wanaokidhi vigezo watahamishiwa katika Shirika jipya na wengine katika Wizara au taasisi mbalimbali za Umma. Aidha, watumishi ambao hawatahamishiwa katika Shirika jipya, Wizarani au taasisi nyingine za Umma ajira zao zitasitishwa na watalipwa stahiki zao zote kwa mujibu wa Sheria na kwa kuzingatia masharti na vigezo vya ajira zao.

Wafanyakazi ambao watahamishiwa katika Shirika jipya na walikuwa wanachangia katika mifuko mbalimbali ya hifadhi ya jamii wataendelea kuratibiwa na Sheria za Mifuko hiyo. Mali na madeni yote ya RAHCO na TRL yatahamishiwa katika Shirika jipya. Vile vile Muswada umeainisha kwamba mikataba, makubaliano, kanuni na nyaraka nyingine zilizoandaliwa na kutungwa kabla ya Sheria hii zitaendelea kutambulika mpaka zitakapoitishwa au zitakapobatilishwa.

Dodoma,
20 Agosti, 2017

MAKAME M. MBARAWA
Waziri wa Ujenzi, Uchukuji na Mawasiliano

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, tunaendelea na sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso.

MHE. MOSHI M. KAKOSO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, ifuatayo ni Taarifa ya Maoni ya Ushauri wa Kamati wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miondombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Reli ya Tanzania ya mwaka 2017 (*The Railways Act, 2017*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, napenda kutumia fursa hii kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Reli ya Tanzania ya mwaka 2017 (*The Railways Act, 2017*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaanza kwa kutoa pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Rais na Serikali kwa hatua kubwa zilizochukuliwa katika kuimarisha sekta ya reli nchini. Muswada huu ni ishara tosha ya kazi kubwa ambayo imefanyika katika muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 7(1)(b) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, inazipa Kamati za Bunge za Kisekta ikiwemo Kamati ya Miundombinu jukumu la kushughulikia miswada ya sheria na mikataba iliyo chini ya Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, muswada huu umeletwa kwa Hati ya Dharula na hivyo kuwa na siku chache za Kamati kuupitia na kuujadili. Tarehe 9 Septemba, 2017 Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Mbunge, aliwasilisha mbele ya Kamati muswada huu, ambapo pamoja na maelezo mengine, alijulisha Kamati manufaa mbalimbali yatakayotokana na kupitishwa kwa sheria hii kwa maendeleo ya sekta ya reli nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda ambao Kamati imepokea Muswada huu kuwa mfupi wadau mbalimbali walialikwa lakini hawakuweza kufika na kuwasilisha maoni yao mbele ya Kamati. Kamati inawashukuru sana Chama cha Wafanyakazi wa Reli Tanzania (*TRAWU*) kwa kufika na kutoa maoni yao mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia fupi ya reli nchini Tanzania; reli ilianza kujengwa na wakoloni Wakijerumani kuanzia Dar es Salaam kwenda Kigoma mwaka 1905 – 1914; wakati huo Shirika la Reli Tanzania lilianzishwa likiitwa Reli ya Tanganyika; ambalo lilikuwa likisimamia Reli ya Kati kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma kwenye Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajerumani walipoondoka (1918) Tanganyika ilitawaliwa na Waingereza kama eneo la udhamini la Shirikisho la Mataifa ambalo kwa sasa linajulikana kama Umoja wa Mataifa na kupata Uhuru mwaka 1961, katika kipindi hicho, Reli ya Tanganyika iliongezwa njia ya kando kutoka Tabora hadi Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1948, huduma zote mbili, yaani reli na bandari ziliunganishwa na hivyo kuanzishwa kwa Shirika jipya la *East Africa Railways & Harbors* ambalo lilikuwa shirika jipya lililosimamia na kutekeleza kazi za reli, bandari za baharini pamoja na huduma za meli kwenye maziwa makubwa ya Victoria (Nyanza), Tanganyika na Nyasa. Shirika hilo jipya liliendelea kuongeza mtandao wa reli, kuboresha huduma za meli kwa kuleta meli mpya katika Ziwa Victoria ambapo mwaka 1967 Jumuiya ya nchi tatu kubwa za Afrika Mashariki ilianzishwa. Hata hivyo, kutokana na changamoto mbalimbali Jumuiya hiyo ilivunjika mwaka 1977. Kuvunjika kwa Jumuiya hii kulisababisha Shirika la Reli (*East Africa Railways*) kuvunjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuvunjika kwa umoja huo ndipo njia za reli, bandari na meli ziligawanywa kati ya nchi tatu zilizokuwa za umoja huo. Shirika la Reli Tanzania lilianzishwa likiwa na matawi ya Dar es Salaam -

Kigoma, Tabora - Mwanza na Kaliua - Mpanda. Kwa upande wa Kenya na Uganda zilianzisha mashirika yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuanzishwa kwa *RAHCO* na *TRL*; mwaka 2007 Shirika la Reli Tanzania lilivunjwa na lilianzishwa shirika lingine kwa ajili ya kumiliki miundombinu ya reli nchini (*Railways Holding Company – RAHCO*). Mwaka huo huo shughuli za uendeshaji wa usafiri wa reli zilihamishiwa kwa *Tanzania Railways Limited (TRL)* na Kampuni ya *rites* kutoka India iliyoingia ubia wa uendeshaji kwa makubaliano ya kuwa na hisa asilimia 49 kwa Tanzania na asilimia 51 kwa *rites*.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya madhumuni ya Serikali kubinafsisha Shirika la Reli Tanzania ilikuwa ni kuweka mazingira ya kuwa na makampuni mengi ya usafirishaji kwa njia ya reli hivyo kurahisisha makampuni hayo kuweza kulipia huduma ya utumiaji wa njia na kubaki kushughulika na uendeshaji peke yake. Hata hivyo, ubinafsishaji huo haukuleta mafanikio yaliyokuwa yanatarajiwa na kusababisha mwaka 2011 Serikali ya Tanzania kuvunja mkataba wake na *rites* na kurejea umiliki na uendeshaji wa Shirika la Reli kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ambayo imekuwa ikikabili uendeshaji wa reli pamoja na uchukuzi wa abiria na mizigo, ni kutokuwepo uwajibikaji wa pamoja kati ya haya mashirika mawili yaani *RAHCO* na *TRL*. Kwa mfano, panapotokea miundombinu ya reli imeharibika au kusombwa na maji, *TRL* imejikuta ikilazimika kugharamia matengenezo ya kipande cha reli husika ili iweze kuendelea kusafirisha abiria wake haraka iwezekanavyo na hivyo kupunguza usumbufu kwao na pia kuepuka kuingia gharama zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni, miongoni mwa malengo yaliyowekwa na Serikali kuhusu kuimarisha miundombinu ya reli nchini ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* ambapo Serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha. Kutokana na

uwekezaji huo mkubwa imeonekana ni muhimu kuunda chombo madhubuti kwa ajili ya usimamizi wa miundombinu hii ambayo inaligharimu Taifa fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Reli wa 2017 unaanzisha Shirika jipya la Reli ambalo pamoja na mambo mengine litakuwa na jukumu la kusimamia, kuendeleza miundombinu ya reli na kutoa huduma za usafiri wa reli. Sheria hii itatumika Tanzania Bara pekee na haitatumika katika uendeshaji wa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA).

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya shirika hili yatakuwa ni kutoa huduma za usafiri wa reli, kujenga na kuendeleza miundombinu ya reli, kuhamasisha na kutunza miundombinu ya reli, kufanya matengenezo ya reli na kuhakikisha kunakuwa na ulinzi na usalama wa miundombinu ya reli pamoja na kuingia kwenye mikataba mbalimbali, ili kulinda masharti ya huduma ya usafirishaji kwa njia ya reli. Mikataba hiyo inaweza kuwa baina ya Serikali na watu binafsi kwa ajili ya kukasimisha madaraka yake ya kuendeleza na kutunza miundombinu ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia uchambuzi uliofanywa na Kamati, yafuatayo ni maoni na ushauri wake:-

(i) Kifungu cha 20(1) kinachoongelea Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji. Kifungu kidogo cha (5) kimeongelea jukumu la Mkurugenzi Mtendaji. Kamati inaona kwamba kifungu hiki kihamie kwenye kifungu cha 21 kinachohusu majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji.

(ii) Kifungu cha 21 kinachoeleza kazi na Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji, kitamke bayana kuwa Mamlaka yake na kazi zake zinatekelezwa chini ya uongozi na udhibiti wa Bodi kama ilivyoainishwa katika kifungu 20(5).

(iii) Kifungu cha 21(1)(b) kinachoongelea jukumu la Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika kuandaa na kutekeleza Kanuni za Maadili kwa Watumishi. Muswada huu

haujabainisha ni nani anayetakiwa kupitisha Kanuni hizo za maadili kwa watumishi baada ya kuwa zimeandaliwa na Mkurugenzi Mtendaji. Kamati inashauri wajibu huo wa kupitisha Kanuni uwe ni jukumu la Bodi.

(iv) Kifungu cha 21(1)(k) kinaeleza kuhusu kuanzisha na kuendesha reli. Kamati inaona kuwa jukumu hili silo la Mkurugenzi Mtendaji badala yake jukumu hilo ni la Shirika hivyo ni ushauri wa Kamati jambo hili kupelekwa kwenye majukumu ya Shirika.

(v) Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 23(7) kinampa Mamlaka Mkurugenzi Mtendaji kutokuzingatia utaratibu wa kiushindani wakati wa kuteuwa watumishi, washauri wa kitaalam au wataalam endapo kuna uharaka wa uteuzi au mazingira mengine maalum. Kamati inashauri kifungu hiki kifanyiwe mabadiliko, hasa kwa upande wa uteuzi wa washauri wa kitaalam ambapo mchakato wake unatakiwa kupitia Sheria ya Manunuzi ya Umma na hivyo mamlaka yake yazingatie Sheria ya Manunuzi ya Umma ambayo kwenye kifungu cha 65 kinatoa utaratibu huo.

(vi) Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 26 kinaongelea utafiti na ukaguzi. Afisa aliyeidhinishwa na Shirika anaweza kuingia kwenye nyumba au eneo la mwananchi yeyote na kufanya ukaguzi na utafiti kwa lengo la kutathmini kama eneo hilo linafaa kwa ajili ya ujenzi wa reli. Pamoja na kwamba anatakiwa kupata kibali cha mwenye nyumba au eneo husika, Kamati inashauri wakati wa ukaguzi huo, ikiwa eneo hilo ni mali ya Shirika la Reli, ni muhimu kuwepo Afisa wa Serikali ya Mtaa kwa ajili ya kujua kinachoendelea kwa wananchi wa mtaa wake. Ikiwa eneo hilo ni jipya, Kamati inashauri Waziri aweke Kanuni za kufuata katika utekelezaji wa jukumu hilo ili kuzingatia matakwa ya Sheria nyingine husika hususan Sheria ya Ardhi.

(vii) Kifungu cha 60 kinaongelea uanzishwaji wa Mamlaka ya Mdhibili. Kifungu hiki hakijaeleza kama mdhibiti huyo ni mtu binafsi au ni Kampuni. Hivyo Kamati inashauri kama ni mtu binafsi kifungu hiki kibaki kama kilivyo lakini

ikiwa ni Kampuni kifungu cha 60(3) kitumie neno "*its*" na si "*his*". Aidha, Kamati inashauri kutolewa tafsiri ya neno "*Regulator*" ili kuleta maana ya anayekusudiwa kutajwa katika Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine ambayo Kamati inashauri ni kama yafuatayo:-

(a) Wakati Sheria hii inapitishwa Serikali inashauriwa kuangalia kwa umakini suala la mishahara kwa wafanyakazi kwani wafanyakazi wa *RAHCO* walikuwa na mishahara mikubwa ukilinganisha na wafanyakazi wa lililokuwa Shirika la Reli (*TRL*) ili kuweka usawa wa tofauti kubwa ya mishahara na kutosababisha matabaka kwa wafanyakazi kwani maelewano mazuri kazini ndiyo msingi wa kuongeza tija.

(b) Shirika jipya litakaloundwa kuweka mipaka na vigingi (*beacons*) vinavyoonekana kwenye maeneo yake ili kuzuia uvamizi unaofanywa na wananchi kwa kutokutambua umiliki wa maeneo hayo. Ikumbukwe kuwa walenzi wa mali za Shirika la Reli ni wananchi kwa hiyo panapokuwa na mahusiano mabaya hujuma huweza kufanyika dhidi ya miundombinu.

(c) Serikali kuweka utaratibu mzuri kwa mwananchi kuweza kupata haki zake pindi kunapokuwepo na matatizo ya kufutwa kwa safari, kuchelewa kwa gari moshi pamoja na kuharibika ili kuondoa usumbufu uliokuwa unajitokeza mara kwa mara kwa wananchi pindi Shirika la Reli linapokuwa limepata dharura na/au kuchelewa kwa gari moshi pasipo kujali haki za abiria.

(d) Serikali kuweka utaratibu mzuri wa wazi na haki utakaotumika kuhamisha wafanyakazi kwenda kwenye shirika jipya au wengine kwenda ofisi nyingine za Serikali hivyo kupunguza au kuondoa malalamiko.

(e) Shirika lipya kuisaidia Serikali katika kufanya utafiti wa kupanua matawi (*spurs*) ya Reli ya Kati kutoka Bandari kavu ya Isaka, Shinyanga hadi Rusumo Mkoani Kagera hivyo

kuwezesha mradi wa kuchimba madini ya *Nickel* huko Kabanga kutekelezeka. Vile vile Serikali ichunguze uwezekano wa kuweka tawi la reli sambamba na bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Isaka ili kupanua uwekezaji katika viwanda katika ushoroba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa ubomoaji au uondolewaji wa wananchi waliomo kwenye maeneo ya Shirika la Reli uendele, isipokuwa wananchi waliomilikishwa maeneo yaliyokuwa ya Shirika la Reli kwa nia njema na kwa kufuata taratibu zote za kisheria wabainishwe na walipwe fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, sasa naomba kutambua Wajumbe wa Kamati hii walioshughulika na Muswada huu kwa namna moja au nyingine, tunawashukuru sana. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashillillah kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athumani Hussein, Makatibu wa Kamati Ndugu Hosiana John na Ndugu Richard Masuke pamoja na Washauri wa Sheria Ndugu Evelyne Shibandiko na Ndugu Mariam Mbaruku kwa kuihudumia Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba niwashukuru sana Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Mnyaa, Mbunge. Vilevile Katibu Mkuu Dkt. Leonard M. Chamuriho akisaidiana na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakati wote wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
MIUNDOBINU KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA RELI
TANZANIA YA MWAKA 2017 (*THE RAILWAYS ACT, 2017*) –
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, napenda kutumia fursa hii kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Reli Tanzania ya Mwaka 2017 (*The Railways Act, 2017*).
2. **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaanza kwa kutoa pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Rais na Serikali kwa hatua kubwa zilizochukuliwa katika kuimarisha Sekta ya Reli nchini. Muswada huu ni ishara tosha ya kazi kubwa ambayo imefanyika katika mfupi.
3. **Mheshimiwa Spika**, Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 7(1) (b) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, inazipa Kamati za Bunge za Kisekta ikiwemo Kamati ya Miundombinu, jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba iliyo chini ya Wizara inazozisimamia.
4. **Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umeletwa kwa hati ya dharula; na hivyo kuwa na siku chache za Kamati kuupitia na kuujadili. Tarehe 09 Septemba, 2017 Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa Mnyaa, (Mb) aliwasilisha mbele ya Kamati Muswada huu, ambapo pamoja na maelezo mengine, alijulisha Kamati manufaa mbalimbali yatakayotokana na kupitishwa kwa Sheria hii kwa maendeleo ya sekta ya reli nchini.
5. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na muda ambao Kamati imepokea Muswada huu ulikuwa mfupi kwa hivyo wadau mbalimbali walialikwa lakini hawakuweza kufika na kuleta maoni yao mbele ya Kamati. Kamati inawashukuru

Chama cha Wafanyakazi Reli Tanzania-TRAWU kwa kufika na kutoa maoni yao mbele ya Kamati.

2.0 HISTORIA FUPI RELI NCHINI TANZANIA

6. **Mheshimiwa Spika**, reli ilianza kujengwa na wakoloni Wakijerumani kuanzia Dar es Salaam kwenda Kigoma mwaka 1905-1914. Wakati huo Shirika la Reli Tanzania lilianzishwa likiitwa Reli ya Tanganyika; ambalo lilikuwa likisimamia reli ya kati kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma kwenye Ziwa Tanganyika. Wajerumani walipoondoka (1918) Tanganyika ilitawaliwa na Waingereza kama eneo la kudhaminiwa la Shirikisho la Mataifa (ambalo sasa hujulikana kama Umoja wa Mataifa na kupata Uhuru mwaka 1961). Katika kipindi hicho, Reli ya Tanganyika iliongezwa njia ya kando kutoka Tabora hadi Mwanza.

7. **Mheshimiwa Spika**, mwaka 1948, huduma zote mbili, yaani reli na bandari ziliunganishwa; na hivyo kuanzishwa kwa Shirika jipya la (*East Africa Railways & Harbors-EAR&H*) ambalo lilikuwa shirika jipya lililosimamia na kutekeleza kazi za reli, bandari za baharini; pamoja na huduma za meli kwenye maziwa makubwa yaani, Victoria (Nyanza), Tanganyika na Nyasa.

Shirika hilo jipya liliendelea kuongeza mtandao wa reli, kuboresha huduma ya meli, kwa kuleta meli mpya katika Ziwa Victoria, ambapo mwaka 1967 Jumuiya ya nchi tatu kubwa za Afrika Mashariki ilianzishwa. Hata hivyo, kutokana na changamoto mbalimbali Jumuiya hii ilivunjika mwaka 1977. Kuvunjika kwa Jumuiya hii kulisababisha Shirika la Reli la (*East Africa railways & harbor-EAR&H*) kuvunjwa.

8. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kuvunjika kwa umoja huu ndipo njia za reli, bandari na Meli ziligawanywa kati ya nchi tatu zilizokuwa za umoja huo. Shirika la Reli Tanzania lilianzishwa likiwa na matawi ya Dar es Salaam-Kigoma, Tabora-Mwanza na Kaliua- Mpanda. Kwa upande wa Kenya na Uganda zilianzishwa Shirika la Reli la Kenya na Shirika la Reli la Uganda.

2.1 Kuanzishwa kwa RAHCO na TRL

9. **Mheshimiwa Spika**, mwaka 2007, Shirika la Reli Tanzania lilivunjwa na lilianzishwa shirika lingine kwa ajili ya kumiliki miundombinu ya reli nchini (*Railways Holding Company-RAHCO*). Mwaka huo huo shughuli za uendeshaji wa usafiri wa reli ilihamishiwa kwa (*Tanzania Railways Limited-TRL*) na Kampuni ya RITES kutoka India iliyoingia ubia wa uendeshaji kwa makubaliano ya kuwa na hisa asilimia 49 kwa Tanzania na asilimia 51 kwa RITES.

10. **Mheshimiwa Spika**, moja kati ya madhumuni ya Serikali kubinafsisha Shirika la Reli Tanzania ilikuwa ni kuweka mazingira ya kuwa na Makampuni mengi ya usafirishaji kwa njia ya reli hivyo kurahisisha makampuni hayo kuweza kulipia huduma ya utumiaji wa njia na kubaki kushughulika na uendeshaji pekee. Hata hivyo, ubinafsishaji huo haukuleta mafanikio yaliyokuwa yanatarajiwa na kusababisha mwaka 2011, Serikali ya Tanzania kuvunja Mkataba wake na RITES na kurejesha umiliki na uendeshaji wa Shirika la Reli kwa asilimia 100.

11. **Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa ambayo imekuwa ikikabili uendeshaji wa reli pamoja na uchukuzi wa abiria na mizigo, ni kutokuwepo uwajibikaji wa pamoja kati ya haya mashirika mawili yaani RAHCO na TRL. Kwa mfano, panapotokea miundombinu ya reli imeharibika au kusombwa na maji, TRL imejikuta ikilazimika kugharamia matengenezo ya kipande cha reli husika ili iweze kuendelea kusafirisha abiria wake haraka iwezekanavyo na hivyo kupunguza usumbufu kwao, na pia kuepuka kuingia gharama zaidi.

12. **Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni, miongoni mwa malengo yaliyowekwa na Serikali kuhusu kuimarisha miundombinu ya reli nchini; ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge* ambapo Serikali imewekeza kiasi kikubwa cha Fedha. Kutokana na uwekezaji huo mkubwa imeonekana ni muhimu kuunda chombo madhubuti kwa ajili ya usimamizi wa miundombinu hii ambayo inaligharimu Taifa fedha nyingi.

13. **Mheshimiwa Spika**, Muswada huu wa Sheria ya Reli, 2017, unaanzisha Shirika jipya la Reli ambalo pamoja na mambo mengine litakuwa na jukumu la kusimamia, kuendeleza miundombinu ya Reli na kutoa huduma za usafiri wa Reli. Sheria hii itatumika Tanzania Bara pekee na haitatumika katika uendeshaji wa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia.

14. **Mheshimiwa Spika**, malengo ya Shirika hili yatakuwa ni kutoa huduma za usafiri wa reli, kujenga na kuendeleza miundombinu ya reli, kuhamasisha na kutunza miundombinu ya reli, kufanya matengenezo ya reli na kuhakikisha kunakuwa na ulinzi na usalama wa miundombinu ya reli pamoja na kuingia kwenye mikataba mbalimbali ili kulinda masharti ya huduma ya usafirishaji kwa njia ya reli. Mikataba hiyo inaweza kuwa baina ya Serikali na watu binafsi kwa ajili ya kukasimisha madaraka yake ya kuendeleza na kutunza miundombinu ya reli.

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

15. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia uchambuzi uliofanywa na Kamati; yafuatayo ni maoni na ushauri wake:-

I. **Kifungu cha 20 (1)** kinachoongelea Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji. **Kifungu kidogo cha (5)** kimeongelea jukumu la Mkurugenzi Mtendaji. Kamati inaona kwamba kifungu hiki kihamie kwenye **kifungu cha 21** kinachohusu Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji.

II. **Kifungu cha 21** kinachoeleza kazi na Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji, kitamke bayana kuwa Mamlaka yake na kazi zake zinatekelezwa chini ya uongozi na udhibiti wa Bodi kama ilivyoainishwa katika **kifungu 20 (5)**.

III. **Kifungu cha 21 (1) (b)** kinachoongelea jukumu la Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika kuandaa na kutekeleza Kanuni za Maadili kwa Watumishi. Muswada huu haujabainisha ni nani anayetakiwa kupitisha Kanuni hizo za maadili kwa Watumishi baada ya kuwa zimeandaliwa na

Mkurugenzi Mtendaji. Kamati inashauri wajibu huo wa kupitisha Kanuni uwe ni jukumu la Bodi.

IV. Kifungu cha 21 (1) (k) kinaeleza kuhusu kuanzisha na kuendesha reli. Kamati inaona kuwa jukumu hili silo la Mkurugenzi Mtendaji badala yake jukumu hilo ni la Shirika hivyo ni ushauri wa Kamati jambo hili kupelekwa kwenye majukumu ya Shirika.

V. Kifungu cha 23(7) kinampa Mamlaka Mkurugenzi Mtendaji kutokuzingatia utaratibu wa kiushindani wakati wa kuteuwa watumishi, washauri wa kitaalam au wataalam endapo kuna uharaka wa uteuzi au mazingira mengine maalum. Kamati inashauri kifungu huki kifanyiwe mabadiliko, hasa kwa upande wa uteuzi wa washauri wa kitaalam ambapo mchakato wake unatakiwa kupitia Sheria ya Manunuzi ya Umma. Hivyo mamlaka yake yazingatie Sheria ya Manunuzi ya Umma ambayo kwenye **kifungu cha 65** kinatoa utaratibu huo.

VI. Kifungu cha 26 kinaongelea utafiti na ukaguzi. Afisa aliyeidhinishwa na Shirika anaweza kuingia kwenye nyumba au eneo la mwananchi yeyote na kufanya ukaguzi na utafiti kwa lengo la kutathmini kama eneo hilo linafaa kwa ajili ya ujenzi wa reli. Pamoja na kwamba anatakiwa kupata kibali cha mwenye nyumba au eneo husika, Kamati inashauri wakati wa ukaguzi huo, ikiwa eneo hilo ni mali ya Shirika la Reli, ni muhimu kuwepo Afisa wa Serikali ya Mtaa kwa ajili ya kujua kinachoendelea kwa wananchi wa mtaa wake. Ikiwa eneo hilo ni jipya, Kamati inashauri Waziri aweke Kanuni za kufuata katika utekelezaji wa jukumu hilo ili kuzingatia matakwa ya Sheria nyingine husika hususan Sheria ya Ardh.

VII. Kifungu cha 60 kinaongelea uanzishwaji wa Mamlaka ya Mdhibili. Kifungu hiki hakijaeleza kama mdhibiti huyo ni mtu binafsi au ni Kampuni. Hivyo, Kamati inashauri kama ni mtu binafsi kifungu hiki kibaki kama kilivyo lakini ikiwa ni Kampuni kifungu cha 60(3) kitumie neno "its" na sio "his". Aidha, Kamati inashauri kutolewa tafsiri ya neno "*Regulator*"

ili kuleta maana ya anayekusudiwa kutajwa katika Sheria hii.

16. **Mheshimiwa Spika**, mambo mengine ambayo Kamati inashauri ni kama yafuatayo;-

a) Wakati Sheria hii inapitishwa Serikali inashauriwa kuangalia kwa umakini suala la mishahara kwa wafanyakazi kwani wafanyakazi wa RAHCO walikuwa na mishahara mikubwa ukilinganishwa na wafanyakazi wa lililokuwa Shirika la Reli Limited (TRL) ili kuweka usawa wa tofauti kubwa ya mishahara na kutosababisha matabaka kwa wafanyakazi kwani maelewano mazuri kazini ndiyo msingi wa kuongeza tija.

b) Shirika jipya litakaloundwa kuweka mipaka na vigingi (*beacons*) vinavyoonekana kwenye maeneo yake ili kuzuia uvamizi unaofanywa na wananchi kwa kutokutambua umiliki wa maeneo hayo. Ikumbukwe kuwa walenzi wa mali za Shirika la Reli ni wananchi kwa hiyo panapokuwa na mahusiano mabaya hujuma huweza kufanyika dhidi ya miundombinu.

c) Serikali kuweka utaratibu mzuri kwa mwananchi kuweza kupata haki zake pindi kunapokuwepo na matatizo ya kufutwa kwa safari, kuchelewa kwa gari moshi pamoja na kuharibika ili kuondoa usumbufu uliokuwa unajitokeza mara kwa mara kwa wananchi . Shirika la Reli limekuwa likifuta safari au kuchelewa kwa gari moshi pasipokujali haki za abiria.

d) Serikali kuweka utaratibu mzuri wa wazi na haki utakaotumika kuhamisha wafanyakazi kwenda kwenye shirika jipya au wengine kwenda ofisi nyingine za Serikali hivyo kupunguza au kuondoa malalamiko.

e) Shirika lipya kuisaidia Serikali katika kufanya utafiti wa kupanua matawi (*spurs*) ya reli ya kati kutoka Bandari kavu ya Isaka (Shinyanga) hadi Rusumo Mkoani Kagera, hivyo kuwezesha mradi wa kuchimba madini ya *Nickel* huko

Kabanga kutekelezeka. Vilevile, Serikali ichunguze uwezekano wa kuweka tawi la reli sambamba na bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Isaka ili kupanua uwekezaji katika viwanda katika ushoroba huo.

17. **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kuwa ubomoaji au uondolewaji wa wananchi waliomo kwenye maeneo ya Shirika la Reli uendeleo isipokuwa, wananchi waliomilikishwa maeneo yaliyokuwa ya Shirika la Reli kwa nia njema na kwa kufuata taratibu zote za kisheria wabainishwe na walipwe fidia.

4. 0 HITIMISHO

18. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, sasa naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia Muswada huu kama ifuatavyo:-

- 1.Mhe. Prof Norman A. Sigalla King, Mb – Mwenyekiti
- 2.Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb - M/Mwenyekiti
- 3.Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb - Mjumbe
- 4.Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb ..
- 5.Mhe. James Francis Mbatia, Mb ..
- 6.Mhe. Mansoor Shanif Hirani, Mb ..
- 7.Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb ..
- 8.Mhe. Saul Henry Amon, Mb ..
- 9.Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb ..
- 10.Mhe. Quambalo Willy Qulwi, Mb ..
- 11.Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb ..
- 12.Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb ..
- 13.Mhe. Dkt.Chuachua Mohamed Rashid, Mb ..
- 14.Mhe. Mery Deo Muro, Mb ..
- 15.Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb ..
- 16.Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb ..
- 17.Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb ..
- 18.Mhe. Dua William Nkurua, Mb ..
- 19.Mhe. Musa Rashid Ntimizi, Mb ..
- 20.Mhe. Lathifah Hassan Chande, Mb ..
- 21.Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb ..

naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Reli ya mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu Namba 6 wa mwaka 2017 ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali tarehe 3 Septemba, 2017 na unaletwa Bungeni kwa Hati ya Dharura licha ya maangalizo mengi yaliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya madhara ya kuleta miswada ya sheria inayohusu mambo nyeti kwa Hati za Dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono masuala yote yanayohusu ujenzi, usimamizi na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ikiwemo reli, lakini tunataka masuala hayo yachambuliwe na kusimamiwa kwa umakini yasije yakaliingiza taifa katika hasara ambazo zingeweza kuepukwa kwa kuwa na muda wa kutosha ili kujiridhisha nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kutunga sheria na baada ya miezi miwili kuifanyia marekebisho kinatoa taswira mbaya kwamba pengine Bunge halikuwa makini vya kutosha wakati wa kupitisha sheria hiyo. Hata hivyo ukweli ni kwamba kinachosababisha mambo kama hayo kutokea ni matumizi mabaya ya hati za dharura katika kupitisha sheria kuhusu mambo ambayo kwa asili yake si ya dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unaanzisha Shirika jipya la Reli (*TRC*) pamoja na Bodi yake. Shirika hili linaweza kuonekana jipya lakini kihistoria Shirika la Reli si jipya kwa sababu Shirika hilo liliwahi kuwepo nchini kwa mujibu wa Sheria ya Shirika la Reli ya mwaka 1977 (*The Tanzania Railways Corporation Act, 1977*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kilicholeta mabadiliko ambayo kimsingi yamechochea kuletwa kwa Muswada huu ni Sheria ya Reli (*The Railway Act*) ya mwaka 2002. Aidha, Sheria ya mwaka 2002 ilisababisha kuanzishwa kwa Kampuni ya Reli (*TRL*) ambayo iliendeshwa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi. Pia sheria hiyo hiyo ilianzisha *Rail Assets*

Holding Company Limited (RAHCO) ambayo ilikuwa na jukumu la kusimamia mali zote na miundombinu ya Reli ambayo ilikuwa inatumiwa na *TRL* kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ieleweke kuwa mwito wa kuunganisha Mashirika haya ya *TRL* na *RAHCO* ni wa muda mrefu ambapo Wabunge mbalimbali kwa mara kadhaa wamekuwa wakiishauri Serikali kuunganisha Mashirika haya ili kuleta ufanisi na kuboresha sekta uchukuzi kupitia reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizokuwa zinakabili mashirika haya zilisababisha kushindwa kutoa huduma ya uchukuzi wa mizigo na abiria na hivyo kusababisha matumizi makubwa kwenye barabara zetu, jambo ambalo lilisababisha barabara hizo kuharibika. Pamoja na mwito kutoka kwa Wabunge na wadau mbalimbali kufanya hivyo kwa miaka mingi Serikali haikuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kurudisha tena Shirika la Reli ni kubwa na ilichelewa kuletwa katika Bunge lako Tukufu. Wakati wa mjadala wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 mmoja wa Wabunge alisema yafuatayo, naomba kunukuu:-

“Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongee suala la pili kuhusu TRL na RAHCO. Mpaka mwaka 2002, Shirika la Reli (TRC) lilikuwa na uwezo wa kufanya kazi yake vizuri. Mpaka mwaka 2002 Shirika la TRC lilikuwa na vichwa 68, mpaka mwaka 2002 Shirika la TRC lilikuwa na mabehewa 1,500, mpaka mwaka 2002 Shirika la TRC lilikuwa na uwezo wa kusafirisha tani 1,500,000; kwa hiyo, mgawanyiko kati ya TRC na RAHCO, ndio umeleta shida katika Shirika la Reli.”

“Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana ni makosa ya Serikali kuingia kwenye mkataba ambao haukuwa mzuri, kati yake na kampuni ya wenzetu wa India, ndio uliosababisha hali hii iliyojitokeza. Sasa rai yangu kwa Serikali, ni lazima hapa leo tutoke na azimio katika Bunge lako Tukufu la kuunganisha

RAHCO na TRL, ni lazima tutoke na tamko hilo, vinginevyo maeneo mengi yaliyokuwa yakifanya vizuri kipindi cha TRC yatakuwa ni magofu."

"Mheshimiwa Mwenyekiti, TRC ilikuwa na karakana nzuri, ilikuwa inahudumia reli yake vizuri, lakini leo maeneo yote hayo hayafanyi vizuri kwa sababu ya TRL kunyimwa nguvu na Shirika la RAHCO ambalo ukiangalia kwa nini lipo hupati majibu yaliyokamilika. TRL haina uwezo wa kukopa kwa sababu haina dhamana, lakini TRL ndiyo inayoangalia mabehewa yake, vichwa vyake na reli kwa wakati mwingine. Naomba sana, muunganishe TRL na RAHCO." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa Shirika la Reli linarudishwa kwa kutumia Muswada huu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha inatatua changamoto zilizopo na kuhakikisha kuwa wahusika wote waliosababisha sekta ya Reli kufika ilipo leo kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikishwaji wa wadau, Kambi Rasmi ya Upinzani imestushwa na kitendo cha wadau kupewa wito wa muda mfupi kuja kuwasilisha maoni yao katika muswada huu. Ni vyema tukaendelea na utaratibu wetu wa siku zote ambao ni shirikishi ili Kamati na Bunge lako Tukufu lipate kwa undani maoni ya wadau wanaoguswa na mabadiliko makubwa yanayopendekezwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si tu kwamba maoni yao yatasikilizwa na Wabunge na hivyo kufanyiwa kazi bali pia unawapa uhalali wadau hao kuisimamia na kuitekeleza Sheria kikamilifu pindi itakapoanza kutekelezwa baada ya kusainiwa na Rais na Kanuni kutungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa ujumla wa Muswada; Sakata la Bomoa bomoa la nyumba za wananchi. Hivi karibuni Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Katavi, Tabora, Kigoma, Kilimanjaro na mikoa mingine nchini imekumbwa

na sakata la bomoa bomoa ambalo linadaiwa kuendeshwa na *RAHCO* kwa madai kuwa wananchi hao wamejenga karibu au kwenye maeneo ya reli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke kuwa wananchi wengine wa maeneo ya Katavi, Tabora na Kigoma wametoa taarifa kuwa wameishi katika maeneo hayo kabla hata ya uhuru wa nchi yetu. Aidha, Shirika la Umeme pamoja na Mashirika/Jumuiya zinazotoa huduma ya maji yametoa huduma katika maeneo ambayo *RAHCO* wanadai ni maeneo ya Reli. Vile vile Serikali imejenga miundombinu ya shule, afya na barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wananchi wamedai kuwa wanazo leseni za makazi au hati za kumiliki maeneo yao zilizotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa au kutoka Wizara ya Ardhi lakini *RAHCO* haijazingatia mambo yote hayo na kuamua kuendelea kutoa noti za kubomoa makazi ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ieleweke kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Shirika la Reli ya mwaka 1977 vifungu vya 16 hadi 23 vilikuwa vinatoa mamlaka kwa shirika kuingia kwenye ardhi yoyote kwa ajili ya shughuli mbalimbali za miundombinu ya reli isipokuwa sheria ilitoa nafasi kwa Waziri anayehusika na ardhi kushauriana na shirika kwa ajili ya kuboresha ufanisi wa masuala hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Reli ya mwaka 2002 kifungu cha 38 kinatengua utekelezaji wa Sheria ya Ardhi, Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 pamoja na Sheria ya Mipango Miji. Aidha, muswada huu katika kifungu cha 28 kinarudia masharti ya kifungu cha 38 cha sheria ya mwaka 2002. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa uwepo wa kifungu cha 28 katika muswada huu ambacho kinarudia kifungu cha 38 cha sheria ya mwaka 2002 inayofutwa kina lengo la kufanya watakaoguswa na miradi ya reli kutolipwa fidia hata kama miundombinu ya

reli itatekelezwa katika ardhi ambayo imeendelezwa na wananchi bila ya kulipwa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikoa ambayo nimeitaja katika hotuba hii hasa Mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi ni takribani nyumba na makazi ya wananchi 3,244 zitabomolewa. Hili si jambo dogo na la kupuuza hata kidogo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia upya uamuzi huu ambao hauendi kuwa baraka kwa wananchi bali utaleta kilio. Ikumbukwe kuwa baadhi ya wananchi kama nilivyoeleza wamekuwepo katika maeneo hayo kwa vizazi sasa lakini wanashangaa kuona kuwa sehemu ya bomoabomoa ambayo inafanya kwa usimamizi wa *RAHCO* inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke pia kuwa wananchi walio wengi wamekiri na wamekubali kubomoa makazi yao ambayo yako ndani ya mita 30 kwa mujibu wa hifadhi ya ardhi ya reli, lakini cha kushangaza maeneo mengi ya Mikoa niliyoitaja hifadhi ya eneo la reli wananchi wanalalamika kuwa imeongezwa zaidi kuliko inavyotakiwa kuwa kwa mujibu wa Sheria ya mita 30 kwa 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuletwa kwa sheria hii kwa hati ya dharura na mkanganyiko mkubwa wa bomobomoa inayoendelea, tunahitaji Serikali itupatie maelezo ya kina na ikiwezekana iagize zoezi hilo lisitishwe.

Aidha, wananchi walio wengi kama nilivyoeleza wameishi kwa muda mrefu kwenye maeneo hayo na hata sheria ya ukomo wa muda inatoa ruhusa kwa mtu ambaye amekuwa katika ardhi kwa muda wa miaka 12 bila usumbufu wa aina yoyote kutoka kwa anayedai kumiliki, basi atakuwa ndiye mmiliki halali wa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya kushangaza kifungu cha 26 cha muswada huu kinatoa mamlaka kwa afisa aliyeidhinishwa na shirika kuingia kwenye nyumba au eneo lolote kwa ajili ya kufanya utafiti na ukaguzi kama eneo husika litafaa kujungwa miundombinu ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi Upinzani inaona kuwa kifungu hiki cha 26 kitakuwa na madhara makubwa sana kwa ardhi ya wananchi. Pamoja na kifungu hicho kumtaka afisa wa Shirika la Reli kuomba ruhusa ya mwenye ardhi, ni vema wawakilishi wa wananchi (Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vitongoji, Vijiji au Madiwani) wakapewa taarifa ili kuhakikisha wawakilishi hao wanakuwa na taarifa ya uwepo wa maafisa wa reli katika mitaa husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza utaratibu mzima wa utwaaji wa ardhi kwa ajili ya shughuli za reli usjikite tu kuomba ruhusa ya mwenye eneo bali inatakiwa ifuate utaratibu wa utwaaji wa ardhi kwa mujibu Sheria za Ardhi pamoja na kuwa kifungu cha 28 kinazuia matumizi ya sheria husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Reli. kifungu cha 21 kinaainisha kwa kina majukumu na mamlaka ya Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Reli, ikiwa ni pamoja na kutengeneza Kanuni za Maadili ya Shirika kwa mujibu wa kifungu cha 21(1)(b) cha muswada. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa huu ni utaratibu mpya kabisa kumpatia Mkurugenzi Mtendaji mamlaka ya kutengeneza Kanuni za Maadili ya Shirika la Reli.

Hata katika utaratibu ambao Bunge hili limekuwa likipitisha mamlaka ya kutunga kanuni hayapo kwa Mkurugenzi Mtendaji bali yapo kwa Waziri mwenye dhamana na sekta husika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhamisha majukumu haya kwa Waziri isipokuwa Waziri apokee maoni kutoka kwa Bodi ya Shirika kuliko kuyaacha kwa Mkurugenzi Mtendaji peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, muswada huu unampa mamlaka mengine Mkurugenzi Mtendaji ambayo kimsingi yanaingiliana na mamlaka ya Shirika la Reli kwa ujumla. Kwa mfano, kifungu cha 21(1)(k) kinampa mamlaka Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Reli ya kuanzisha na kuendesha reli. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri jukumu hili liende kwenye Bodi.

Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kifungu cha 23(7) cha Muswada kifutwe kwa sababu kifungu hiki kitatoa mwanya ambao unaweza kusababisha kushindwa kuzingatiwa kwa utawala bora na hata kusababisha hasara kwa Shirika. Hii inatokana na mapendekezo ya Muswada huu kutoa ruhusa na kumpa mamlaka Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Reli kutozingatia utaratibu wa kiutendaji wakati wa kuteua watendaji na wataalam endapo kutakuwa na dharura. Hii itatoa mwanya wa rushwa. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuitaka Serikali kuhakikisha kuwa inafuta kifungu hiki na kuhakikisha kuwa katika wakati wote Sheria ya Manunuzi ya Umma inazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu abiria kurudishiwa nauli baada ya kuchelewa kwa gari moshi/treni; kifungu cha 38(2) cha Muswada kikibaki kama kilivyo kitaleta athari hasa kwa sekta binafsi. leleweke kuwa watu hawasafiri kwa matembezi au kutembelea ndugu na jamaa peke yake. Dunia ya leo ni ya kiushindani na ni ya kibiashara, kitendo cha kuchelewesha kurudisha nauli kwa saa 24 baada ya gari moshi/treni kuchelewesha safari kitalirudisha nyuma shirika na kushindwa kuingia kwenye ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza muda wa kuwarudishia nauli abiria baada ya treni kuchelewa uwe masaa sita badala ya masaa 24 ili kuwafanya watendaji wa shirika kuwajibika ipasavyo. Hata hivyo, kama Serikali itaona ni vema muda ukabaki ule ule basi angalau kuwe na jukumu la shirika kuwapatia abiria ambao wamechelewesha chakula na malazi ili kuwapunguzia usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, faini kwa abiria ambao hawana tiketi; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa na matakwa ya kifungu cha 47(2) kumtoza abiria asilimia 100 ya nauli pale anapopanda bila kuwa na tiketi. Ni ukweli usiopingika kuwa abiria wengi wanatoka maeneo ya mbali na njia ya reli na hivyo wanaweza kujikuta hawajakata tiketi ya safari au mara kadhaa ofisi za kutolea tiketi huwa zinakuwa na foleni na pengine abiria ana

udharura. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri angalau abiria anayepanda gari moshi/treni bila kuwa tiketi atozwe angalau asilimia 50 zaidi ya nauli aliyotakiwa kutozwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; kama nilivyosema hapo awali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingi masuala yanayohusu ujenzi na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ikiwemo reli. Hata hivyo, masuala hayo hayana budi kufanywa kwa umakini ili kutoibua migogoro au hali ya kutoelewana kati ya wananchi na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba masuala yote yanayolalamikiwa na wananchi hususan ubomoaji wa nyumba zao na utwaaji wa maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa reli yanashughulikiwa ili Sheria hii mpya ya reli inayotungwa iweze kukubalika kwa wananchi na hivyo kuweza kutekelezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko ya wananchi yasiposhughulikiwa ipasavyo na wananchi wakapata haki yao Sheria hii itashindwa kufanya kazi, na Bunge litakuwa limepoteza muda wake kutunga sheria ambayo itashindwa kutekelezwa vizuri na wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha, ahsante. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO, MHESHIMIWA JAMES FRANCIS MBATIA
(MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI YA
UPINZANI KUHUSU MUSWADA WA RELI WA MWAKA 2017 -
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. UTANGULIZI NA MASUALA YA JUMLA KUHUSU MUSWADA

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la 2016, naomba kuwasilisha

maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Reli ya mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu namba 06 wa mwaka 2017 ulichapishwa kwenye gazeti la Serikali tarehe 03 Septemba, 2017 na unaletwa Bungeni kwa hati ya dharura licha ya maangalizo mengi yaliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya madhara ya kuleta miswada ya sheria inayohusu mambo nyeti kwa hati za dharura.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono masuala yote yanayohusu ujenzi, usimamizi na uboreshaji wa miundo mbinu mbalimbali ikiwemo Reli; lakini tunataka masuala hayo yachambuliwe na kusimamiwa kwa umakini yasije yakaliingiza taifa katika hasara ambazo zingeweza kuepukwa kwa kuwa na muda wa kutosha ili kujiridhisha nayo. Kitendo cha kutunga sheria na baada ya miezi miwili kuifanyia marekebisho kinatoa taswira mbaya kwamba pengine Bunge halikuwa makini vya kutosha wakati wa kupitisha sheria hiyo, lakini ukweli ni kwamba kinachopelekea mambo kama hayo kutokea ni matumizi mabaya ya hati ya dharura katika kupitisha Sheria kuhusu mambo ambayo kwa asili yake si ya dharura.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unaanzisha Shirika "jipya" la Reli (TRC) pamoja na Bodi yake. Shirika hili linaweza kuonekana jipya lakini kihistoria Shirika la Reli si jipya kwa sababu Shirika hilo liliwahi kuwepo nchini kwa mujibu wa Sheria ya Shirika la Reli ya mwaka 1977 (The Tanzania Railways Corporation Act, 1977).

Mheshimiwa Spika, kilicholeta mabadiliko ambayo kimsingi yamechochea kuletwa kwa Muswada huu ni Sheria ya Reli (The Railway Act) ya mwaka 2002. Aidha, Sheria ya mwaka 2002 ilipelekea kuanzishwa kwa Kampuni ya Reli (TRL) ambayo iliendeshwa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi. Pia Sheria hiyo iliyanzisha Reli Assets Holding Company Limited (RAHCO) ambayo ilikuwa na jukumu la kusimamia mali zote na miundombinu ya Reli ambayo ilikuwa inatumiwa na TRL kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, naomba ieleweke kuwa mwito wa kuunganisha Mashirika haya ya TRL na RAHCO ni wa muda mrefu ambapo Wabunge mbalimbali kwa mara kadhaa wamekuwa wakiishauri Serikali kuunganisha Mashirika haya ili kuleta ufanisi na kuboresha sekta uchukuzi kupitia reli.

Mheshimiwa Spika, Changamoto zilizokuwa zinakabili mashirika haya zilipelekea kushindwa kutoa huduma ya uchukuzi wa mizigo na abiria na hivyo kupelekea matumizi makubwa kwenye barabara zetu jambo ambalo lilipeleka barabara hizo kuharibika. Pamoja na mwito kutoka kwa Wabunge na wadau mbalimbali kufanya hivyo kwa miaka mingi serikali haikuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kurudisha tena Shirika la reli ni kubwa na ilichelewa kuletwa katika Bunge lako tukufu. Wakati wa Mjadala wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 mmoja wa wabunge alisema yafuatayo; naomba kunukuu,

“Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongee suala la pili kuhusu TRL na RAHCO. Mpaka mwaka 2002, Shirika la Reli (TRC) lilikuwa na uwezo wa kufanya kazi yake vizuri. Mpaka mwaka 2002 Shirika la TRC lilikuwa na vichwa 68, mpaka mwaka 2002 Shirika la TRC lilikuwa na mabehewa 1,500 mpaka mwaka 2002 Shirika la TRC lilikuwa na uwezo wa kusafirisha tani 1,500,000; kwa hiyo, mgawanyiko kati ya TRC na RAHCO, ndiyo umeleta shida katika Shirika la Reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana ni makosa ya Serikali kuingia kwenye mkataba ambao haukuwa mzuri, kati yake na kampuni ya wenzetu wa India, ndiyo uliosababisha hali hii iliyojitokeza. Sasa rai yangu kwa Serikali, ni lazima hapa leo tutoke na azimio katika Bunge lako Tukufu la kuunganisha RAHCO na TRL, ni lazima tutoke na tamko hilo, vinginevyo maeneo mengi yaliyokuwa yakifanya vizuri kipindi cha TRC yatakuwa ni magofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TRC ilikuwa na karakana nzuri, ilikuwa inahudumia reli yake vizuri, lakini leo maeneo yote hayo hayafanyi vizuri kwa sababu ya

TRL kunyimwa nguvu na Shirika la RAHCO ambalo ukiangalia kwa nini lipo hupati majibu yaliyokamilika. TRL haina uwezo wa kukopa, kwa sababu haina dhamana, lakini TRL ndiyo inayoangalia mabehewa yake, vichwa vyake na reli kwa wakati mwingine, naomba sana, muunganishe TRL na RAHCO”.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa Shirika la Reli linarudishwa kwa kutumia Muswada huu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha inatatua changamoto zilizopo na kuhakikisha kuwa wahusika wote waliosababisha sekta ya Reli kufika ilipo leo kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria.

1.1. Ushirikishwaji wa Wadau

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imestushwa na kitendo cha wadau kupewa wito wa muda mfupi kuja kuwasilisha maoni yao katika muswada huu. Ni vema tukaendelea na utaratibu wetu wa siku zote ambao ni shirikishi ili Kamati na Bunge lako tukufu lipate kwa undani maoni ya wadau wanaoguswa na mabadiliko makubwa yanayopendekezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, sio tu kwamba maoni yao yatasikilizwa na Wabunge na hivyo kufanyiwa kazi bali pia unawapa uhalali wadau hao kuisimamia na kuitekeleza Sheria kikamilifu pindi itakapoanza kutekelezwa baada ya kusainiwa na Rais na Kanuni kutungwa.

2. UCHAMBUZI WA JUMLA WA MUSWADA

2.1 Sakata la Bomoabomoa la Nyumba za Wananchi

Mheshimiwa Spika, Hivi karibuni Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Katavi, Tabora, Kigoma, Kilimanjaro na Mikoa mingine nchini imekumbwa na sakata la bomoabomoa ambalo linadaiwa kuendeshwa na RAHCO kwa madai kuwa wananchi hao wamejenga karibu au kwenye maeneo ya reli.

Mheshimiwa Spika, ieleweke kuwa wananchi wengine wa maeneo ya Katavi, Tabora na Kigoma wametoa taarifa kuwa wameishi katika maeneo hayo kabla hata ya uhuru wa nchi yetu. Aidha Shirika la Umeme pamoja na Mashirika/Jumuiya zinazotoa huduma ya maji yametoa huduma katika maeneo ambayo RAHCO wanadai ni maeneo ya Reli. Vile vile Serikali imejenga miundombinu ya shule, afya na barabara.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wananchi wamedai kuwa wanazo leseni za makazi au hati za kumiliki maeneo yao zilizotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa au kutoka Wizara ya Ardhi lakini RAHCO haijazingatia mambo yote na kuamua kuendelea kutoa noti za kubomoa makazi ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba ieleweke kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Shirika la Reli ya mwaka 1977 vifungu vya 16 hadi 23 vilikuwa vinatoa mamlaka kwa Shirika kuingia kwenye ardhi yoyote kwa ajili ya shughuli mbalimbali za miundombinu ya Reli isipokuwa Sheria ilitoa nafasi kwa Waziri anayehusika na Ardhi kushauriana na Shirika kwa ajili ya kuboresha ufanisi wa masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Reli ya mwaka 2002 kifungu cha 38 kinatengua utekelezaji wa Sheria ya Ardhi, Sheria ya Ardhi ya Vijiji za mwaka 1999 pamoja na Sheria ya Mipango Miji. Aidha Muswada huu katika kifungu cha 28 kinarudia masharti ya kifungu cha 38 cha Sheria ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa uwepo kifungu cha 28 katika Muswada huu ambacho kinarudia kifungu cha 38 cha Sheria ya mwaka 2002 inayofutwa, kina lengo la kufanya watakaoguswa na miradi ya reli kutolipwa fidia hata kama miundombinu ya reli itatekelezwa katika ardhi ambayo imeendelezwa na wananchi bila ya kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, katika Mikoa ambayo nimeitaja katika hotuba hii hasa Mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi ni takribani nyumba na makazi ya wananchi 3,244

zitabomolewa. Hili sio jambo dogo na sio la kupuuza hata kidogo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia upya uamuzi huu ambao hauendi kuwa Baraka kwa wananchi bali utaleta kilio. Ikumbukwe kuwa baadhi ya wananchi kama nilivyoeleza wamekuwepo katika maeneo hayo kwa vizazi sasa lakini wanashangaa kuwa sehemu ya bomoabomoa ambayo inafanya kwa usimamizi wa RAHCO.

Mheshimiwa Spika, ieleweke pia kuwa wananchi walio wengi wamekiri na wamekubali kubomoa makazi yao ambayo yako ndani ya mita 30 kwa mujibu wa hifadhi ya ardhi ya reli, lakini cha kushangaza maeneo mengi ya Mikoa niliyoitaja hifadhi ya eneo la reli wananchi wanalalamika kuwa imeongezwa zaidi kuliko inavyotakiwa kuwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kuletwa kwa Sheria hii kwa hati ya dharura na mkanganyiko mkubwa wa bomobomoa inayoendelea, tunahitaji Serikali itupatie maelezo ya kina na ikiwezekana iagize zoezi hilo lisitishwe. Aidha, wananchi walio wengi kama nilivyoeleza wameishi kwa muda mrefu kwenye maeneo hayo na hata Sheria ya ukomo wa muda inatoa ruhusa kwa mtu ambaye amekuwa katika ardhi kwa muda wa miaka 12 bila usumbufu wa aina yoyote kutoka kwa anayedai kumiliki, basi atakuwa ndiyo mmiliki halali wa eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kushangaza kifungu cha 26 cha Muswada huu kinatoa mamlaka kwa Afisa aliyeidhinishwa na Shirika kuingia kwenye nyumba au eneo lolote kwa ajili ya kufanya utafiti na ukaguzi kama eneo husika litafaa kujengwa miundombinu ya Reli.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi Upinzani inaona kuwa kifungu hiki cha 26 kitakuwa na madhara makubwa sana kwenye ardhi ya wananchi pamoja na kifungu hicho kumtaka Afisa wa Shirika la reli kuomba ruhusa ya mwenye ardhi, ni vema wawakilishi wa wananchi (Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vitongoji, Vijiji au Madiwani) wakapewa

taarifa ili kuhakikisha wawakilishi hao wanakuwa na taarifa ya uwepo wa Maafisa wa Reli katika Mitaa husika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza utaratibu mzima wa utwaaji wa ardhi kwa ajili ya shughuli za Reli usijikite tu kuomba ruhusa ya mwenye eneo, bali inatakiwa ifuate utaratibu wa utwaaji wa ardhi kwa mujibu Sheria za Ardhi pamoja na kuwa kifungu cha 28 kinazuia matumizi ya Sheria husika.

2.2 Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Reli

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 21 kinaainisha kwa kina majukumu na mamlaka ya Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Reli ikiwa ni pamoja na kutengeneza Kanuni za Maadili ya Shirika kwa mujibu wa kifungu cha 21 (1)(b) cha Muswada. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa huu ni utaratibu mpya kabisa kumpatia Mkurugenzi Mtendaji mamlaka ya kutengeneza Kanuni za Maadili ya Shirika la Reli.

Mheshimiwa Spika, hata katika utaratibu ambao Bunge hili limekuwa likipitisha, mamlaka ya kutunga Kanuni hayapo kwa Mkurugenzi Mtendaji bali yapo kwa Waziri mwenye dhamana na sekta husika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhamisha majukumu haya kwa Waziri isipokuwa Waziri apokee maoni kutoka kwa Bodi ya Shirika kuliko kuyaacha kwa Mkurugenzi Mtendaji peke yake.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unampa mamlaka mengine Mkurugenzi Mtendaji ambayo kimsingi yanaingiliana na mamlaka ya Shirika la Reli kwa ujumla. Kwa mfano kifungu cha 21 (1)(k) kinampa mamlaka Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Reli ya kuanzisha na kuendesha reli. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri jukumu hili liende kwenye Bodi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kifungu cha 23(7) cha Muswada kifutwe kwa sababu kifungu hiki kitatoa mwanya ambao unaweza kusababisha kushindwa kuzingatiwa kwa utawala bora na hata kusababisha hasara kwa Shirika. Hii inatokana na

mapendekezo ya Muswada huu kutoa ruhusa na kumpa mamlaka Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Reli kutozingatia utaratibu wa kiutendaji wakati wa kuteua watendaji na wataalam endapo kutakuwa na dharura. Hii itatoa mwanya wa rushwa na ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuitaka serikali kuhakikisha kuwa inafuta kifungu hiki na kuhakikisha kuwa katika wakati wote Sheria ya Manunuzi ya Umma inazingatiwa.

2.3 Kuhusu Abiria Kurudishiwa Nauli Baada ya Kuchelewa kwa Gari Moshi/Treni

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 38(2) cha Muswada kikibaki kama kilivyo kitaleta athari hasa kwa sekta binafsi. Ieleweke kuwa watu hawasafiri kwa matembezi au kutembelea ndugu na jamaa peke yake. Dunia ya leo ni ya kiushindani na ni ya kibiashara. Kitendo cha kuchelewesha kurudisha nauli kwa masaa 24 baada ya Gari Moshi/Treni kuchelewesha safari kitalirudisha nyuma Shirika na kushindwa kuingia kwenye ushindani.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza muda wa kuwarudishia nauli abiria baada ya Treni kuchelewa uwe masaa sita badala ya masaa 24 ili kufanywa watendaji wa Shirika kuwajibika ipasavyo. Hata hivyo, kama Serikali itaona ni vema muda ukabaki uleule basi angalau kuwe na jukumu la shirika kuwapatia abiria ambao wamecheleweshwa chakula na malazi ili kuwapunguzia usumbufu.

2.4 Faini kwa Abiria ambao hawana Tiketi

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa na matakwa ya kifungu cha 47(2) kumtoza abiria asilimia 100 ya nauli pale anapopanda bila kuwa na tiketi. Ni ukweli usiopingika kuwa abiria wengi wanatoka maeneo ya mbali na njia ya Reli na hivyo wanaweza kujikuta hawajakata tiketi ya safari au mara kadhaa ofisi za kutolea tiketi huwa zinakuwa na foleni na pengine abiria ana udharura. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri angalau abiria

anayepanda Gari Moshi/Treni bila kuwa tiketi atozwe angalau asilimia 50 zaidi ya nauli aliyotakiwa kutozwa.

3. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingi masuala yanayohusu ujenzi na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ikiwemo reli. Hata hivyo, masuala hayo hayana budi kufanywa kwa umakini ili kutoibua migogoro au hali ya kutoelewana kati ya wananchi na Serikali. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba masuala yote yanayolalamikiwa na wananchi hususan ubomoaji wa nyumba zao na utwaaji wa maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa reli yanashughulikiwa ili Sheria hii mpya ya reli inayotungwa iweze kukubalika kwa wananchi na hivyo kuweza kutekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya wananchi yasiposhughulikiwa ipasavyo na wananchi wakapata haki yao, Sheria hii itashindwa kufanya kazi, na Bunge litakuwa limepoteza muda wake kutunga Sheria ambayo itashindwa kutekelezwa vizuri na wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

.....
WILLY Q. QAMBALO (Mb)

**Kny. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO**

13 Septemba, 2017

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa mawasilisho. Sasa ninayo majina ya upande mmoja tu, upande mmoja haujaleta majina, kwa hiyo, nitaanza na haya majina niliyonayo hapa mbele. Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhary Michael.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kwa namna ambavyo Serikali imeanza kuona umuhimu mkubwa wa kuboresha huduma za reli hapa nchini na hivyo kuweza kuja na muswada ambao utatunga sheria ya kuweza kusimamia masuala ua usafiri wa reli hapa nchi. Tukitambua kabisa kwamba reli ndio njia pekee ya uhakika ya usafiri wa mizigo hapa nchini lakini pia reli ndio njia pekee ya usafiri wa uhakika kwa wananchi wetu na hasa wale ambao ni maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, muswada huu ni muhimu sana, na kama ukitekelezwa vizuri nina imani kabisa utaenda kusaidia sana kwenye suala zima la usafiri hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaunganisha mashirika mawili sasa *RAHCO* pamoja na *TRL* tuweze kuwa na shirika moja kubwa. Ningependa kujua, kwanza wakati watumishi wa *TRL* wanahamia *RAHCO* wapo ambao mpaka leo hawajapata haki (stahiki) zao. Kwa hiyo, wakati mnaenda kuanzisha shirika jipya, je, stahiki za wale watumishi ambao walikuwa hawajalipwa mpaka leo wanaendelea kulalamika, zitalipwa kwa namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukiangalia madhumuni ya muswada huu ni mazuri, moja wapo unaenda kulinda miundombinu lakini pia kwenda kuweka *demarcation* katika ya maeneo yetu. Tumekuwa na tatizo kubwa, na hapa niungane na Kamati pamoja na taarifa ambayo imesomwa na upande wa upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi sasa hivi wanalalamika sana, wamejenga kwenye maeneo ambayo kwa miaka mingi hawakujua kwamba ni maeneo ya *railway*. Wengine walipewa mpaka hati kwenye maeneo hayo lakini leo wanakwenda kubomolewa. Suala lingine ni yale maeneo yanatofautiana kati ya eneo na eneo. Ukiangalia Mkoa wa Tabora, eneo la Tabora Mjini, eneo ambalo wanaambiwa ni

hatua 80, ukija Kaliua ni hatua 120. Kwa hiyo, kiukweli ni wananchi wengi sana wataathirika. Tumekuwa tunauliza kwamba kwanini kuwepo na tofauti hii. Kama barabara ni mita 60 na tunategemea pia kuwa *railway* ambayo ni *standard gauge* lakini haiwezekani kutofautiana Tabora Mjini na Kaliua tofauti na Urambo tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sheria hii inayokuja, tungependa tupate uhakika kwamba haswa upana wa reli ya *standard gauge* ambayo inategemewa kujengwa ni ya aina gani? Lakini pia wale wananchi ambao walikuwa wamejenga miaka mingi na leo wanaenda kubomolewa, nini watasaidiwa na Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, hatukatai kuwepo na miundombinu hii lakini pia wananchi hawakatai pia kuhama yale maeneo lakini kiukweli kuna maeneo ambayo wengine wana hati na wanaambiwa kwamba wamejenga kwenye *railway*, ina maana hapo nyuma kulikuwepo na udhaifu mkubwa. Maeneo ya *railway* kwa kutokuwepo na alama za uhakika yaligawanywa na Wizara ya Ardhi, watu wakajenga lakini leo wananchi ambao ni *innocent*, walipewa hati wanakwenda kubomolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na sheria hii tungependa Serikali iangalie wananchi ambao kiukweli si makosa yao na wakati huo kulikuwa hamna alama lakini leo wanakwenda kunyanyasika. Leo ukimbomolea mtu nyumba hana mahali pa kwenda, ndani ya Kaliua peke yake zaidi ya nyumba 200 zitabomolewa na wananchi ambao ni maskini hana uwezo hata wa kufanya chochote leo hapo alipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye sheria ni ukweli kwamba Mkurugenzi tunaona anapewa mamlaka makubwa sana, kitu ambacho hakiwezekani, mpaka anaambiwa kwamba aweze kuteua kwa dharura na hivyo kutokufuata sheria za uteuzi wakati anapofanya kuweza kuteua mtu anaetakiwa kwenye nafasi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tusiweke mwanya, lazima taratibu zifuatwe kwenye uteuzi, hakuna uharaka wa kumteua mtu ambaye anaenda kushughulikia suala ambalo ni la muhimu anakwenda kutumika kwenye kazi ambako ni husika kwa kutegemea dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya dharura yamekuwa yanatumiza sana, kwa hiyo, tunaomba mamlaka makubwa aliyopewa mkurugenzi yaondoke yaende kwenye bodi. Vilevile linapotokea suala la uteuzi sheria zifuatwe na si kuteua hivi hivi, tutajikuta tumeondoka kwenye lengo halisi la muswada huu na kuja kuweka watu ambao ni dhaifu au ku-*create* mwanya ambao utaleta utendaji ambao ni utendaji mbovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la nauli. Kwamba wamesema pia muswada utasimamia pia masuala ya nauli na masuala ya usafiri kwa ujumla. Sasa hivi tuna shida kubwa sana, na hii inatokana na kuwepo kwa uchache wa mabehewa. Tatizo la kuwepo kwa uchache wa mabehewa limesababisha wananchi wengi kushindwa kutumia usafiri wa reli.

Kwa hiyo ninaomba, pamoja muswada huu wa sheria pia suala la uwepo wa mabehewa ya kutosha liende sambamba, kwa sababu sasa hivi wananchi wengi wanalipa bei *double*. Kama nauli kutoka Kaliua kwenda Dar es Salaam shilingi 23,000 leo wanalipa mpaka shilingi 50,000 kutokana na kulinguliwa zile tiketi.

Kwa hiyo tunaomba kwanza mabehewa yawepo ya kutosha lakini pia utaratibu wa nauli uwe *standard*, ijulikane kabisakwamba nauli kutoka Kaliua kwenda Dodoma kiasi gani, kutoka Kaliua kwenda Dar es salaam ni kiasi gani ili kuondoa tabia za walanguzi kwenda kulangua tiketi na matokeo yake wananchi masikini wanaotaka kutumia barabara ya reli wanashindwa kutumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tulikuwa na maeneo ya magenge yaliyohusiana na suala la ulinzi wa barabara ya

reli. Bila kuwepo kwa ulinzi wa uhakika hii miundombinu haiwezi kulindwa. Mwanzoni tulikuwa na magenge barabarani kwa ajili ya kulinda miundombinu ya barabara ya reli, leo yale yote yamekufa hakuna anaeyaangalia, vile vyuma vimepotea na watumishi waliokuwepo kule kwanza hawakulipwa haki zao waliondolewa lakini pia hakuna anayeangalia miundombinu hiyo sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sambamba na kuwepo kwa sheria hii pamoja na muswada huu, tunaomba pia wale wananchi ambao waliondolewa kwenye yale magenge, waliokuwa wanafanya kazi ya kulinda miundombinu ya reli na hawakulipwa na mpaka leo wapo mtaani kwanza wakapewe haki zao lakini pia magenge yale yaboreshwe ili miundombinu hii ambayo ni ya gharama kubwa sana iboreshwe na kulindwa ili iweze kuwepo leo, kesho na kesho kutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naomba nirudie tena Serikali iangalie kwa namna ya pekee suala la wananchi ambao watabomolewa maeneo yao ili kupisha upanuzi wa barabara ya reli kwa kuwa wananchi wale kiukweli wana hali mbaya na vilio ni vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kama wataachwa kama ilivyo sasa hivi watateseka sana na mwisho wake wengine wataishia kupoteza maisha kwa sababu hawana namna ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante.
(Makofi)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Japhary Michael atafuatiwa na Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, Mheshimiwa Anna Lupembe ajiandae.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Pamoja na hoja zangu nyingi kwamba zinaangua alipopita mchangiaji aliyetangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ninaunga mkono hoja ya kuunganisha Shirika la *TRL* na *RAHCO*, jambo ambalo tumelipigia kelele kwa muda mrefu na nashukuru Mungu kwamba leo limetekelezwa; linaweza likachangia katika ubora wa huduma ya shirika la Reli lenyewe kwa maana ya iliyokuwa *TRL* lakini na kwa maana miundombinu ya reli yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu kubwa ambayo naiomba Serikali iangalie kwa makini ni hoja ya ubomoaji. Maeneo mengi wananchi wamekaa kwa muda mrefu, kama walivyotangulia kusema wengine, Serikali ikiwa inawaangalia, mamlaka mbalimbali zikiwa zinawaangalia. Pamoja na kwamba kuna sheria ambazo pia zinawaruhusu wanapokaa muda mrefu kuwa na haki hiyo ya kuwa katika maeneo hayo, lakini watumishi wa *RAHCO* walikuwepo, wameangalia watu wakijenga *structures* mbalimbali katika hifadhi ya reli lakini hawakuchukua hatua. Leo wananchi wale wanaadhibiwa kwa kuvunjiwa nyumba zao, wananchi maskini ambao hawana uwezo na Mtanzania kujenga nyumba sio jambo jepesi, leo anavunjiwa kirahisi, lakini wale waliosababisha hiyo adha hawajaonesha kuchukuliwa hatua yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni vizuri Serikali ikatazama kwanza namna gani inaweza ikatumia busara kuwasaidia hawa wananchi waliojenga hizo nyumba angalau kwa kufikiri kuwapa fidia ili waweze kukabiliana na changamoto za maisha mbele ya safari. Ni ukweli kwamba ni lazima maeneo hayo ya hifadhi ya reli yabaki yakiwa wazi, lakini wananchi waliojenga kwa sababu waliachiwa wakajenga, basi wafikiriwe jinsi ya kutoa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata wale maafisa wa Serikali ambao hawakutimiza wajibu wao basi wachukuliwa hatua stahili ili angalau mambo haya yasijirudie tena. Kama tutaacha kuwachukulia hatua maana yake wataendelea kuona ni jambo la kawaida na yatakuwa ni maisha ya kawaida kwa watumishi wengine ambao wapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ni kwamba kuna watu ambao wako kwenye maeneo tayari kihalali kwa sababu wana hatimiliki na wamepitia mchakato wote wa kubadilisha maeneo hayo. Pale Moshi kuna eneo ambalo sasa hivi ninavyoongea kuna vurugu iko pale, watu 48 wameathirika, wamewekewa alama ya "X" eneo ambalo haliko kwenye hifadhi ya reli, lakini inasemekana huko nyuma ilikuwa ni eneo la reli, miaka zaidi ya sabini iliyopita. Mamlaka ya Serikali za Mitaa ilishaomba mabadiliko ya matumizi ya eneo lile na wakakubaliwa na Wizara ya Ardhi, watu wamepimiwa, wamepewa vibali vya ujenzi, leo hivi wanaambiwa kwamba hata eneo ambalo lilikuwa la halmashauri, ina hatimiliki, nalo limewekwa alama ya "X" , ni la kuvunjwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unajaribu kujiuliza Serikali inafanyaje kazi? Mimi naamini kabisa kwamba Wizara ya Ardhi ina *records* za ardhi za maeneo yote, ramani zote, haiwezi kutoa kibali cha mabadiliko ya matumizi ya eneo kama eneo hilo lina hati nyingine mpaka libatilishe ile hati. Sasa ilikuaje watu wapewe hati juu ya hati nyingine kama hali iko hivyo?

Kwa hiyo, nadhani Serikali ina haja ya kujitathmini kwa kuyaangalia maeneo na kuyavunja kwa vigezo mbalimbali si kwa kigezo kimoja. Kwamba kila mtu aangaliwe ni namna gani aliingia katika eneo na namna gani anapaswa kusaidiwa ili angalau wananchi wasipate sana hasara kutokana na uamuzi huu wa Serikali wa kuvunja maeneo ambayo yalikuwa ni maeneo ya reli na mojawapo naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie sana eneo la Mji wa Moshi kwa sababu mji ule wanaovunjiwa hawapo kwenye hifadhi ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la abiria ambao bahati mbaya wanakuwa wamecheleweshewa safari yao na Shirika la Reli ni lazima liangaliwe. Kama tunataka kuliingiza shirika hili kwenye ushindani ni lazima liwe tayari kuwafidia abiria ambao kwa uzembe wao ndio wamewachelewesha. Kama abiria wanapaswa kusafiri saa

tano asubuhi, wasafiri, na kama hawasafiri kwa sababu wamecheleweshwa na Shirika la Reli basi wafidiwe. Wafidiwe gharama ya malazi, wafidiwe gharama ya chakula, kwa sababu huo ni uzembe wa Shirika la Reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wananchi wanapokuwa wamecheleweshwa halafu wakapata adhabu ni kulidumaza Shirika la Reli na kuliacha lisiwe katika ushindani. Ni lazima shirika hili liwe la kibiashara na liingie katika ushindani kama mashirika mengine. Na shirika hili hatutegemei abiria wake wawe ni watu wa ndani tu, hata wa nje wanaweza wakasafiri, watalii wanaweza wakatamia reli kusafiri. Sasa kama hatuna sheria za kimataifa za namna ya kuwahudumia abiria maana yake tutakuwa hatuko kibiashara na shirika linaweza likapata pia shida ya kufa tena mbele ya safari. Kwa hiyo ni vizuri tujitahidi tutoe huduma nzuri na ya kutosha kwa abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tiketi; tiketi wanasema kwamba kama umepakia treni sehemu ambayo siyo bila tiketi unapaswa kulipa *penalt* ya asilimia 100. Lakini lazima tuangalie jiografia ya nchi yetu; maeneo mengi inapopita treni ni maeneo ya vijijini sana ambako ni mbali kutoka kwenye stesheni zetu.

Sasa kama mwananchi anataka kusafiri na eneo analotakiwa aende akakate tiketi ni mbali sana ambapo gharama yake ni kubwa na akapanda kwenye treni ambapo ameweza kupanda, kumpiga faini ya asilimia 100 ni kuwaumiza wananchi wa Tanzania ambao ni maskini, na wanaopanda treni ni watu wa vijijini. Ni vizuri tuangalie hiyo, kwamba kwa nini isiwe asilimia 50 ili iwe *affordable* kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la haki ya wafanyakazi. Kuna malalamiko kama wenzangu walivyosema, ya iliyokuwa *TRC* huko nyuma mpaka leo hayajafanyiwa kazi vizuri, tunabadilisha sasa hivi hapa tunarudi tena kwenye *TRC*, sasa tuangalie namna gani tunakabiliana na suala la wafanyakazi ili lisije likawa na shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Frank Mwakajoka ajiandae.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema naipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu wa Sheria ya Reli wa mwaka 2017. Sheria hii tumekuwa tukizungumza muda mrefu sana namna gani mashirika haya mawili yaani *RAHCO* na *TRL* wanaweza kuungana kwa ajili ya ufanisi wa Shirika letu la Reli. Naipongeza Serikali kwa kutuletea muswada huu na ninaunga mkono hoja ya muswada huu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ninayo machache ya kuongelea kwenye muswada huu, Naomba nianze na suala hili la wafanyakazi wa lililokuwa Shirika la Reli (*TRC*) baadaye likaenda *RAHCO* na sasa tunarudi tena kwenye *TRC*. Wenzangu wameshaongelea lakini na mimi ninapenda tu kuwekea mkazo kwamba sasa hii inakuwa kama ni danadana, hawa wametoka *TRC*, wale wafanyakazi wengi bado hawajapata haki zao, lakini wamekuja *TRL* na sasa Serikali wanatuambia kwamba madeni haya yote yatahamishiwa tena kwenye shirika jipya. Sasa ifike mahali Serikali iwe *serious* na jambo hili kwa sababu wafanyakazi wanapokuwa hawajaridhika huwa kunatokea matatizo mengi yakiwemo haya ya hujuma mbalimbali ambazo zinarudisha nyuma uendeshaji wa shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo yalitokea mengi, kwa nini shirika lililokuwa *TRC* lilivunjika. Moja ya matatizo hayo yaliletwa na wafanyakazi wenyewe, lakini pia na baadhi ya sheria ambazo hazikuwa nzuri ambazo sasa nyingine zinafanyiwa marekebisho madogo. Kwa mfano

udhibiti wa tiketi za abiria kwenye ile *TRC* haukuwa mzuri sana kiasi ambacho kilipelekea shirika kupata hasara nyingi. Pia udhibiti wa wizi wa mafuta, shirika lilikuwa likipoteza sana mafuta kwa sababu ya wizi ambao ulikuwa unafanyika na baadhi ya wafanyakazi ambao walikuwa si waaminifu wa Shirika hilo la Reli lililopita. Sasa ninamuomba Mheshimiwa Waziri pamoja na wale ambao watakuwa wanamsaidia waweke uzito mkubwa katika jambo hili kwa sababu ni moja ya vitu vilivyosababisha kuanguka kwa iliyokuwa *TRC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba na mimi niende kwenye suala hili ambalo sasa limekuwa ni kama janga, na ni janga kwa wananchi, hasa hili la bomoabomoa. Niseme mimi Tabora Mjini ni mmoja wa wahanga wakubwa wa bomoabomoa. Tabora Mjini wako wananchi ambao wamejenga ndani ya maeneo ya reli, yaani nikisema mita 30 kwa 30, maeneo yale ya kawaida, lakini pale stesheni 75 kwa 75, wapo wananchi ambao walijenga ndani ya maeneo ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme mimi kama Mbunge wa Tabora Mjini, lakini pia kama Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kusimamia ujenzi huu wa *standard gauge*, pamoja na Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa kwa kutuletea ujenzi huu, tunahitaji sana maendeleo. Tunahitaji maendeleo kwa ajili ya kupata hii *standard gauge*, lakini maendeleo wakati mwingine yanakuja na vilio, vilio hivi ni pamoja na hii bomoabomoa. Pale Tabora Mjini hivi ninavyoongea wale ambao wamejenga ndani ya maeneo ya reli wengi wameanza wenyewe wananchi kubomoa na kuondoka, nawapongeza sana wananchi wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna suala la sintofahamu kwa wale ambao wamepimiwa maeneo yale na mamlaka ambazo nazo zimesajiliwa na Serikali. Kwa mfano ambao wamepewa maeneo kuanzia maafisa mipango miji wa manispaa walipima wakapitisha ramani zao na zikawa *approved* Wizara ya Ardhi na wakapewa hati, wananchi hawa ni wengi sana na wamekumbwa na zoezi

hili, na ni kweli wengine ukipima wanakuwa ndani ya maeneo ya reli sasa hivi kwa sababu kuna ramani ya reli na ramani iliyopo sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hawa waliowapimia ambao ni manispaa, wananchi hawa ni *very innocent* hawajui chochote. Ninaiomba Serikali ione namna gani itawafikiria wananchi hawa. Naelewa Mheshimiwa Rais ana huruma, tumewahi kuona wamachinga wakionewa huruma pamoja na kwamba sehemu nyingine hawakupaswa kuwepo lakini walipewa sehemu nyingine ya kwenda kujihifadhi. Sasa wananchi hawa kwa kuwa walipewa na vyombo halali, na wengine wako mpaka mita 500 nje ya reli, ninaomba Serikali ione itafanyaje kuhusu wananchi hawa kwa sababu kwa kweli wengi ni maskini, kama walivyosema wenzangu na ni wengi mno na hawajui pa kwenda baada ya hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi mamlaka zilizowapa, mbona Dar es Salaam kule nakumbuka kuna baadhi ya watendaji ambao waligawa maeneo sehemu mbalimbali lakini Serikali ilizungumza kwamba wale ambao waliwapa hawa na wao wawajibike. Kwa eneo hili la bomobomoa, tunapenda pia Serikali itufahamisha kwamba wale ambao wamewagawia wananchi hawa maeneo hayo na bado wapo na hawajasema chochote, sijui inakuaje? Vilevile kwa kuwa wamegawiwa na manisapaa, pale ambapo Serikali haiwezi kutenga fedha kwa ajili ya kuwafidia hawa, basi manispaa zile ziwajibike kulipa fidia kwa wananchi ambao walitoa ile ardhi na mpaka wananchi wakapewa hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, na mimi niseme kile kifungu namba 26 pamoja na vifungu vingine ambavyo vimependekezwa na Kamati yetu ya Miundombinu, basi Serikali iweze kuzingatia kwa sababu vifungu vingine vina mapungufu makubwa, na hasa hiki kifungu namba 26 ambacho kinamruhusu Mdhibiti wa *TRL* au wa Shirika la Reli kwenda kukagua peke yake bila kuishirikisha Serikali, ile ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ile *reserve* ya reli iweze kuongelewa vizuri kisheria, *reserve* ya reli imekaaje, iweze kuwa sawasawa na barabara, barabara kuna *beacon*. Anaonekana kabisa mtu hata akitaka kuvamia anaona zile alama kwamba hili sasa ni eneo la barabara katika reli haiko hivyo. Sasa ninamuomba Mheshimiwa Waziri kwamba hili waliwekee kipaumbele kwa sababu ni kweli, leo unaweza ukawa unabomoa huku kesho ulikobomoa mwingine anajenga...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakasaka muda wako umemalizika.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Anna Lupembe atafuatiwa na Mheshimiwa Frank Mwakajoka na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ajiandae.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia muswada huu muhimu sana kwa ajili ya wananchi wa Tanzania. Naomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa uzima na uhai, tuko mahali hapa kwa mara nyingine tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwa kuunganisha *TRL* pamoja na *RAHCO* kwa sababu tulikuwa tunaipigania sana kwa sababu tulijua shirika hili likiwa pamoja litakuwa shirika kubwa kwa ajili ya wananchi wa Tanzania na tukiangalia Shirika la Reli ambalo lilikuwa linaitwa *TRC* zamani lilifanya kazi kubwa na shughuli zao zilikuwa nzuri; sasa tulivyogawanyika pale kazi zilikuwa haziendi vizuri kwa sababu *TRL* walikuwa peke yao na *RAHCO* walikuwa peke yao, lakini leo tunazungumzia kuunda shirika lingine tena jipya

ambalo litafaya kazi vizuri kutokana na sheria hii ambayo tumeileta leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kama wenzangu walivyosema; sisi watu wa Mpanda tunahusika sana na reli hii kwa sababu reli hii ndiyo tegemeo kubwa la wananchi wa Mpanda kwa ajili ya kupitia mizigo na abiria. Ndani ya Wilaya ya Mpanda kuna maeneo makubwa sana ambayo wananchi wa Mpanda watabomolewa nyumba zao. Hili jambo ni kilio kikubwa sana kwa wananchi wa Mpanda kwa sababu ukiangalia pale Mpanda Mjini kuna maeneo ya Tambuka Reli na Ugala wananchi wote watabomolewa nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tu tusesitize kama sisi Waheshimiwa Wabunge. kwa sababu tunatetea wananchi wetu, Wabunge wengi wamesema kwa ajili ya bomoabomoa hii tunaomba kwa sababu hawa wananchi ni maskini, wengine hawana uwezo kabisa wa kujenga nyumba nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali waliangalie upya wale ambao wapo mbali kidogo wawaache kwa sababu ni tatizo. Sisi Wabunge tunavyorudi huko majimboni, tulirudi kipindi hiki cha nyuma kidogo ilikuwa shida, kila mwananchi anakuja kukulilia tutakwenda wapi tunabomolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, ni sikivu, basi waliangalie upya zile mita ambazo wale ambao wako mita mbali kidogo wawaache kwa sababu hii itatuletea shida kidogo kwa sababu wananchi wengi ambao wako katika mguso huu wa kubomolewa nyumba ni maskini sana. Tunaomba Serikali ipitie upya ili tuweze kuwasamehe ambao wapo mbali kidogo wasibomolewe nyumba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile shirika hili lilikuwa lina wafanyakazi; wafanyakazi wa *RAHCO* na *TRL*, kama wenzangu walivyosema, wengine bado wanadai haki zao.

Basi tunaomba Serikali, tunasisitiza walipwe ili hili shirika liweze kwenda vizuri. Vilevile tunampongeza sana Mkurugenzi aliyepewa dhamana ya shirika hili, kulishika *TRL* na sasa linaingia kwenye *TRC*, Ndugu Masanja, anafanya kazi vizuri tunaona. Sasa hivi treni yetu inatembea kwa wakati na muda kamili, lakini kuna tatizo kidogo sisi watu wa Mpanda mmetuletea mabehewa machache sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mpanda wanategemea sana treni. Sasa hivi watu wanaotaka kuunganisha treni kutoka Mpanda mpaka Dar es Salaam wanachaguliwa wanawake 15 na wanaume 15. Hii imekuwa kero wananchi wa Mpanda wanaamka saa 10 za usiku, wanaenda kukaa foleni kusubiri tiketi, mlinzi akitoka pale anawapa wanawake 15 na wanaume 15, hii ni kero kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa sababu hili shirika sasa linaundwa upya, nafikiri mipango na mikakati yake itakuwa mizuri sana. Mpanda kuna abiria wengi sana, tunaomba muitazame Mpanda kwa jicho la huruma; badala ya kutuletea behewa moja, tuleteeni mabahewa hata matatu kwa sababu wananchi wa Mpanda wanapanda sana treni. Sasa hii wanavyopewa wanawake 15 na wanaume 15 inakuwa ni kero na ni shida.

Tunaomba sana mtusaidie kwa hilo kwa sababu shirika hili linaimarishwa upya. Tunaomba basi kuimarisha reli. Sasa kwa sababu shirika hili linakuwa shirika moja, kuna maeneo ambayo *RAHCO* walikuwa hawajayapitia sasa reli haikuwa nzuri, ilikuwa inadengadenga (inasuasua). Basi sasa kwa sababu shirika ni moja, tunaomba uimarishaji wa reli kutoka Mpanda mpaka Tabora uwe mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu amezungumzia kuhusu magenge. Haya magenge yalikuwa yanasaidia sana kwa sababu kutoka genge moja mpaka genge lingine kama hakuna uangalizi, kuna watu majangili ambao wanakwenda kung'oa reli, wanang'oa reli treni ikifika pale inaweza kudondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hii nina mfano nayo kabisa, kuna siku moja nilikuwa nasafiri kutoka Katumba kuelekea Ugala, hapo katikati kulikuwa na magenge yamefungwa. Sasa kuna majangili walienda kung'oa zile reli, bahati nzuri kulikuwa kuna mwehu akaisimamisha treni na yule dereva alikuwa mtiifu akasema huyu mwehu anaisimamisha hii treni acha nisimamisha; alivyosimamisha yule mwehu akamwambia usipite huko wameng'oa mataluma, yule dereva alimsikiliza yule mwehu, kweli kushuka kwenda kuangalia akakuta mataluma 10 yametolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huyu dereva asingekuwa msikivu yale mabehewa ya ile treni yangeanguka na watu wangepata ajali na wengine wangepoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya magenge yalikuwa yanasaidia kwa sababu wale maafisa magenge kule vijijini walikuwa wanapita kuisafisha, ile reli, ilikuwa inakuwa imara treni ikija inapita kwa usalama na wananchi wanakuwa wako katika hali ya usalama zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, TRC ilikuwa ina majengo makubwa sana, shirika hili lilikuwa kubwa, lilikuwa na mtazamo mpana, walikuwa wana Mahoteli kama *Railway Hotel, Iringa Hotel*, walikuwa wana mabasi, shirika hili lilikuwa kubwa sana. Sasa kutokana na kuingia kwenye ubia yela majengo yote yakagawanyika, yakauzwa na mengine yakatelekezwa maana yake mengine yamekuwa kama vile magofu. Ninaomba kupitia hili Shirika jipya ambalo tunaliunda upya, yale ambayo yaliyokuwa yanafanywa wakati ule, walikuwa wana magari ya mafuta, walikuwa wana mabasi, viimarishwe zaidi kwa ajili ya wananchi ili waweze kupata usafiri wao kwa urahisi na wepesi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha wa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Anna Lupembe muda wako umekwisha.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Frank Mwakajoka atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na Mheshimiwa Mussa Ntimizi ajiandae.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kwanza kushukuru sana hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, imeandaliwa vizuri na kama ushauri huu uliotolewa kwenye hotuba hii utazingatiwa unaweza ukaboresha zaidi sheria hizi na tukafanya vizuri zaidi kwenye Shirika letu la Reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa ambacho ninataka kukizungumza ni kwamba Shirika hili la Reli lilikuwepo huko nyuma baadae likafutwa na sasa limerejeshwa upya na hiki ni kilio cha Wabunge wengi ambao walikuwa wakidai kwamba tunatakiwa kuliunda upya shirika hili, lakini kikubwa tu ni kwamba ni vizuri sana Serikali iwe inafanya utafiti wakati inataka kuanzisha mashirika mbalimbali au kubadilisha sheria mbalimbali kwa ajili ya kuanzisha mashirika ili kuleta tija katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeonekana kabisa katika nchi hii, kitengo cha utafiti kimeonekana kabisa kwamba hakihudumiwi ipasavyo na hakifanyi kazi zinazotakiwa na ndiyo maana tunaona kila kinachoanzishwa kinaanzishwa halafu baadae kinakufa na tunarudi kuja kuanzisha kingine. Hii inaonyesha ni jinsi gani ambavyo tumekuwa na Hati za Dharura nyingi sana katika Bunge hili ambazo zinaletwa na Serikali. Tunafikiri kitengo cha utafiti kiimarishwe zaidi ili waweze kufanya utafiti ukiwa ni wa kiwango cha juu na ambao tukianzisha uwekezaji wowote uwekezaji ule unapata tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa nataka nizungumzie kuhusiana na bomoabomoa ambayo

inaendelea katika maeneo mbalimbali hasa kwenye maeneo ambayo reli inakwenda kujengwa na reli inakopita. Wananchi wanalalamika sana na takwimu zilizopo sasa hivi ni kwamba karibuni nyumba 3,244 (makazi ya wananchi) yatakwenda kubomolewa wakati wa ujenzi wa reli na hao wananchi wote asilimia kubwa ni wananchi ambao wanaonesha kabisa kwamba wako kwenye mipango miji. Wengi wamepimiwa nyumba/viwanja vyao na wakapewa na Serikali lakini leo hakuna ufafanuzi wowote unaotolewa kwa wananchi hawa ni jinsi gani ambavyo wanaweza wakalipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, na jambo hili linaleta chuki kubwa sana kwa wananchi na linaathiri sana ustawi wa maisha ya wananchi wenyewe. Tunafikiri kazi ya Serikali ni kuhakikisha kwamba ustawi wa wananchi unakuwa vizuri na siyo kuharibu ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri Serikali ingekuwa inatoa mwelekeo kwamba hawa wananchi wote ambao tayari wako kihalali na wamepewa ardhi hizo na Serikali na wamejenga, wamewekeza katika maeneo hayo Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inawafidia wananchi hawa ili waendelee kuishi katika maisha yao ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine wananchi hawa wamekuwa wakienda Mahakamani mara kwa mara na Mahakama imekuwa ikitoa *stop order* ya utekelezaji wa uvunjaji wa nyumba cha kushangaza ni kwamba, unakuta Serikali inaendelea na uvunjaji wa nyumba pamoja na *stop order*. Tunafikiria sana kwamba Serikali inaleta miswada mbalimbali ya sheria hapa na sheria hizi zinakuwa zinatumiwa katika nchi hii lakini wananchi wakifuata sheria bado Serikali haitaki kufuata sheria na kuona Mhimili wa Mahakama una wajibu wa kuhakikisha kwamba unawasaidia wananchi hawa na badala yake inaonekana kwamba Serikali ina dharau Mhimili wa Mahakama, inaendelea kuvunja, wananchi wanaendelea kulalamika na hawajui waende wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo lazima Serikali pia ijue kwamba Mhimili wa Mahakama ni muhimu sana na Serikali ndiyo inatakiwa kuwa ni ya kwanza kabisa kutekeleza Sheria za Nchi lakini inaonekana kwamba Serikali imeshindwa kutekeleza sheria za nchi, wananchi wamekwenda Mahakamani Serikali inaendelea kuvunja wakati Mahakama imeshazua, sasa jambo hili kwa kweli linasumbua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona pia kumekuwa na tatizo kubwa sana, sheria ambayo imeletwa leo hasa kwenye kifungu cha 28 ambacho huko nyuma kilikuwepo, kilikuwa ni kifungu cha 32 kwenye Sheria ya mwaka 2002, bado kimerajeshwa kama kilivyo. Kinaendelea kutoa haki kwa mwananchi kama reli ikipita kwenye nyumba yangu hakuna majadiliano, wanachokifanya wao ni kuangalia hili eneo linaweza likapitishwa reli basi, mimi ni mtu wa kuondoka hakuna ufafanuzi wowote uliotolewa kwenye sheria hii, kwamba nini ambacho kitaendelea baada ya kuona ya kwamba lile eneo reli itapita, mwananchi atafaidika namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ile Sheria ya Fidia inaonekana kwamba kwenye Sheria ya Reli haitumiki kabisa, kwa maana hiyo wakiamua kupitisha kwenye eneo lako, kwenye shamba lako au wakiamua kupitisha kwenye nyumba yako ina maana kwamba hiyo reli itapita pale na hakuna fidia yoyote itakayotolewa kwako. Jambo hili linaonesha kabisa kwamba Serikali ni namna gani inajipanga kutokutekeleza ile sheria ambayo imeleta yenyewe na imeitunga yenyewe kuonesha kwamba mwananchi yeyote ana haki ya kumiliki ardhi na kwa sababu ni mtu anayeendeleza ile ardhi kama kuna jambo lolote linakwenda kufanyika pale au kutekelezwa katika eneo lile basi atalipwa fidia, jambo hili halionekani kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni pamoja na hawa wananchi ambao tumesema 3,233, hawa wananchi ni wengi sana na katika nchi hii imekuwa ni tatizo kubwa, bomoa bomoa kila maeneo. Ukienda kwenye barabara bomoa bomoa inaonesha kabisa Wizara ya Ujenzi

haiko makini ni kwa nini imeshindwa kuweka alama katika maeneo yake yote, ukianza barabara lakini pia ukienda kwenye reli na maeneo mengine, imeshindwa kuweka alama ambazo zinaonyesha kwamba wananchi wanapokuwa wapo kwenye maeneo yao au wanapotaka kujenga wawe wanajua kwamba haya maeneo ni maeneo ya reli au ni maeneo ya barabara, Wizara imeshindwa kutekeleza wajibu wake. Tunataka tujue Serikali sasa hivi ina mpango gani kuhakikisha kwamba inaweka alama hizo ili wananchi hawa wasiendelee kupata matatizo ya namna hiyo siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima ikubaliane nasi kwamba kitendo cha kumvunjia mwananchi wake nyumba ni kumrudisha nyuma na kurudisha maendeleo nyuma ya wananchi. Kwa hiyo, ni lazima Serikali ijpange kama inataka kufanya maendelezo sehemu yoyote ni lazima ikubali kwamba kama kuna wananchi wako pale basi wananchi wale wafidiwe na baada ya kufidiwa basi wakajenge makazi mengine katika maeneo ambayo wanaweza wakaishi na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanapata shida ukienda kwenye barabara Watanzania wanalala nje, leo kwenye reli hawa wananchi nani atawahifadhi wananchi wote hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijaweka hata utaratibu ni namna gani wananchi hawa itakwenda kuwahifadhi, wanawaona kama ni watu ambao hawakustahili kabisa kuwepo pale wakati Serikali pia ilikuwepo kwa nini haikuweza kusimamia haya ambayo yalikuwa yanafanyika kipindi hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wananchi wapewe nafasi kubwa ya kusikilizwa na pia wahakikishe kwamba wanapewa maeneo ya kujihifadhi kwa kipindi hiki ambacho tayari Serikali inataka kuwaondoa katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni pamoja na sheria

hii ukiangalia Kifungu cha 16 mpaka 23 Mamlaka ya Reli yule mtu anayesimamia yale maeneo anaweza akaenda kwenye kijiji au kwenye makazi ta mtu na akaanza kufanya tathmini ni namna gani wanaweza wakapitisha reli hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yale maeneo wako viongozi wa Serikali za Mitaa, wako viongozi wa vijiji, wako Viongozi wa vitongoji na Waheshimiwa Madiwa wakashirikishwa katika yale maeneo nini ambacho kinaendelea pale na watoe ushauri wao na ikiwezekana wawe na nafasi kwenye sheria hii ni namna gani ushauri wao pia unaweza ukachukuliwa na kwenda kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Ntimizi, tutamalizia na Mheshimiwa Margaret Sitta.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia. Moja niipongeze Serikali kwa dhati kabisa kwa kuunganisha mashirika haya mawili na kuwa shirika moja na kuifuta *RAHCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakuwa katika mitazamo miwili, moja *specific* kwenye sheria lakini mwingine utakuwa ni mchango wa jumla. Nikichukua sheria hii iliyoletwa na Serikali, ukienda *page number eight*, kifungu namba tano kwenye *objects of corporation, there is no anywhere* kwenye *objective* za shirika zimesema *specifically* kwamba tunaanzisha shirika hili kwa ajili ya *commercial interest* na kutengeneza faida, hakuna. Ukitazama *objective* na kila kitu kilichooneshwa hapa *it is pure service delivery and not profit making organization*, na hili ni tatizo *from the day one*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningeshauri, katika kipengele namba tano tungeongeza kifungu, tunasema kwamba; *“to invest and generate profit for the United Republic of Tanzania”* ili *management* inapoingia madarakani ijue

jukumu lake la kwanza ni kutengeneza fedha kwa ajili ya Serikali, hilo jambo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nikienda *page number ten* kwenye *composition of Board*, ningeshauri tungekuwa *specific* katika aina ya watu tunaowaweka katika *board* na mmojawapo wa wawakilishi akawepo wa kutoka *private sector* kwamba katika *board members* watakaokuwa wanatengeneza *board* ya shirika hili mmojawapo atoke katika sekta binafsi, kwa sababu shirika hili linatarajia kufanya biashara na umma ili huyu mtu wa sekta binafsi angalau apeleke *the mindset, the perception* ya kufanya biashara katika *board*.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni ushauri wangu kwamba tunapotengeneza *composition* tuseme *specifically* kwamba kutakuwa na uwakilishi wa mtu kutoka katika sekta binafsi ili tusitoe *room* unaweza wakashangaa wakachangukiwa Makatibu Wakuu wa Serikalini tupu humu ndani, halafu tukarudi kule tulikotoka kwa sababu tuna *bad experience*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *functions of the board page number eleven*, kifungu namba 13. Tugesema moja ya *function* ya *board* ni ku-*approve annual strategic plans* na ku-*evaluate monthly performance* ya *management*, ili kui-*commit management* kuwa ina-*provide monthly report* ya *performance* ya shirika halafu kila *quarter board* ina-*evaluate* hizi *performance* za kila mwezi ili tuweze ku-*take corrective measures* mapema badala ya kusubiri muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo jingine nilitaka niende *page number 33* na hapa nataka niishauri Serikali kwamba kwenye *financial provisions*, kwenye *Finance Bill* tuliyopitisha hivi karibuni tuliweka *exemptions* ya *levy*, ningeomba kifungu namba 69(4) ambacho kinasema; "*The provision of subsection 3(c) shall not apply to exemption provided under the East African Community Custom Management Act.*"

Mheshimiwa Naibu spika, hapa tungeongeza *exemption* tulizotoa kwenye *levy* ambayo tulikuwa tuna-charge 1.5 percent kwenye mafuta ya ndege, kama mtakumbuka kwenye *Finance Bill* tulifuta tozo hii ya reli kwenye mafuta ya ndege ili kufanya viwanja vyetu vya ndege kuwa *competitive*. Tusipofanya hii *exemption* kipengele hiki kinaenda ku-over rule maamuzi tuliyoyapitisha kwenye *Finance Bill* and this will be a problem. (Makofi)

Mheshimiwa naibu Spika, ningeshauri kwenye *liability* za *TRC* nilitaka niishauri Serikali; tunajenga *standard gauge railway system* kwenye nchi yetu, *we will be competing* na watu wengine. Ukisoma *liability*, shirika limejiwekea *protection* isiyokuwa na vipimo. Twende *page numbe 22* kifungu namba 38 *“The Corporation shall not be liable for any loss arising from the delay cause by the failure of any train to start on or complete any journey within set time”* nani anaye-determine hii *set time*? ni shirika lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni *loophole* na nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, *the bottom line* ya *railway business* siyo kusafirisha abiria ni mizigo, sasa tuta-compete na wenzetu *if this protection* tuliyojiwekea haitokuwa *competitive* na wengine, *investment* tunayofanya kama nchi itakuwa *waste*. Tukae tufikirie kwamba kuna *another Northern Corridor* ina hiyo *standard gauge railway system* ya Kenya ambayo inaenda hadi Kigali na *our objectives* ni kwenda ku-save market ya Congo, ku-save market ya Kigali na maeneo ya namna hiyo. Kwa hiyo, ukitazama hiki kipengele tumejifunga sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele namba 40 kinasema hivi naomba Waheshimiwa Wabunge mnisikie:

“The liability of the corporation in respect of any animal, shall not in any case exceed the appropriate amount set out in the tariff book unless at the time of acceptance of such animal by the corporation.” Kwa nini tuiseme; *“as per the market rate”* ili ku-provide confidence ya mtu anayekuja kuchukua huduma kwamba mkinisababishia hasara mimi

nitakuwa *determined* na soko siyo *tariff book* uliyotengeneza wewe, *this is not competitive*, nataka niiambie Serikali hapa na Mkurugenzi wa *TRL* yuko hapa ametoka kwenye *private sector*, *he should not get the disease of magonjwa ya Serikalini*. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

He is running the organization ambayo tunatarajia kwenda kutengeneza fedha. Lazima iwe *more competitive*, sheria hizi tukae tukijua wafanyabiashara wataangalia sheria yetu ya shirika, wataangalia sheria ya mashirika *competitive*, haya ni ya upande wa kisheria. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme mambo ya jumla wenzangu Waheshimiwa Wabunge wameongelea sana suala la bomoa bomoa. Tabora ni moja ya eneo *affected*. Zinabomolewa kaya zaidi ya 500 Tabora, miongoni mwao ni watu waliojenga zaidi ya miaka 50, 60, 70, 80 wapo watu waliojenga katika maeneo hayo. Kuna bibi anavunjiwa nyumba ana umri wa miaka 80 hana familia yuko peke yake, alipewa hati na Serikali, alikuwa analipa kodi za Serikali anafanya nini. Ningeomba Waziri pamoja na kuwa hatujaja kujadili, tunajadili sheria, *give us a statement of hope* kwenye hili jambo *because tuna-represent* watu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Serikali inajenga *standard gauge* na ningeomba kwa heshima Serikali na *TRL* sasa tumeipatia *assets* za kutosha, jamani hatuwezi kujenga *standard gauge* kwa fedha zetu za ndani, *this will be a dream which we will never be realized*. Niishauri Serikali sasa mmruhusu *TRL* aende kwenye dunia kutafuta fedha za ku-*invest* kwenye *standard gauge*, hatuwezi kufanya kila kitu kwa fedha zetu za ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajenga reli kwa hela yetu ya ndani, tunajenga *megawatts 2100* za umeme kwa hela yetu ya ndani, tunanunua ndege kwa hela yetu ya ndani, *we are going to suffocate this economy*, huu ni ushauri. Iruhusuni *TRL* ikakope ijiendeshe na nimshauri Mkurugenzi wa *TRL* na Waziri, *it is uneconomical* kujenga reli kwenda Mwanza

kwanza, twendeni Kigoma, twendeni Kalemii, twendeni Uvinza, twende Msongati halafu jengeni Mwanza. Niitahadharishe Serikali msiweke fedha za wananchi *for political reasons.* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka ukanda huo ningependa nipande Bukene *standard gauge*, lakini *it is not going to pay*. Fanyeni *cost benefit analysis*, wapi tunapeleka, tukienda Lake Tanganyika tutahudumia *part of Congo*, tukienda Kalemii tutahudumia *the Western part of Congo*, tukienda Uvinza tukaenda Msongati tutabeba mzigo wa Nikel siku ya mwisho reli hii itajiendesha kibiashara. Niitahadharishe tena Serikali kwa heshima...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bashe muda wako umekwisha. Kabla hujakaa umezungumza kwamba Mkurugenzi ambaye yuko maeneo haya asije akaugua ugonjwa wa Serikali. Hebu futa hiyo kauli kwamba Serikalini kuna ugonjwa.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nafuta. (Makofi)

NABU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Musa Ntimizi, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajjandae.

MHE. MUSA R. NTIMIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kidogo katika Muswada huu wa Reli.

Kwanza kabisa binafsi nina furaha leo kuiona Serikali imepokea mawazo na ushauri wetu tuliokuwa tunatoa siku nyingi kuhusiana na kuunganisha *RAHCO* na *TRL*. Tulikuwa tunatoa mawazo hayo kwa sababu tulikuwa tunahitaji tupate shirika ambalo litaisaidia nchi na litasaidia wananchi wetu katika kupata huduma za usafiri. Leo tunashuhudia

Serikali imekubali wazo letu na sasa tunaelekea kuyaunganisha mashirika mawili ya *TRL* na *RAHCO* kuunda shirika jipya la *TRC*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya watu wanasema tunarudi kule kule lakini kwa muswada ulivyo, tunaunda shirika jipya la *TRC* baada ya kuunganisha *TRL* na *RAHCO*. Naunga mkono muswada huu kwa asilimia mia moja, lakini mimi pia ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Tumeishauri Serikali kwa kiwango kikubwa sana lakini yapo ambayo pia ningengezea kama mchango kwa niaba ya wananchi wa Igalula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema tunaunda sasa Shirika la *TRC* lakini pia Serikali yetu sasa iko katika mkakati mkubwa wa kujenga reli ya *standard gauge* kuanzia Dar es Salaam kuelekea Tabora. Na mimi kabla sijafika mbali niungane na wazo la Mheshimiwa Hussein Bashe la kuangalia faida ya *standard gauge* kuipeleka Kigoma kabla ya kuipeleka Mwanza, kiuchumi itatusaidia zaidi kuliko hili wazo la sasa la kuipeleka kwanza Mwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, reli inapoboreshwa, tutakapojengewa *standard gauge* sisi kama nchi tutapata faida kwa maana ya kwanza tutasafirisha mizigo yetu mingi na mizito kupitia reli yetu. Tutatunza barabara zetu ambazo tunatumia gharama kubwa sana kuzijenga kwa kodi ya wananchi, nina hakika kabisa tukiitengeneza reli ikawa bora ikasafirisha mizigo mingi hela zile tunazotengeneza barabara zitaenda kwenye maeneo mengine ya uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tutachangia Pato la Taifa, Tutasafirisha mizigo mingi, maana yake sasa Serikali itapata kodi nyingi, itapata pesa nyingi shirika letu la reli sasa litaweza kuchangia katika Pato la Taifa badala ya sasa Shirika la Reli linaendeshwa na ruzuku kutoka Serikali Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Igalula reli ni usafiri tunaoutegemea sana. Kata ya Tura, Kizengi, Kata ya

Goweko na Kata ya Igalula kwa asilimia mia moja wanategemea usafiri wa reli. Kuimarika kwa shirika hili kutasaidia usafiri wa mazao yao, kutasafirisha asali yao, kutasafirisha wananchi wao na vilevile kupunguza shida kubwa ya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unaanzisha Shirika jipya la *TRC* na Bodi ya Wakurugenzi, kifungu namba nne cha muswada, tunaitaka bodi sasa iwe na muono wa kibiashara wa shirika hili. Tuondokane na kule ambako tulikuwa tunaliendesha shirika hili kama kutoa huduma ya usafiri tu, lakini sasa shirika na bodi inayoundwa ikaangalie namna ya shirika hili kujiendesha kibiashara. Tuondokane na mazoea. Shirika hili lilivyokuwa mwanzo lilikuwa linaendeshwa kwa mazoea, lakini sasa tunataka kwa sababu tunaanzisha shirika jipya, liwe jipya sio kwa kubadilisha jina lakini liwe jipya kwa huduma zitakazotolewa, tuwe na mabehewa ya kutosha ya kusafirisha mizigo na abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani kulikuwa na wizi mkubwa wa mafuta na vipuri udhibitiwe, pia huduma za ndani ya treni zilikuwa haziridhishi. Mabehewa mengine yalikuwa mpaka yana kunguni na chawa ndani. Hatuwezi kufanya biashara kwa mazoea. Vilevile tuboreshe mtandao wa reli, reli ilikuwa inapata ajali mara kwa mara kwa sababu mtandao wa reli ulikuwa umeshachoka kwa kiasi kikubwa sana. Pia tujali muda, muda wa safari treli mara nyingi ukikata tiketi, unaweza ukakata tiketi kuondoka saa 12 lakini ukakaa stesheni mpaka saa 12 kesho yake safari bado haijaanza. Tunaomba sasa shirika hili linalokuja liangalie yote haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapotaka kuanzisha shirika hili jipya tuangalie maslahi ya wafanyakazi wetu. Tuliingia mgogoro mkubwa sana wakati tunaanzisha *RITES* na *RAHCO*, wafanyakazi wakaenda Mahakamani wanadai haki zao. Kudai haki zao wafanyakazi wetu wana nafasi ya kuhujumu shirika kwa namna moja au nyingine. Mimi nashauri wakati tunaanzisha mchakato huu maslahi ya wafanyakazi

yashughulikiwe kwanza, walipwe madai yao kwanza ndiyo sasa tuhame *a fresh* kwenye shirika jipya la TRC. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu namba tano cha Muswada kinazungumzia majukumu ya shirika. Kinazungumzia uendeshaji wa reli ndani ya mtandao na miundombinu yake. Kuhakikisha ulinzi na usalama wa mazingira ya reli. Hapa nataka nisemee suala ambalo Wabunge wamelisemea sana, kuhusiana na bomoabomoa sasa. Kama shirika hili lingeendelea kutunza mipaka na maeneo yake kwa muda mrefu, haya matatizo ambayo tumeingia sasa yasingekuweko. Wananchi wamejenga kwa zaidi ya miaka 40 katika maeneo haya, leo wanakuja kuambiwa wanavunjiwa. Shirika lilikuwa wapi? Mamlaka zilikuwa wapi? Lakini tunachokiomba sasa wananchi wetu wanataka *standard gauge*, wanataka reli iliyo bora. Wale waliokuwa katika zile mita za reli wako radhi kuondoka, lakini kuna mgogoro mkubwa wa wananchi wetu ambao walijenga yanayosemekana ni maeneo ya reli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba wananchi hawa Serikali iwaangalie na ikiwezekana mamlaka zilizohusika katika kufanya haya waweze kuchukuliwa hatua ili wananchi wetu waweze kupata haki yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Margaret Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoko mezani inayohusu uanzishaji wa shirika jipya la reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naipongeza sana Serikali, mimi natoka Mkoa wa Tabora Wilaya ya Urambo, kwa miaka yote tumetegemea usafiri wa reli, kwa hiyo, katika mambo ambayo naipongeza Serikali ya awamu hii hasa ni uamuzi wa kujenga reli hii kwa *standard gauge*.

Hongera sana Serikali, endeleeni kuimarisha reli inayotarajiwa kujengwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni maombi na ushauri wakati huo huo; sisi kama wananchi wa Urambo tunategemea sana *station* ya Urambo, natoa ombi maalum kwa Serikali kwamba *station* ya Urambo iimarishwe kwa sababu huwa inakuwa na wasafiri wengi sana wanaoshuka pale. Lakini wakati huohuo sio kuimarishwa *station* tu lakini pia iwekewe ulinzi kwa sababu mara nyingi kama ratiba itabadilika, ikiwa treni inapita usiku ni jambo la hatari sana. Kwa hiyo, naomba ulinzi uimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili katika Wilaya ya Urambo tuna *check line* mahali ambao wananchi wanavuka reli. Tunaomba zile *check line* ziendeele kuwepo na ziimarishwe, zikiwemo za Usoke, Sipungu, Ulasa, Urambo nakuomba pia Kata ya Vumilia haina *check line*, tunaomba iwekewe pale kwa sababu kuna kijiji watu wanaishi upande wa kaskazini ambayo inawapa shida sana kuvuka reli. Tunaomba *check line* iwepo katika Kata ya Vumilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishauri Serikali, magenge yaliyokuwepo yarudishwe, yaimarishwe, yalikuwa yanasaidia kuimarisha ulinzi wa reli. Wakati huo huo, zamani kulikuwa na wakaguzi wa reli, tunaomba wakaguzi wa reli waendeele kuwepo kwa sababu walikuwa wanasaidia kukagua reli kila siku badala ya kusubiri ajali itokee. Walikuwa wanatambua sehemu zenye matatizo kabla reli haijafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kumekuwa na matukio mabaya sana ya uhalifu ndani ya mabehewa. Naomba pia ndani ya mabehewa kuwe na ulinzi hasa wanaposhuka usiku au wanapopanda usiku tunaomba ulinzi uwepo ndani ya mabehewa wanayosafiria wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunatoa wito kwa Serikali kuwalipa wafanyakazi waliokuwa katika shirika ambalo sasa linaisha muda wake ambalo limeunganisha kwenda kwenye hili shirika jipya la reli TRC. Tunaomba

wafanyakzi wote kabla hawajahamia huko wawe wamelipwa fedha zao kuondoa usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuiambia Serikali kwamba suala hili ni la biashara, litatusaidia wananchi kwa usafiri wetu wenyewe na mizigo ikiwemo tumbaku ambayo mizigo hii ilikuwa inaharibu sana barabara zetu ambazo zimejengwa kwa gharama kubwa. Kwa hiyo mizigo hii mikubwa itasaidia kuokoa barabara zetu. Pia tutapata fedha nyingi kutokana na mizigo inayotoka Congo, Uganda, Rwanda na nchi nyingine za jirani, kwa hiyo itasaidia pia kuimarisha uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimaliziae kwa kusema kwamba wananchi wa Urambo na Tabora kwa ujumla tunakaribisha sana Serikali ijenge hii reli haraka iwezekanavyo ili itusaidie, ulikuwa ni utaratibu wetu kutegemea zaidi reli kuliko barabara. Baada ya kusema hayo naendelea kuipongeza Serikali, tunaomba reli ijengwe haraka iwezekanavyo ili tuondokane wa njia zingine za usafiri ambazo pia zimekuwa ghali kwa wananchi wenye uwezo mdogo kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii kukushukuru sana, pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia kwenye Muswada huu. Pia napenda kuishukuru sana Kamati yetu ya Kudumu ya Miundombinu, ni Kamati ambayo nafikiri leo wamefurahia sana kwa sababu kwa kipindi chote hicho walikuwa wamesimamia kwa makini kwamba *TRL* na *RAHCO* lazima iwe kampuni moja. Nafikiri walikuwa wanafanya hivyo kwa sababu walikuwa wanajua hasa changamoto zilizopo katika kampuni yetu ya *TRL*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sababu za msingi ambazo zimesababisha tuweze kuunganisha *TRL* na *RAHCO*. Kwanza kabisa kiutendaji, *TRL* ina wafanyakazi takribani 1,900 wakati *RAHCO* ina wafanyakazi 38. *TRL* kazi yake kubwa ni kuendesha usafiri wa treni, *RAHCO* kazi yake kubwa ilikuwa ni kujenga miundombinu. Sasa hizi kazi kikawaida zinatakiwa zifanywe pamoja lakini kulikuwa na changamoto kubwa hapo zamani. Kwa mfano, kukitokea tatizo kwenye barabara na *RAHCO* kama hawako tayari kwenda kutengeneza barabara hiyo au reli ina maana *TRL* wanashindwa kufanya kazi. Kwa vile ilikuwa siku zote *TRL* inategemea sana *RAHCO* na *RAHCO* wakati mwingine hawako tayari kufanya kazi yao ya kufanya ukarabati wa njia za reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ilisababisha kwanza kushuka kwa kiasi kikubwa cha mapato ya *TRL* pia kwa upande mwingine ilisababisha vilevile utendaji wa bandari yetu. Pia ilisababisha vilevile uharibifu wa barabara kwa sababu mizigo mingi sana ilianza kuhamia kwenye barabara. Kwa bahati nzuri tulliona kama Serikali na Kamati yetu ya Bunge waliliona wakalisimamia na leo hii tumefanikiwa kuleta Muswada huo. Tunawashukuru sana wale ambao walisimamia jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipekee vile vile napenda nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amesimamia sana sana utengenezaji wa muswada huu kwa ajili ya sheria hii ambayo leo tunataka tuipitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli muswada huu umekuja wakati muafaka kwa sababu sasa hivi nchi yetu iko katika ujenzi wa *standard gauge*. Tuna mpango ambao tunajenga *standard gauge* kwa awamu, sasa tumeanza awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro ambayo ni takribani kilometa 215 ujenzi umeanza, ukijumlisha na zile barabara za kupishana, takribani kilometa 300. Ujenzi huu umegharimu takribani dola za Kimarekani bilioni 1.219.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili itaanza Morogoro mpaka Makutupora. Sasa hivi tumeshampata

Mkandarasi na mazungumzo yanaendelea baina ya Serikali na Mkandarasi huyo kuhakikisha kwamba kazi hiyo inaanza kujengwa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili itakuwa ni Makutupora mpaka Tabora, Tabora – Isaka – Mwanza. Vilevile kutoka Tabora kwenda Kigoma halafu kutoka Tabora kwenda Mpanda – kazi hiyo inafanywa na tunajipanga na tunafanya kila linalowezekana ili kazi hiyo ianze mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mambo mengi Waheshimiwa Wabunge wamechangia. Kwanza tunashukuru sana kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wote wameukubali muswada huu asilimia mia moja. Tunawashukuru sana kwa sababu wanajua muswada huu una manufaa makubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na maoni mawili, matatu ambayo nitajaribu kuyagusia moja baada ya lingine. Kwanza kulikuwa na suala la *ticket* kwamba faini kubwa kwa ajili ya tiketi wale waliokuwa hawana tiketi tumeweka faini asilimia moa moja. Ni kweli tumeweka faini hii kwa sababu tunataka watu sasa wachukue dhamana, wawe na *responsibility*. Mtu hawezi tu kupanda treni bila ya kulipia tiketi, haiwezekani! Lazima Watanzania sasa tubadilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna changamoto. Kuna baadhi ya maeneo ambayo kweli hayana vituo vya kukatia tiketi. Kwenye sheria hii ukienda kwenye kifungu cha 47(3) imezungumzia kuhusu maeneo ambayo hayana vituo vya kukatia tiketi. Sasa hili limeangaliwa vizuri kwenye sheria hii na katika maeneo hayo mtu ataruhusiwa kupanda kwenye treni na atakata tiketi mle ndani ya treni. Lakini maeneo yote ambayo mtu anapanda treni bila tiketi atalipa faini asilimia moa moja. *Otherwise* lazima tubadilike na tuhakikishe kwamba tunasimamia sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyokwenda utaratibu mwingi sasa tutakwenda kwenye *electronic ticket*. Hutahitajika hata kwenda kwenye kituo cha kukata tiketi,

kwenye simu yako, kama unaponunua vocha, unapolipia maji, kama unapolipia umeme wa luku na tiketi itakuwa hivyo hivyo.

Kwa hiyo, nawaomba Watanzania wenzangu, nawaomba Waheshimiwa Wabunge muelewe sasa lazima kwa wale ambao hawatalipa tiketi au hawatanunua tiketi lazima walipe faini asilimia mia moja, vinginevyo tukifanya hivyo hii biashara haitaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la magenge. Ni kweli magenge ni muhimu sana katika uendeshaji wa reli na hapo katikati tulipokuwa na *TRL* mambo ya magenge yamekufa lakini sasa tunaanza upya na tutahakikisha kwamba tunaimarisha magenge sehemu zote ambazo njia za reli zinapita. Tukifanya hivyo tunaamini hata utendaji, usalama wa reli sasa utaimarika zaidi kwa vile hili ni jambo zuri na tunaendelea kulisimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala ambalo limezungumzwa sana na kila Mheshimiwa Mbunge aliyesimama hapa kuhusu wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi waliokuwa *TRC* ambao walihamia *TRL* ajira zao ziliendelezwa kwa masharti ya ajira waliyokuwa nayo. Wote ambao walitokea *TRC* tuliwapeleka *TRL* na *RAHCO* na ajira zao ziliendelezwa kama mikataba yao ilivyosema na malimbikizo yao ya madeni yote yalilipwa.

Kwa vile Waheshimiwa Wabunge, wale wote ambao walikuwepo *TRC* (*Tanzania Railway Corporation*) ya zamani wote tumewalipa na maslahi yao na haki zao zote za utaratibu wa kazi tulizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi waliokuwa *East African Railways Corporation* nao vilevile stahili zao zote walilipwa. Ni utaratibu wa Serikali unapomhamisha mtu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine stahili zake na haki zake zote zinalipwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa wafanyakazi wa *TRL* na *RAHCO* watakaohamishiwa kwenye shirika jipya hili, stahili zao zitalipwa. Ukienda kwenye muswada huu, kuanzia kwenye kifungu cha 115 mpaka 118 tunazungumza haki za wafanyakazi wa *RAHCO* na *TRL*. Wote ambao watahamishwa haki zao zitaangaliwa na wale ambao watapelekwa Serikali, haki zao zitaangaliwa; na wale ambao watapelekwa kwenye taasisi mbalimbali, haki zao zitaangaliwa; na wale ambao wataachishwa kazi haki zao zitaangaliwa na watalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie Wabunge kwamba sheria hii imeangalia mambo yote hayo, na sisi kama Serikali tumejipanga vizuri. Kulikuwa na suala lingine kuhusu utaratibu wa ufanyaji kazi kwenye sehemu za reli kuhusu *survey and inspection*. Ukienda kwenye kifungu cha 26 - *Surveys and Inspection*, tumesema pale; "*an authorized officer of the Corporation may, on the production of evidence of such authorization if required to do so enter on any land or a dwelling house,*" anaweza kuingia popote. Hicho ni cha kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda tena kifungu cha 26(2) inasema; "*Before an authorized officer enters any land or a dwelling house he shall obtain consent of the owner or occupier of the land or dwelling house.*" Kwa hiyo, hawawezi tu kwenda kuingia isipokuwa lazima wafuate utaratibu huo ambao tumeueleza na hiyo tumeeleza vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la fidia. Serikalini tunapomhamisha mtu, kwa mfano kama barabara imemfuata mwananchi, Serikali inalipa fidia, lakini kama mwananchi au raia yeyote amevamia barabara, hatuwezi kulipa fidia, na sisi tunasimamia sheria. Ukiangalia kwenye muswada huu tumeeleza *very clearly* kuhusu mambo ya fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye kifungu cha 34(4); "*Acquisition of land and property right during the railway works,*" tumeongea *very clear*. "*A railway order should contain such provision as a Corporation considered necessary or experience for the purpose of the order.*" Then ukienda zaidi

ukisoma mwisho pale namba nne; *“the Corporation should pay compensation equivalent to the value of the land or the other property rights acquired.”* Kwa vile iko *very clear* kwenye Muswada huu tutalipa kutokana na mali iliyoko pale na ndiyo tunavyofanya siku zote Serikalini. Kwenye barabara tunafanya hivyo hivyo na kwenye reli tunafanya hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kwamba tukiandika hizi sheria tunaangalia zaidi maslahi ya nchi. Hatuangalii leo tu, lakini tunaangalia hata miaka kumi mbele kwa sababu *technology* inabadilika na kila kitu kinabadilika, ndiyo maana tunaenda mbele. Kwa hiyo, hilo jambo limeangaliwa vizuri na ninaomba ndugu wananchi na Waheshimiwa Wabunge msiwe na wasiwasi na jambo hilo, liko vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na swali kwamba tuweke kwenye madhumuni ya shirika kwamba ionekane kama ni shirika la kufanya biashara. Wakati wote ukitengeneza shirika, madhumuni makubwa ya shirika ni kufanya biashara. Kufanya biashara maana yake ni faida, vinginevyo hakuna maana ya kutengeneza shirika lolote. Madhumuni yaliyoandikwa kwenye muswada huu tunamini kabisa italifanya *TRA* kutengeneza faida. Jambo tunalotakiwa sisi kama Serikali ni kulisimamia lifanye kazi kutokana na sheria ambayo tunaipendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile muswada huu umetoa maelezo au vifungu mbalimbali vinazungumzia jinsi ya kulipa uwezo shirika linalokuja kuchukua mkopo. Shirika ambalo lilikuwepo zamani ilikuwa haliwezi kufanya mkopo, lakini shirika jipya hili leo litakuwa na uwezo wa kuchukua mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye kifungu cha 6(1)(n) imeeleza *very clear* na kinasema: *“enter into any arrangement with any person or any relevant entity which, in opinion of the Board, shall promote or secure the provision, or improved provision or any service or facility which may separate provide and without prejudice to the generality any*

of the other function.” Ninazungumza kwamba wanaweza kuingia mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ukienda *section 14*, iko *very clear* zaidi. *Section 14(b)* ya muswada huu; “*subject to any other directions which may be given by the Minister the Board may: (b) approve the proposal to borrow money for the purpose of the Corporation.*” Limeruhusiwa au litaruhusiwa kuchukua mkopo kwa ajili ya uendeshaji, kwa ajili ya ujenzi wa miundmbinu. Kwa vile mambo haya yote tumeangalia vizuri na kama Serikali, na yako vizuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu jina *TRC*. Kwa nini tuliamua tuite *Tanzania Railway Corporation (TRC)*? Zamani kulikuwa na *TRC* na watu wote ambao wanakaa Kanda ya Ziwa walikuwa wanasafiri na Shirika hilo la Reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika hilo lilifanya kazi vizuri sana na kila Mtanzania alikuwa ameona kazi iliyokuwa ikifanywa na *TRC*. Baadaye katikati hapo tukaunganisha baina ya *TRC* na kampuni ile ya Wahindi. Bahati mbaya sana ndiyo tukapata *TRL*, lakini kazi iliyofanywa na *TRL* ilikuwa mbaya sana, hairidhishi. Kila mtu siku zote aliyekuwa anakumbuka *TRC*; sisi kama Serikali kwa kuangalia *brand name* nzuri, tukaona hili shirika letu Watanzania wengi bado wanatamani *TRC*, tukaamua tuite *TRC as brand name*. Hii ni *brand name*, tunafanya *marketing*. Tunaamini Watanzania wengi leo wakisikia *TRC* watakupa *TRC* ya zamani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo, tunaamini *TRC* yetu mpya itaweza kufanya kazi kwa ufanisi na itafanya kazi vizuri zaidi kuliko *TRC* ya zamani. Kwa vile *TRC* hii ni mpya kabisa, ina mambo mapya, inakuja na *standard gauge*, inakuja na treni ambayo itakwenda kwa kilometa 160 kwa saa, Watanzania hawajawahi kuona. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache, sasa naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaratibu wetu. Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Reli wa Mwaka 2017
[The Railways Bill, 2017]

Ibara ya 1

Ibara ya 2

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 3

Ibara ya 4

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 5

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 6

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 7

Ibara ya 8

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 23
Ibara Mpya ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 26

Ibara Mpya ya 27

Ibara Mpya ya 28

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 29

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 30

Ibara Mpya ya 31

Ibara Mpya ya 32

Ibara Mpya ya 33

Ibara Mpya ya 34

Ibara Mpya ya 35

Ibara Mpya ya 36

Ibara Mpya ya 37

Ibara Mpya ya 38

Ibara Mpya ya 39

Ibara Mpya ya 40

Ibara Mpya ya 41

Ibara Mpya ya 42

Ibara Mpya ya 43

Ibara Mpya ya 44

Ibara Mpya ya 45

Ibara Mpya ya 46

Ibara Mpya ya 47

Ibara Mpya ya 48

Ibara Mpya ya 49

Ibara Mpya ya 50

Ibara Mpya ya 51

Ibara Mpya ya 52

Ibara Mpya ya 53
Ibara Mpya ya 54
Ibara Mpya ya 55
Ibara Mpya ya 56
Ibara Mpya ya 57
Ibara Mpya ya 58

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 59

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 60
Ibara Mpya ya 61
Ibara Mpya ya 62
Ibara Mpya ya 63
Ibara Mpya ya 64
Ibara Mpya ya 65
Ibara Mpya ya 66
Ibara Mpya ya 67

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 68

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 69
Ibara Mpya ya 70
Ibara Mpya ya 71
Ibara Mpya ya 72
Ibara Mpya ya 73
Ibara Mpya ya 74
Ibara Mpya ya 75
Ibara Mpya ya 76

Ibara Mpya ya 77
Ibara Mpya ya 78
Ibara Mpya ya 79
Ibara Mpya ya 80
Ibara Mpya ya 81
Ibara Mpya ya 82
Ibara Mpya ya 83
Ibara Mpya ya 84
Ibara Mpya ya 85
Ibara Mpya ya 86
Ibara Mpya ya 87
Ibara Mpya ya 88
Ibara Mpya ya 89
Ibara Mpya ya 90
Ibara Mpya ya 91
Ibara Mpya ya 92

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 93

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 94
Ibara Mpya ya 96
Ibara Mpya ya 97
Ibara Mpya ya 98
Ibara Mpya ya 99
Ibara Mpya ya 100
Ibara Mpya ya 101
Ibara Mpya ya 102
Ibara Mpya ya 103
Ibara Mpya ya 104
Ibara Mpya ya 105
Ibara Mpya ya 106
Ibara Mpya ya 107

Ibara Mpya ya 108
Ibara Mpya ya 109

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 110
Ibara Mpya ya 111
Ibara Mpya ya 112
Ibara Mpya ya 113
Ibara Mpya ya 114
Ibara Mpya ya 115
Ibara Mpya ya 116
Ibara Mpya ya 117

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali la 2
Jedwali la 3

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

NDG. JOSHUA CHAMWELA- KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza
kazi yake.

(Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya
28(2) nakusudia kuongeza nusu saa ili tuweze kumaliza kazi
iliyoko mbele yetu. Sasa nitawahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Waliofiki wameshinda, kwa hiyo, tunaendele. Mtoa Hoja, Taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada Ibara kwa Ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Reli ya mwaka 2017 sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Haja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge. Katibu.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Walioafiki wameshinda. Kwa hiyo tunaendelea, Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuanzisha Shirika la Reli Tanzania, kuainisha madhumuni na majukumu yake ikiwemo kusimamia miundombinu ya reli, kutoa huduma za usafiri wa reli pamoja na mambo yanahusiana na hayo *(A bill for an Act to establish the Tanzania Railways Corporation to make better provision for development, maintenance and*

promotion of rail infrastructure, rail transport services and to provide for other related matter).

(Kusomwa Mara ya Tatu)

(Muswada wa Sheria ya Reli Tanzania wa mwaka 2017 (The Railways Bill, 2017) Ulipitishwa na Bunge

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa upande wetu kama Bunge tumekamilisha hii kazi. Nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake walioifanya hii kazi kwa weledi mkubwa na kuweza kuhakikisha kwamba shirika letu linaweza sasa kuanza upya ili litusaidie sisi wananchi na tunayo matumaini makubwa sana.

Nichukue pia fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi kubwa na nzuri mliyoifanya hasa Kamati ya Miundombinu kwa kuweza kupitia muswada huu kwa uangalifu na kuweza kutupa maoni yao ya kuona namna bora ya kwenda nalo hili jambo. Serikali imefanya marekebisho kwenye maeneo kadhaa kwa kupitia mawazo ya Waheshimiwa Wabunge waliyokuwa wameyatao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu. Tuwatakie kila la heri upande wa Serikali kwenye utekelezaji wa sheria hii pale ambapo itakuwa imeshapata Kibali cha Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Katiba yetu Ibara ya 97.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge muswada huu umeshapitishwa leo na Bunge, Muswada wa Sheria ya Reli ya mwaka 2017 *(The Railways Bill, 2017)*. *(Makofi)*

Sasa kabla sijaahirisha Bunge, Waheshimiwa Wabunge nina maneno machache kuhusu miswada ya dharura. Jambo hili limekuwa likijirudia kila wakati, sasa ni vizuri hata kama tunazungumza tuwe tunazungumza tukiwa wote tuko kwenye uelewa ulio sawasawa.

Kanuni zetu zinaweka utaratibu wa kutumia Hati ya Dharura, lakini Kanuni hizo hizo zimeweka masharti ya matumizi ya Hati ya Dharura. Sasa mimi naamini Bunge lilitumia hekima kwa kuona kwamba kuna wakati Waheshimiwa Wabunge watatakiwa kuangalia Miswada kwa hali ya dharura na masharti yamewekwa ili isiwe kila jambo litahesabiwa kwamba ni la dharura.

Sasa inatokea kila wakati tunalizungumzia hili jambo kana kwamba huwa linatolewa mahali na kuletwa kwetu na sisi tunaenda nalo tu namna hiyo, hapana. Kanuni yetu ya 80 imeweka utaratibu na masharti. Sasa masharti hayo yakitimizwa, sisi Wabunge tukionekana tena tunalalamikia, basi tulalamikie Kanuni zetu, ili tuzitengeneze zikae sawa. Kwa sababu tukiwa tunalalamika, ni sisi wenyewe tulioweka haya masharti na tumeweka haya masharti kwa kuangalia mazingira tuliyonayo.

Sasa kwa kifupi, ili tuwe tunaenda wote sawasawa hata tunapotaka kuleta hoja hii ni kwamba masharti ya msingi yako matatu. Moja ni kwamba hati ni lazima isainiwe na Mheshimiwa Rais. Hati ya Dharura lazima isainiwe na Mheshimiwa Rais. Ikishasainiwa na Mheshimiwa Rais, inaenda kwanza Kamati ya Uongozi ili Kamati ya Uongozi ijiridhishe.

Sasa Kamati ya Uongozi siyo ya Serikali, ni ya Bunge hili, kwa sababu ni viongozi wale ambao tumewachagua wenyewe kwa kuwaamini kwamba wakakae katika Kamati ya Uongozi, ndio wanaokaa huko na wako viongozi wa pande zote zilizoko humu Bungeni.

Kwa hiyo, tunapolizungumzia hili jambo la dharura, siyo kwamba linakuja tu. Sasa Kamati ya Uongozi ina maamuzi, siyo lazima ikubaliane na ile Hati ya Dharura, inaweza ikaridhia ama ikakataa. Sasa ile Kamati ikiridhia, lile jambo linafuata sasa yale masharti ambayo yamewekwa katika Kanuni ya 93.

Sasa tusiwe tunalizungumza hili jambo mpaka wananchi wetu wakawa watushangaa kwamba hawa

Wabunge siku hizi huwa wanafanyaje kazi? Kwa hiyo, utaratibu wa Hati ya Dharura ni kwamba Muswada utaangaliwa kwa kipindi hicho hicho cha Bunge ambalo Hati imeletwa, lakini itafuata utaratibu wote. Isipokuwa hausomwi tu katika vipindi vya Bunge tofauti. Kwenye Bunge hilo hilo, lakini utaratibu lazima ufanywe, ndiyo maana Kamati zinasoma taarifa hapa kwa maana ya kwamba zilipewa hiyo kazi, zimeifanyia kazi na zimeleta hilo jambo.

Kwa hiyo, hata sisi tunapotaka kulieleza katika taarifa zetu, lazima tulieleze kwa namna hiyo, kwa sababu, sisi ni Wawakilishi wa wananchi na wananchi wanatuamini kwamba tunafanya kazi ya kutunga sheria. Kama tunataka kuonesha kana kwamba hatutungi sheria kwa sababu jambo limeletwa kwa Hati ya Dharura, hapana. Sisi wenyewe ndio tulioruhusu Hati ya Dharura kwa kutumia Kanuni zetu. Kwa hivyo, kama sisi wenyewe ndio tulioruhusu, basi tumeona umuhimu wa jambo hilo.

Jambo la tatu ni kwamba Kamati ya Bunge lazima iifanyie kazi hiyo sheria hata kama imekuja kwa Hati ya Dharura. Kwa hiyo, mambo haya tunapoyazungumza kwenye ripoti zetu upande wa Kamati, lakini pia upande wa Kamati Rasmi ya Upinzani tuwe tunaangalia muktadha wa Kanuni zetu namna zinavyosema. Tukianza kuzilalamikia sisi wenyewe, sisi ndio tuliotengeneza na sisi ndio wenye uwezo wa kuzibadilisha pale tunapoona zinasumbua.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Alhamisi, tarehe 14 Septemba, 2017 Saa Tatu Asubuhi.

(Saa 7.00 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 14 Septemba, 2017, Saa Tatu Asubuhi)